Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 3 Februari, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA MASOKO:**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Ushindani kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 [*The Annual Report and Audited Accounts of Fair Competition Commission for the Financial year 2009/2010]*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Taarifa ya Serikali ya Utekelezaji wa Azimio la Bunge juu ya Uendeshaji wa Sekta Ndogo ya Gesi Nchini.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 39

**Uwekezaji wa Kibiashara wa Nchi ya Libya Tanzania**

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI** aliuliza:-

Aliyekuwa Kiongozi wa Libya Marehemu Kanali Muamar Gaddafi, alijulikana sana kwa kuwekeza mabilioni ya dolla kwenye nchi mbalimbali za Kiafrika, kibiashara na kijamii kama hoteli, barabara na misikiti:

(a) Je, Tanzania ilifaidikaje na uwekezaji wa Gaddafi kibiashara hapa nchini?

(b) Kwa kuwa, Serikali ya Tanzania haitambui Serikali ya mpito ya Libya. Je, ni nani anayesimamia uwekezaji wa biashara wa Marehemu Kanali Gaddafi hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, mabadiliko hayo hayabadilishi maudhui ya swali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo katika Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)*, Marehemu Kanali Muammar Gaddafi hakuwahi binafsi kuwekeza kibiashara hapa nchini.

Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo katika Kituo cha Uwekezaji Nchini *(TIC)*, kuna mradi mmoja tu uliandikishwa kutoka nchini Libya na Kampuni ya *North Africa Investment Trading Company*. Uwekezaji huu ni wa kampuni kutoka Libya, siyo wa Kanali Muammar Gaddafi, binafsi kama swali la msingi lilivyouliza.

Jina la mradi uliowekezwa ni *Bahari Beach Hotel Ltd.* ambao una wanahisa wafuatao:-

(i) Bwana Abdallah O. Hiblo (Hisa 33.34%).

(ii) Bwana Mohamed O. Gmat (Hisa 33.33).

(iii) Bwana Hussein A. Omrani (Hisa 33.33%).

Kampuni hiyo ilinunua Hoteli ya *Bahari Beach* kupitia *Presintial Parastatal Sector Reform Commission* mwaka 1998. Kampuni hiyo iliwasilisha andiko la biashara la kuwekeza jumla ya dola za Marekani milioni 5.8 na pia kutengeneza nafasi za ajira 160.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Marehemu Kanali Muammar Gaddafi, hakuwekeza kibinafsi kibiashara hapa nchini, hakuna anayesimamia uwekezaji wake kwa kuwa haupo.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

(i) Hiyo *organisation* iliyotajwa kwamba ndiyo imewekeza katika *Bahari Beach Hotel* ilikuwa ni ya Serikali kwa maana ilikuwa chini ya Serikali ya Kanali Muammar Gaddafi. Bado nafahamu Serikali imesema kwamba haitambui utawala mpya wa waasi *(NTC)*. Kwa hiyo, bado nilitaka kujua yale maslahi ya iliyokuwa Serikali ya Gaddafi yanasimamiwa na nani sasa hivi kwa sababu Serikali ya Tanzania haiitambui Serikali ya sasa hivi ya Libya?

(ii) Nafahamu kwamba, Serikali hii ilikuwa na urafiki na Kanali Muammar Gaddafi na inafahamika kwamba, Tanzania kwa muda mrefu imekuwa maarufu kwenye medani za kimataifa hasa Barani Afrika katika kushawishi.

Je, Serikali hii ya Tanzania ilishawishi vipi marafiki zake wengine wa AU (Nchi za Afrika) kwenda kumsaidia Gaddafi dhidi ya uvamizi wa *NATO* kama ilivyokuwa inasemwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Joseph Osmund Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini, kwa maswali yake mawili ya nyongeza.

Nikianza na swali la kwanza kwamba, kampuni hii iliyowekeza ni ya Serikali ambayo ilikuwa chini ya Mheshimiwa Muammar Gaddafi wakati ule akiwa hai! Ninachojua ni kwamba, Serikali ya Tanzania kama moja ya nchi ambazo ziko chini ya Umoja wa Afrika, ilikuwa na uhusiano na nchi ya Libya.

Sasa uhusiano huu wa Serikali hizi mbili hauwezi kuwa wa kibinafsi, ni wa Serikali na Serikali. Kwa hivyo, bado nasisitiza swali la msingi linauliza kama Muammar Gaddafi aliwekeza. Hakuwekeza ni kampuni ambayo nimeitaja na wenye hisa ndiyo imewekeza na kama kampuni hiyo bado ipo basi itafuata taratibu ambazo zinakubalika kitanzania kufuatilia uwekezaji huo.

Swali la pili kwamba, Serikali ilikuwa ni rafiki wa Muammar Gaddafi! Nako kama swali la msingi lilivyojielekeza nisingependa kuhusisha Serikali na mtu binafsi Marehemu Muammar Gaddafi. Serikali hizi mbili kama zilivyokuwa chini ya Umoja wa Nchi za Afrika zilikuwa na uhusiano kwa vyovyote na kwa hivyo naomba uhusiano huu usiwe wa mtu binafsi na Serikali bali wa Serikali zetu mbili.

**NAIBU SPIKA:** Nilimwona Mheshimiwa Zitto Kabwe, swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana kuona kwamba, Serikali yetu inaweza kuwa na *opportunistic diplomatic relations*. Inafahamika wazi kabisa Serikali iliyokuwa ikiongozwa na Kanali Muammar Gaddafi ilikuwa na uhusiano wa karibu sana na Tanzania. Inafahamika wazi kabisa kwamba, *LAICO* (*Libya Arab Investment Company*) ni moja ya kampuni ambazo zimewekeza si tu Tanzania, bali katika nchi nyingi sana za Afrika.

Kwa ushauri wa nchi kubwa, nchi za mabeberu, nchi za *NATO,* iliagizwa kwamba, mali zote za *LAICO* ambazo Gaddafi na Serikali yake wamewekeza ndani ya Afrika ziwe *freezed*. Napenda kufahamu Serikali ya Tanzania ili-*freeze*? Kama ili-*freeze,* fedha ambazo Serikali ya Libya iliisamehe Serikali ya Tanzania kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya Sementi iko wapi na iliwekezwa katika *Tanzania Investment Bank?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zitto Kabwe, kama ifuatavyo.

Kwanza ninapinga kwa nguvu zote kwamba Serikali yetu ya Tanzania ina *opportunistic diplomatic relations*. *(Makofi)*

Nafikiri Mheshimiwa Zitto mwenyewe asingependa hilo na ndivyo ilivyo kwamba, sisi tunahusiana na nchi zingine zikiwemo ambazo ziko kwenye Umoja wa Afrika kwa taratibu ambazo zinakubalika kwa nchi ambayo ni *independent*, ni *autonomous* na ina uamuzi wake yenyewe kufuatia taratibu za kimataifa ambazo zinakubalika. Kwa hivyo, naomba tufute kauli hii kabisa kwamba, tuna *opportunistic diplomatic relations*. *(Makofi)*

Pili kwamba, kulikuwa na makampuni ya Libya ambayo yaliwekeza. Yaliwekeza kibiashara na yalifanya hivyo kwa sababu tuna uhusiano unaokubalika wa nchi na nchi. Kwa sababu sisi ni nchi huru na inayojitegemea sitegemei kwamba, tunapokea amri kutoka nchi zingine au makampuni au Mashirika ya Kimataifa. (*Makofi*)

Na. 40

**Kufungwa kwa Barabara ya Kongowe – Bagamoyo**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Barabara ya kutoka Kongowe - Bagamoyo ambayo ni fupi na imefanya uchumi wa maeneo hayo kuchangamka lakini imefungwa katika mazingira tata.

(a) Je, Serikali ina sababu gani za msingi za kuifunga barabara hiyo?

(b) Je, ni lini sasa barabara hiyo itafunguliwa ili kuchochea shughuli za kiuchumi kati ya Kongowe na Bagamoyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kutoa maelezo ya ufafanuzi kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kongowe – Bagamoyo ni barabara inayounganisha Wilaya ya Kibaha na Bagamoyo.

Barabara hii inakatisha Halmashauri mbili ambazo ni Halmashauri ya Mji Kibaha na Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo. Kwa upande wa Halmashauri ya Mji Kibaha barabara hii ina urefu wa Km. 13.8 kutokea Barabara Kuu ya *TANZAM Highway* hadi mpakani mwa Wilaya ya Bagamoyo ambapo ina urefu wa Km. 11.1 uzio ulio ndani ya Msitu wa Hifadhi ya Taifa Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msitu huu wa Hifadhi ya Taifa unalindwa na Sheria ya Misitu Namba. 14 ya mwaka 2002, *Cap* 323 ambayo imeweka utaratibu wa namna ya kuingia na kutoka ndani ya msitu kwa kuweka viwango vya ushuru kama ilivyoonyeshwa katika Gazeti la Serikali Na. 429 la tarehe 9 Desemnba, 2011 likisomwa pamoja na Tangazo la Serikali Na. 153 la mwaka 2004. Aidha, kipande cha barabara chenye urefu wa km. 2.7 kutoka barabara kuu ya TANZAM hadi *Check Point* ya kuingiza msituni kimekuwa kikifanyiwa matengenezo kwa ushirikiano kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na Chuo cha Utafiti wa Misitu kilichopo Kibaha.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo mafupi naomba kujibu swali la Mheshimwa Silvestry Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Serikali imeweka kizuizi katika baraara hii kwa mujibu wa sheria ya misitu Na. 14 ya mwajka 2002 ili kuzuia wizi na uharibifu unaofanywa na watu wanaopita ndani ya msitu ambao baadhi yao ni waharibifu.

(b) Kama ilivyoelezwa hapo juu kizuizi hicho kimewekwa kisheria na kipo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii, nia na shabaha ya kizuizi hicho ni kulinda Msitu wa hifadhi na maliasili iliuopo ndani.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa barabara hii ipitayo *Forest* – Bana- Yombo hadi Bagamoyo ni kiungo muhimu kati ya mji wa Kibaha na Bagamoyo, na kwa kuwa ni kichocheo cha uchumi kati ya miji hii miwili.

(a) Serikali sasa haioni kwa kufanya hivyo imeendelea kudhoofisha jitihada za kukuza miji hii midogo inayoendelea kukua?

(b) Ni kwanini sasa Serikali isichukue hatua ya kuwashirikisha wananchi wanaotumia barabara hizi ili kuweza kulinda misitu hii kwa kuwafanya wahusika na walinzi shirikishi ili wananchi hawa waweze kuendelea kuitumia barabara hii na iweze kuleta manufaa makubwa katika uchumi wa miji hii miwili kinyume na jinsi ambavyo tunaona misitu mingine muhimu na hata Mbuga za Wanyama barabara zikipita bila tatizo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *concern* ya Mbunge anayoileta hapa ninaiona, lakini sasa anazungumza habari ya uchumi. Kama unazungumzia habari ya uchumi hapa unaangalia uchumi katika mapana yake.

Uchumi unakuonesha jinsi watu wanavyozalisha na jinsi ambavyo wanagawanya mali na vitu vingine. Msitu huu niliousema hapa ni muhimu sana na ninyi wote Waheshimiwa Wabunge mnajua kwamba, tusipokuwa waangalifu sana na namna tunavyohifadhi misitu yetu tutapata matatizo makubwa na msitu ule ukienda ukifa maana yake ni kwamba, hakuna maji pale na hakuna kitu chochote na wananchi wa Kibaha wanaoishi katika eneo lile watahama pale.

Sasa sijui kama kuna uchumi zaidi ya huo. Yaani unachoangalia hapa ni kwamba, hifadhi ile imewekwa pale na vizuizi vyote vimewekwa pale ili kuzuia na kuhakikisha kwamba, ile hifadhi inabaki pale na mvua ziweze kunyesha na mambo mengine. Ndiyo msingi wa jambo hili linalozungumzwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba imeathiri mambo ya uchumi na nini. Ni kweli kwamba, watu wanatakiwa kuzunguka sasa kwenda mpaka Mlandizi. Hii sihitaji kwenda chuo kikuu kuelewa jambo hilo. *Simple knowledge* tu inatosha kukuambia kwamba ukatishe hivyo. Lakini unafanya nini? Wanasema kupanga ni kuchagua. Tunachokiona hapa na ambacho

tunakitetea ni kwamba, msitu ule *the moment* unakuwa *loose* na Sheria, ukaacha watu wanakatisha tu pale, huna msitu pale *and therefore* huna watu wa Kibaha pale. Kwa hiyo, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili hili na namna ya kuwashirikisha. Mwanafunzi wa Sheria aliulizwa *what is law?* Akasema; "*Law is simple common sense*". Ndiyo! (*Kicheko*)

Sasa tunachozungumza hapa ni jambo la kawaida tu hivi, kwamba tunachohitaji kufanya hapa ni kwenda kuwaelimisha wananchi wetu kuhusu Sheria hii kwamba tumeiweka pale ili izuie hali ya uharibu isije ikatokea katika msitu ule.

Mimi namwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko tayari kama Wizara kwenda kukaa naye ili tuone jinsi ambavyo tunaweza tukawaelimisha wananchi kuhusu Sheria hii ili jambo hili liweze kutekelezwa kama linavyosemwa.

Na. 41

**Mgogoro wa Ardhi Babati Mjini**

**MHE. PAULINE PHILIPO GEKUL** aliuliza:-

Mgogoro wa ardhi katika Jimbo la Babati Mjini hasa Kata ya Bagara Ziwani na Komoto umedumu kwa muda mrefu sasa. Halmashauri ya Mji wa Babati imeshindwa kutatua mgogoro huo kwa kushindwa kuwalipa wananchi husika fidia stahiki:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya Halmashauri hiyo iliyoshindwa kulipa haki za wananchi hao na kuhatarisha hali ya amani kwenye maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 eneo la Mtaa wa Bagara Ziwani, Kata ya Bagara lilipimwa na kupewa jina la Kitalu "AA". Uthamini ulifanyika mwaka 2004 na kuidhinishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali mwaka 2005. Uthamini huo unajumuisha pia eneo la Mtaa wa Miomboni. Jumla ya wananchi 214 walifanyiwa uthamini (Mtaa wa Bagara Ziwani wananchi 180 na Mtaa wa Miomboni wananchi 34). Polisi Mkoa wa Manyara waliomba na kugawiwa kiwanja. Kwa ajili ya ujenzi '*barracks*' na walilipa jumla ya Shs. 50,597,332.28 kwa ajili ya kuwalipa wananchi husika fidia (Shs. 42, 612,426.00) na upimaji wa eneo (Shs. 7,984,906.28).

Shilingi 17,996,168.00 zililipwa fidia kwa wananchi 14 wa maeneo ya Mitaa ya Maisaka A, Mrara na Komoto na Shilingi 12,361,339.40 zililipwa kwa wananchi 16 wa eneo la Mtaa wa Bagara Ziwani. Shilingi 14,875,882.00 zilizotengwa kwa ajili ya kuwalipa wananchi 10 wa Mtaa wa Bagara Ziwani hazikuchukuliwa na wahusika kwa madai kuwa fidia hiyo ni ndogo na kutaka kupewa viwanja vyote kwenye maeneo yao yaliyopimwa. Pia wananchi 15 wa Mtaa wa Komoto walikataa kuchukua fidia ya kiasi cha shilingi 8,907,408 kwa madai ya kupatiwa viwanja vyao vyote vilivyopimwa kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2009/2010 sehemu ya eneo la Mtaa wa Komoto ambayo ilikuwa haijapimwa, ilifanyiwa uthamini na vilipimwa viwanja 630. Wananchi 71 walilipwa fidia kiasi cha shilingi 116,685,288. Wananchi 38 walipewa viwanja kama fidia. Wananchi 22 walikataa kuchukua fidia kwa madai kuwa wapewe viwanja vyao vyote vilivyopimwa kwenye maeneo yao. Wananchi hao wamefungua kesi Namba 23/2009 katika Mahakama ya Ardhi Kanda ya Arusha. Kesi hiyo inaendelea na imepangwa kusikilizwa tena tarehe 26 Machi, 2012. Serikali inasubiri uamuzi utakaotolewa na chombo hiki cha Kisheria.

**MHE. PAULINE PHILLIPO GEKUL**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa tatizo hili la mgogoro wa ardhi kwa wananchi wa Babati ni la muda mrefu vile ambavyo Naibu Waziri alivyokiri kwamba limeanza tangu mwaka 2004 takriban miaka 8 sasa tatizo hilo halipatiwi ufumbuzi.

Kwa kuwa wananchi wa maeneo tajwa yaani wananchi wa Negamsii, Komoto na Maisaka wamekosa imani kabisa na Halmashauri yao kwanza kwa kwenda wao kupima maeneo ya wananchi bila ya kuwashirikisha, lakini pili wananchi kutokulipwa fidia stahiki. Je, Serikali au Wizara ya TAMISEMI iko tayari kushirikiana na Wizara ya Ardhi kwenda Babati kukutana na wananchi hao ambao wamekosa imani kabisa na Halmashauri ili hatimaye kero zao hizo ziweze kutatuliwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge ametuonyesha kwamba kuna tatizo pale Babati. Tulisema hapa juzi kwamba hatutampuuza Mbunge wa aina yoyote. Ameonyesha jambo hili tulizungumza na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Mkoa amekiri kwamba kuna tatizo pale, nimezungumza na Mkurugenzi Mtendaji anaitwa Stella yuko Arusha kwenye Semina anakiri na yeye anasema kweli kuna tatizo pale.

Tumezungumza na viongozi wote pale kimsingi wanakubali kwamba kuna tatizo pale. Nimetoa takwimu zote hapa ambazo zinatakiwa na Mheshimiwa Gekul nafikiri umezisikia takwimu nilizokupa hapa. Anasema sisi na Wizara ya Ardhi tushirikiane twende pale Babati tukaliangalie tatizo hili. Hatuna tatizo kabisa na jambo hili. *(Makofi)*

Tutazungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, tutazungumza na Mheshimiwa Mkuchika ili tupate kibali cha kwenda pale. Lakini *minus* jambo lifuatalo. Pale Komoto shauri lile Mheshimiwa Gekul anisikilize vizuri liko Mahakamani *our Government is a Westminster model, whereby the judiciary, executive* na *legislature*. Hili suala tukienda pale hatutaligusa kwa sababu liko Mahakamani. Kwa hiyo, tunakwenda kushughulika na haya masuala yote yaliyozungumzwa hapa hatuna tatizo kabisa na hilo tutakwenda sisi Babati kama alivyoomba tutapeleka kwanza wataalam na baadaye tutakwenda sisi wenyewe.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilikuwa naomba kuuliza. Je, Serikali haioni kwa sababu sheria inairuhusu kutoa maeneo ya watu kwa ajili ya matumizi mbadala.

Sasa fidia wanapochelewesha kwa mfano hii ya Babati, Babati Mjini, Babati Vijijini, maeneo kule Gaitamaro jirani na *TANAPA*. Je, Serikali haioni unapochelewesha sheria hiyo hiyo inasema kwamba unatakiwa kulipa fidia stahiki kutokana na (*market value)* bei iliyopo sokoni. Hao wananchi wanachopinga pale ni ile fidia waliyolipwa ni ndogo kutokana na ile bei iliyopo ya *market value*. Serikali haioni kwamba utakapochelewesha na pindi utakapopata fedha ilipe kutokana na bei ya *market value* iliyopo wakati huo watakapolipa fidia? (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jitu kwa swali zuri.

**NAIBU WAZIRI ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi na. 4 ya mwaka 1999 kifungu cha 3 kikisomwa pamoja na Sheria ya Mipango Miji Na. 8 ya mwaka 2007 inasema kwamba ni kweli kuwa ardhi inapotwaliwa italipiwa fidia inayolingana na hali ya soko ya ardhi kwa wakati huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inapofanya uthamini wa ardhi kwa madhumuni ya kuendeleza au kujenga mji inazingatia vigezo vyote hivyo vimeelezwa katika sheria zote mbili. Pia Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 inasema kwamba "Ikiwa fidia imechelewa kulipwa kuanzia tarehe ilipoidhinishwa basi kwa kila mwaka ambayo imechelewa kwamba uthamini utafanyika ili kuhakikisha fidia inakwenda na thamani ya wakati ule, lakini thamani itakayoongezwa haitazidi asilimia 6 ya thamani ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ardhi ya Babati kama tulivyoeleza na kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri thamani yake ilithaminiwa iliidhinishwa mwaka 2005 basi itakapofika wananchi wale wako tayari kulipwa Serikali itatazama hivyo kwa kuzingatia sheria hiyo.

Na. 42

**Huduma ya Maji Safi na Salama Kondoa Kaskazini**

**MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MHE. ZABEIN M. MHITA)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kuwa wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini wanapata huduma ya maji safi na salama ili waondokane na kero mbalimbali wanazozipata?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mbunge wa Kondoa Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya maji safi na salama katika Wilaya ya Kondoa ni mita za ujazo 12,485.2 kwa siku wakati upatikanaji wa maji hayo ni mita za ujazo 4,244.95 kwa siku. Hivyo nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa upo upungufu wa upatikanaji wa maji ambao ni sawa na mita za ujazo 8,240.25 kwa siku.

Aidha, Jimbo la Kondoa Kaskazini lina visima vya maji 35 na kati ya hivyo vinne (4) havifanyi kazi, miradi ya maji mtiririko katika vijiji 22 na visima vifupi katika vijiji 9. Kwa kuzingatia hali hii, Serikali imeweka mipango mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama ili kutosheleza mahitaji yaliyopo. Mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Uchimbaji wa visima vitano (5) katika Jimbo la Kondoa Kaskazini katika vijiji vya Choka, Madisa, Soera, Kwadelo na Kirere cha Ng'ombe kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji *(WSDP)*. Utekelezaji wa miradi hii ni kutokana na bakaa ya fedha za Programu cha shilingi milioni 160.3 za mwaka 2010/2011.

Aidha, kimechimbwa kisima cha maji katika kijiji cha Songolo ambacho kimepata maji ya chumvi. Halmashauri imeazimia kutumia shilingi milioni 5.5 kwa ajili ya kujenga mradi wa uvunaji wa maji ya mvua katika kijiji hicho ili kuondoa tatizo hilo.

*(ii)* *Belgium Fund for Food Security* imechimba kisima katika Kijiji cha Kondomairo kwa gharama ya shilingi milioni 45.0. Kazi zinazoendelea ni usanifu ili kujenga miundombinu ya maji.

(iii) Kupitia *TASAF,* Serikali inategemea kukamilisha miradi ya maji ya visima virefu katika Vijiji vya Tumbelo, Ororimo na Kwadinnu na vimepata maji ya kutosha. Kazi zinazoendelea ni ununuzi wa pampu na kuzifunga. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa shilingi milioni 204.9 ili kukamilisha kazi hizo.

(iv) Katika mwaka 2011/2012, Halmashauri imeweka mpango wa kujenga miradi ya uvunaji maji ya mvua katika taasisi tano (5) kupitia fedha za Ruzuku ya Maendeleo katika Serikali za Mitaa (LGCDG) kiasi cha shilingi milioni 320. Aidha, visima viwili vitachimbwa katika eneo la Bicha ili kuongeza wingi wa maji katika maeneo ya Bomani, Kwapakacha na Dama.

(v) Kupitia *TANAPA,* Halmashauri imechimba kisima kirefu katika Kijiji cha Chubi ambacho kinapakana na mbuga ya Tarangire kilichoko katika Jimbo la Kondoa Kaskazini. Jumla ya shilingi milioni 25.0 zitatumika kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa hapo juu, ni dhahiri kwamba Serikali inachukua hatua za dhati kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma za maji safi na salama katika jimbo la Kondoa Kaskazini.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:**Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nina imani kabisa Mheshimiwa Zabein ataridhika na majibu ambayo Mheshimiwa Waziri ameyatoa. Hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kama ilivyotokea katika kijiji cha Songolo huko Kondoa, kisima kimechimbwa lakini maji yaliyopatikana ni ya chumvi. Hii nina maana kwamba kuna matatizo katika teknolojia ya utafutaji maji. Lakini kuna Chuo Kikuu kipya cha Nelson Mandela, kimeanzishwa kule Arusha kina sehemu ya sekta hii ya maji.

Je, Wizara inasema nini kuhusu namna ya kuboresha na kuwezesha chuo hicho kusaidia katika kuondoa tatizo hili ambalo linatugharimu fedha nyingi?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni kwamba bado kuna matatizo makubwa katika Halmashauri nyingi hasa ikiwemo Halmashauri ya Wilaya Muheza kwa watendaji wale wa Idara ya Sekta ya Maji kwamba uwezo wao ni mdogo.

Je, TAMISEMI kama sehemu inayosimamia Halmashauri inatoa ushauri gani wa kuwezesha Halmashauri kupata watendaji wazuri ili kupunguza gharama ambazo tunazipata katika utafutaji wa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nakubaliana naye kwamba yapo maeneo ambayo tunachimba maji halafu unakuta yale maji hayana kiwango ambacho kinakubalika kwa matumizi ya binadamu. Kwa mfano ukikuta kama yana chumvi asilimia kubwa ambayo hairuhusiwi. Sasa hili si suala la utaalamu vipimo ambavyo tunakuwa navyo ni kujua kwamba maji yapo.

Sasa ukishayapata maji yale lazima tuyapime. Kwa hiyo, hatuna vipimo kujua kabisa kwamba tukichimba chini huko tutakuta maji yenye kiwango fulani cha ubora. Kwa hiyo hilo linatokea baada ya kwamba tumeshapima, tunaangalia tunakuta maji yale hayafai.

Kuhusu kituo cha Nelson Mandela, ni kweli vipo vinafanya utafiti namna ya kupata maji chini ya ardhi. Sasa vipimo ambavyo tunavitumia sasa hivi vinaonyesha unyevuunyevu yaani haina ya ile miamba, kwa hivyo suala la kuwa na maji ya kiwango linategemea na jiolojia ya eneo lile.

Sasa tunaendelea kuboresha vipimo na unabidi uchukue eneo kubwa sio eneo la kijiji kile uchukue mwamba ule historia yake ina-*cover* eneo kubwa ndio unaweza ukajua maeneo fulani utapata maji ya kiwango cha aina fulani. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILLINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nina swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizopo katika Maziwa Makuu na kwa kuwa Tanzania ina vyanzo vingi vya maji tofauti na nchi za Misri, Libya ambazo ziko katika majangwa. Je, Serikali sasa inaweza kutueleza ni kwa nini imeshindwa kwa takriban miaka 50 kuondoa kero ya maji ambayo maeneo mengi ya Tanzania yamekuwa ikiikabili?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:**Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Tanzania ina rasilimali za maziwa mengi. Tunaposema kwamba sio tumeshindwa kutoa maji kwa wananchi. Ni kwamba tumesema tunajenga ile *capacity* ya vijiji. Tunaposema tunashirikisha vijiji katika kukua na miundombinu ya maji tunachukua teknolojia tumeanza na hii ya visima.

Tumejua tukichukua teknolojia ya visima tutachukua eneo kubwa kwa muda mfupi. Lakini baada ya kuona kwamba kwenye visima kumekuwa na matatizo sasa tunaanza kujenga uwezo wa kibajeti ili tuanze kuchukua maji kutoka kwenye maziwa ili tuweze ku-*cover* maeneo mengi zaidi. *(Makofi)*

Na. 43

**Leseni za Viwanda Kuwa Jambo la Muungano**

**MHE. SULEIMAN NASSOR OMARI (K.n.y. MHE. HUSSEIN MUSSA MZEE)** aliuliza:-

Kwa mujibu wa nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, leseni za viwanda ni jambo la Muungano:-

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni hoja gani zilijengwa mpaka jambo hilo likawa la Muungano wakati shughuli za maendeleo ya viwanda si jambo la Muungano?

(b) Je, ni faida gani zimepatikana juu ya uamuzi huo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, swali lake lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 1967 Sheria Na. 10 ya kusajili na kusimamia viwanda vya Taifa, ilitungwa. Sheria hii haikuwa ya Muungano mpaka mwaka 1982 sheria hiyo ilipofanyiwa marekebisho kuwa ya Muungano. Hii ni kwa sababu, Serikali iliona kuna umuhimu wa kuwa na uwiano katika maendeleo ya viwanda Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwepo kwa sheria hii, mafanikio yake hayakuwa makubwa sana kutokana na nchi yetu kufanya maamuzi ya kuwa na soko huria miaka 4 tu baadaye yaani mwaka 1986. Hivi sasa viwanda vingi Zanzibar vinasajiliwa kupitia Sheria ya Uwekezaji Zanzibar chini ya *ZIPA (Zanzibar Investment Promotion Agency*).

Kutokana na mabadiliko ya Sera za Viwanda *(Import Substitution and Basic Industry Strategy),* Baraza la Wawakilishi lilipitisha Sheria ya Uwekezaji Zanzibar mwaka 1997 ili kuanzisha Kituo cha Uwekezaji Zanzibar ambacho kilichukua majukumu ya masuala ya uwekezaji na usajili wa Viwanda Zanzibar. Kwa kuzingatia mabadiliko hayo, Sheria ya Usajili wa Viwanda inahitaji mapitio ili iendane na mazingira ya sasa ya biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mazingira hayo niliyoyaeleza hapo juu, Sheria ya Usajili wa Viwanda Na. 10 ya mwaka 1967 na marekebisho ya Sheria Na. 13 ya mwaka 1982 ni miongoni mwa sheria ambazo zipo kwenye mpango wa kufanyiwa marekebisho na Serikali ili iendane na mazingira ya sasa ya uwekezaji katika sekta ya viwanda. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN NASSOR OMAR**: Mheshimiwa Naibu Spika, nina suala dogo la nyongeza.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Muungano zote zina maeneo ya *EPZ.*

Je, kuna ushirikiano gani baina ya *EPZ* hizi mbili katika kuendeleza maeneo hayo?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema kwamba tunayo maeneo ya *EPZ* Zanzibar, tunayo maeneo ya *EPZ* Tanzania Bara na upo ushirikiano mkubwa sana kati ya taasisi hizi mbili. *ZIPA* ambayo imenzishwa mwaka 1997 ndiyo imekuwa inaendeleza kwa upande wa Zanzibar ushirikiano mkubwa wa *EPZ* ya Tanzania Bara ambayo nayo imeanzishwa si siku nyingi sana. Katika ziara zote za viongozi wa wajuu wanapokwenda nje kwa ajili ya kuhamasisha wawekezaji Tanzania kila kwenye msafara utakuta kuna mwakilishi wa *ZIPA* na mwakilishi wa *EPZ* kwa upande wa Tanzania Bara na wote wanapata fursa ya kusemea pande zote mbili za Muungano kuhusu fursa za uwekezaji katika viwanda na katika maeneo mengine katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hivyo tu, yapo mambo mengine ambayo tuna mashirikiano mazuri. Kwa mfano kwenye *Tanzania Bureau of Standards*, maana yake ubora wa bidhaa ndiyo unafanya bidhaa ile inauzika zaidi nje. Kwa hiyo, kazi ya *ZIPA* na kazi ya *EPZ* haitakuwa na manufaa makubwa kama hatutakuwa na ubora katika maeneo yote mawili ya Muungano. *TBS* kwa upande wa Tanzania bara imekuwa na ushirikiano mzuri sana na upande wa pili wa Muungano hadi sasa Zanzibar imeanzisha *Zanzibar Bureau of Standards* ambayo sasa hivi *TBS* inafanya kazi ya kuhakikisha kwamba wanafanya

mashirikiano ya karibu kuhakikisha kwamba *ZBS* inakuwa na nguvu kama *TBS* kwa upande wa Tanzania Bara.

Lakini vilevile Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka mara zaidi ya moja mmetaka *SIDO* ambayo iko upande wa Tanzania Bara iweze kutoa ushauri wa namna ya kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo upande wa pili wa Muungano na Wizara ya Viwanda na Biashara haijasita kuiagiza *SIDO* ishirikiane na Wabunge, ishirikiane na upande wa pili wa Muungano kuhakikisha kwamba maendeleo ya viwanda Zanzibar yanainuka na Maendeleo ya viwanda yakiinuka basi hata kazi ya *ZIPA* na *EPZ* ambayo ndiyo kazi kubwa wanaifanya yaku-*promote* uwekezaji katika pande zote mbili za Muungano inakuwa rahisi.

**MHE. TUNDU A. LISSU**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kama nimesikia majibu sawasawa ya Mheshimiwa Waziri ni kwamba masuala yote ya *Industrial Licensing* na *Statistics* kwa upande wa Zanzibar yanatekelezwa na mamlaka ya Zanzibar ikiwemo *ZIPA;* na kwa mujibu wa Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, masuala haya ni masuala ya Muungano yanayotakiwa yatekelezwe na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Sasa Waziri anataka kutuambia kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano imekuwa inavunjwa?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama nilivyosema mwanzoni kwamba sasa hivi masuala ya Usajili wa Viwanda Zanzibar yanafanywa kupitia *ZIPA* na suala hili liliamuliwa kutokana na mashauriano ambayo yanafanyika kati ya pande zote mbili za Muungano kwa maana ya kwamba kurahisisha utendaji kuhakikisha kwamba pande zote zinanufaika kwa maana ya kuwa na viwanda.

Sasa mazungumzo ambayo yanafanyika kwa pande zote mbili yanasimamiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa kupitia ile Kamati ambayo imeundwa kutoka pande zote mbili za Muungano na katika makubaliano yale ndiyo ikaonekana kwamba suala hili ambalo la kurahisisha utendaji wakati tunasubiri kuletwa Bungeni waendelee kutekeleza lakini kwa mashirikiano na upande huu wa pili wa Tanzania Bara.

Kwa hiyo, mimi sioni kwamba kuna Katiba imevunjwa hapo masuala haya ni ya utekelezaji, ni masuala ya kiuchumi, masuala ya manufaa wakati tunasubiri Bunge lipitishe hatuoni kama kuna mgogoro wowote ambao umetokea na hata kwenye kero za Muungano ukiangalia kwenye *list* pale hutaona kwamba suala la usajili wa viwanda ni suala ambalo ni la kwanza ambalo linaletwa kubwa ndiyo maana suala hili linafanyika. Lakini kama nilivyosema mwanzoni ni kwamba Serikali imejipanga kuleta Muswada hapa ili kuhakikisha kwamba Sheria hiyo inabadilishwa jinsi ambavyo mambo yake yanafanyika kiuhalisia. *(Makofi)*

Na. 44

**Mashamba ya Mkonge Yaliyotelekezwa – Korogwe**

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI** aliuliza:-

Yapo mashamba ya Mkonge yasiyoendelezwa katika Kata za Mnyuzi, Kwagunda, Mkalamo, Kerenge, Magoma, Mashewa na Makuyuni wakati wananchi wa maeneo hayo hawana mashamba kwa ajili ya kilimo.

Je, Serikali inatoa kauli gani ya kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanatolewa kwa wananchi yatumike kwa kilimo badala ya kuyaacha bure kama ilivyo sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika , mashamba ya Mkonge yaliyo katika Kata, Kwagunda, Mkalamo, Kerenge, Magoma na Mashewa bado yanamilikiwa na Bodi ya Mkonge Tanzania. Aidha Bodi ya Mkonge

nayo ina makubaliano ya kuendeleza mashamba hayo na Kampuni ya *Katani Ltd.* Hata hivyo, kwa muda mrefu sasa mashamba hayo hayajaendelezwa kwa kukosa mtaji.

Mheshimiwa Naibu Spika , ili kuendeleza mashamba hayo, Bodi ya Mkonge imechukua hatua zifuatazo:-

1. Kupima mashamba yote ili kutoa Hati Miliki kwa *Katani Ltd.* na Hati ndogo *(Sub-Title*) kwa wakulima wadogo ili wazitumie Hati hizo kupata mikopo.

2. Kuandaa utaratibu wa kuwapatia Hati za Utambulisho wakulima wadogo ambazo zitatambulika na kutumika kisheria wakati wanasubiri upimaji ukamilike.

Aidha, *Katani Ltd.* tayari wamepata mkopo kutoka *NSSF* ambao watautumia kukopesha wakulima wadogo kwa kutoa huduma ya kulima, kupanda na kutunza mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linalotakiwa ni kuhakikisha kwamba wakulima wanaelewa vizuri masharti ya kilimo cha mkataba watakaoingia na *Katani Ltd.* Hii ni kwa sababu mara nyingi baadhi ya watoa huduma za kilimo wasio waaminifu wanatumia mwanya wa uelewa mdogo wa wakulima kuwanyima haki zao hasa kwa kufanya makato makubwa na kuwapa bei ndogo. Namshauri Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kushirikiana na Wizara yangu kuhakikisha kwamba maslahi ya wakulima katika kilimo cha mkataba cha mkonge yanalindwa. Jambo hili ni muhimu hivi sasa ambapo bei ya tani ya Singa ya mkonge imepanda na imefikia zaidi ya Dola za Kimarekani 1,600. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI**: Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa tarehe 13 Septemba, 2010 saa nane mchana siku ya siku ya Jumatatu kwenye Jimbo langu Mheshimiwa Rais alikuja akahutubia mkutano wa hadhara na akatamka waziwazi kwamba mashamba yote yasiyoendelezwa yatagawiwa kwa wananchi wa kawaida. Je, Serikali itaanza kuyagawa lini mashamba hayo?

Kwa kuwa katika jibu lake la msingi amezungumza kwamba hawa mabwana wameshapatiwa mkopo na mashirika wanahela. Kuna wafanyakazi wengi wa Mkonge katika Tanzania hii hawajalipwa marupurupu yao mpaka leo hii. Sasa kwa kuwa wamepewa hela kwanini wasianze kuwalipa wafanyakazi ambao wamewatumikisha kwa muda mrefu bila mafao yao? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakubaliana naye kwamba mashamba haya kwa muda mrefu yamekuwa hayaendelezwi na kama nilivyoeleza sababu kubwa ni ukosefu wa mtaji. Lakini kwa Mheshimiwa Rais kama alivyosema mwenyewe aliahidi kwamba wakulima watapewa fursa ya kuyatumia mashamba hayo. Pamoja na kwamba tunafanya utaratibu mashamba haya yapimwe tunatafuta fedha kutoka kwenye Wizara yangu kutoka shilingi milioni 230 ndizo zinatakiwa na mamlaka za kuendeleza Bonde la kuendeleza Mto Rufiji Rubada ndiyo watakaopima mashamba hayo ili yaweze kugawiwa kwa lengo la kupata Hati Miliki. Lakini wakati utaratibu huo unafanyika nadhani ni jambo la busara kabisa kwamba kuliko mashamba yaendelee kuwa mapori basi tutatumia utaratibu ili mashamba hayo yaendelee kulimwa hata kwa kuazimwa kuliko kuyaacha yaendelee kuwa mapori kwa sababu haileti busara yoyote.

Lakini la pili, hili suala la kulipa ninayo taarifa kweli kwamba *Katani Ltd.* wamekopa kutoka *NSSF* na nilikuwa sijui lakini nimeyaona haya mambo katika magazeti. Ninachopata taarifa sasa ni kwamba *NSSF* wao waliwekeza kiasi cha bilioni 8.33 kupitia *Katani Ltd.,* Kwa utaratibu wao wa kuwekeza katika mashamba. Lakini ninachotaka kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge ni kwamba kilimo cha mkataba siku zote kina matatizo na mara nyingi hawa watu wa katikati wanapenda kumwonea mkulima. Tutakachokifanya Wizara yangu itaunda kikosi kazi itakayoshirikisha Wizara yangu, *CHC* kwa upande mwingine kwa sababu *PSRC* sasa hawapo pamoja na wadau wengine ili tuangalie ule mkataba waliokuwa wameingia ikoje, maana mara nyingine kwenye mikataba hii kuna vipengele ambavyo ni vya usuluhishi. Sasa inawezekana walitumia ujanja kwa kuwa wakulima hawavijui wakatumia nafasi kama hiyo. Sasa tunataka tutumie ujanja kwa kuwa wakulima hawavijui wakatumia nafasi kama hiyo. Sasa tunataka tutumie kile kilimo cha mkataba tuangalie haki ya wakulima ni ipi. Nataka nimwahidi kwamba tutaunda *task force* hii tufuatilie halafu tuwabane hawa tuweze kuwalipa wakulima.

**MHE. YUSUPH A. NASRI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa kuwa kero na adha ya mashamba ya mkonge Korogwe vijijini yanaendena sambamba na kero hiyohiyo kwa mashamba ya mkonge yaliyoko Korogwe Mjini. Labda tumwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, *Katani Ltd.* walikopa *NSSF* kwa kutumia hati za mashamba gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninayotaarifa kwamba *Katani Ltd.* walikopa kwa mgongo wa Bodi ya Mkonge. Kwa sababu walitumia hati milki ya Bodi ya Mkonge. Nilipofuatilia taratibu hizi nimeambiwa kwamba kuna makubaliano ambayo tayari waliingia kati ya *Katani Ltd.* na Bodi ya Mkonge ambayo ndani ya makubaliano hayo yanawaruhusu *Katani Ltd.* kutumia hati ile kuweza kukopa. Ndiyo maana nikasema naomba tuondoe *benefit of doubt* hapa. Sisi tutaweka *task force* iweze kuchunguza mambo yote haya pamoja na uhalali wa *Katani Ltd* kutumia Hati Milki ya Bodi ya Mkonge kupata mkopo kwa ajili ya kuendeleza mashamba hayo.

**MHE. RITA L. MLAKI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Japo sitoki Mkoa wa Tanga lakini nimefanya kazi Mkoa wa Tanga kuhusiana na mashamba haya kwa muda mrefu nikiwa Serikalini. Kwa kuwa tumeona tatizo la mkonge katika nchi yetu na tumeona mashamba mengi makubwa katika Mkoa wa Tanga ni ya mkonge na mkonge umeshindwa kushindana na mifuko ya *jute* inayotoka Bangladesh. Je, Serikali haioni umefika wakati mwafaka wa kusaidia kupata mwekezaji ambaye yupo tayari *Delmonte* kuchukua yale mashamba kwa *sub-lease* ili kuweza kujenga kiwanda cha matunda na hapo hapo wale wakulima wa Mkoa wa Tanga ambao unastawi matunda sana waweze kupata kazi na pia kupata mtaji?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rita Mlaki anataka mashamba yale ya mkonge yabadilishwe matumizi kusudi waweze kutumia kulima mazao mengine. Sasa kama nilivyosema mashamba yote ambayo hayajaendelezwa kweli ni kinyume cha taratibu za ubinafsishaji. Kinachatakiwa ni kuangalia yale mashamba ambayo hayajaendelezwa taratibu zitumike kulingana na masharti tuliowekeana. Lakini pamoja na hayo nataka pia niseme kwamba si kweli sasa kwamba mkonge unakwenda chini. Hali ya sasa hivi mkonge unakwenda juu na kama nilivyosema kwenye soko la dunia bei imefika dola 16,000 kwa tani. Kwa hiyo, ni zao ambalo tunataka msukomo zaidi. Huko nyuma liliharibiwa kutokana na singa bandia lakini sasa hivi naona mkonge unakwenda vizuri. Nadhani ni vizuri tuangalie namna ya kuliboresha zao hili la mkonge. *(Makofi)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika Jimbo la Same ya Mashariki Kata ya Ndungu kuna shamba kubwa sana la mkonge ambalo nalo limetelekezwa. Lakini shamba lile sasa limekuwa ni tatizo kwa sababu linaathiri mradi wa umwagiliaji wa Kata ya Ndugu. Je, Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye alifanya kazi pale anaweza akaja akaangalia ni kiasi gani lile shamba sasa linaathiri ule mradi kwa sababu limetelekezwa halilimwi mkonge, yanafanywa mambo ambayo si ya kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, eneo nalifahamu vizuri. Nitakuja tuangalie namna ya kuboresha.

**MHE. HALIMA J. MDEE**: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Taarifa ya ufuatiliaji mashamba yaliyotolewa na *CHC* Januari, 2012 inayonyesha kwamba mashamba 14 yenye ukubwa wa hekta 50,000 wawekezaji waliokabidhiwa katika Mikoa ya Morogoro na Tanga hayafanyi kazi kabisa. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na Mheshimiwa Mdee kwamba yapo mashamba mengi, tena nadhani twende *case by case*. Tuyatizame *in totality* nadhani yapo mashamba nadhani 32. Kati ya hayo kama sita ni kaputi kabisa mengine yanasuasua. Lakini kama nilivyosema nadhani iko haja ya sisi kuunda *task force* kuyafanyia tathmini mashamba yote haya ili hatimaye tuweze kumshauri Mheshimiwa Rais ambaye ndiye ana dhamana na matumizi ya ardhi. Kwa sasa mimi nafikiri tukubaliane tufanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Na. 45

**Kuimarisha Zao la Kahawa**

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA** aliuliza:-

Serikali kupitia Sera yake ya Kilimo Kwanza ina nia ya kuimarisha Zao la Kahawa na kwa sababu bei ya kahawa imepanda kwenye Soko la Dunia:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje Wakulima wa Vunjo kutumia fursa hiyo kuongeza uzalishaji wa kahawa?

(b) Inavyoonekana bei ya kahawa itaendelea kuwa juu kwa miaka 20 ijayo. Je, mkulima wa kahawa atakuwa anapata bei gani kwa kilo moja ya kahawa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa kahawa uliongezeka kutoka tani 40,000 mwaka 2009/2010 hadi tani 60,575 mwaka 2010/2011. Katika mwaka 2011/2012, uzalishaji wa kahawa unatarajiwa kupungua kutoka tani 60,575 hadi tani 45,000. Upungufu huo unatokana na tabia ya Zao la Kahawa kupungua uzalishaji katika msimu unaofuatia msimu wa uzalishaji ulioongezeka. Hii ni tabia ya kawaida ya zao hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwasaidia Wakulima wa Vunjo na wengine wote nchini, Serikali inaendelea kutekeleza mkakati wa kuendeleza tasnia ya kahawa kwa kusimamia mambo muhimu yafuatayo:-

(i) Kupitia Kituo cha Utafiti wa Kahawa *TaCRI* na maafisa ugani, kuhamasisha upandaji wa miche bora ya kahawa na yenye ukinzani na magonjwa ya chulebuni na kutu ya majani.

(ii) Kuwaandalia wakulima mazingira ya soko la pamoja ili wanufaike na bei za mnadani.

(iii) Kufufua kilimo cha kahawa katika Mikoa iliyokuwa ikilima kahawa kwa wingi zamani na kuhamasisha kilimo hicho katika Mikoa mingine ya Mara, Mwanza, Kigoma, Tanga, Morogoro, Iringa na Rukwa. Hivyo, Serikali itawasaidia Wakulima wa Vunjo kupanda miche bora ya kahawa yenye ruzuku ya Serikali.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2010/2011 bei ya kahawa ilipanda kufikia shilingi 7,000 kwa kilo ya kahawa safi ya Arabica ya *Grade A* kutoka wastani wa shilingi 5,000 kwa kilo katika mwaka 2009/2010. Aidha, bei ya mnada wa Moshi ilipanda na kufikia shilingi 10,000 katikati ya mwezi Januari 2012. Bei ya kahawa ya Arabica kwa kawaida huratibiwa na Soko la New York "C" na kahawa ya Robusta inaratibiwa na Soko la *London Internationa Future Exchange*. Mkakati wa Serikali sasa ni kuhakikisha kwamba mkulima anapata angalau asilimia 80 ya bei katika soko la Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kwamba, baada ya kushauriwa tayari Mheshimiwa Mrema amewasiliana na Wizara yangu na Viongozi wa Taasisi ya *TaCRI* ili kuona namna ya kuboresha kilimo cha kahawa katika Jimbo la Vunjo. Nampongeza sana Mheshimiwa Mrema kwa juhudi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nimefurahi na Wananchi wa Vunjo wamefurahi kusikia kwamba bei ya kahawa kwenye Soko la Dunia mwezi Januari ni shilingi 10,000 kwa kilo. Ili mkulima aweze kunufaika na bei hiyo, najua kuna mchwa wengi kwenye Vyama vya Msingi, kwenye Chama Kikuu cha KCU na kwenye Bodi ya Kahawa, wanaotafuna hela za wakulima. Sasa, ili huyu mkulima aweze kunufaika na hii bei ya shilingi 10,000, Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba mkulima anapata angalau asilimia 80 ya bei ya Soko la Dunia ili kumpa moyo kwa sababu sisi ni wakulima wazuri sana wa kahawa lakini tulipokosa bei nzuri basi watu wakaamua kukata kahawa wakalima nyanya na mboga?

Ninaomba hilo ili lisirudiwe, Serikali ita-*guarantee* vipi kwamba bei hii kwa miaka 20 ijayo inapatikana ili kumpa moyo mkulima wa kahawa wa Jimbo la Vunjo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Vunjo yenyewe na Mkoa wa Kilimanjaro, *traditionally* ni wakulima wa kahawa, siyo watu wa kufundishwa kahawa. Mmemsikia Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko muda mfupi uliopita akisema kwamba, ubora wa bidhaa ndiyo unaoweka bei nzuri sokoni. Sasa, kwa bei za mazao, kweli kabisa Soko la Dunia ndilo linalotutikisa tikisa. Sisi pia tunalo jukumu sasa kwa upande wetu, ndiyo hapo ninasema kwamba, tuongeze ubora wa mazao haya kuanzia shambani, kwenye huduma za ugani, kutengeneza mazao yenyewe, kukoboa kwa kutumia *central pulperies,* tuache kukoboa kwa kutumia vile vimashine vya kizamani ili zao lile liwe na thamani ambayo ni nzuri, liuzike katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina mfano mzuri pale kwangu wameanza miaka kama miwili iliyopita tu; wamepandisha bei ya kahawa pale Mhangi kutoka shilingi 1,800 kwa kilo sasa wanauza kwa shilingi 5,800 na wanaendelea kuongeza. Bei hii imeongezeka kutokana na kuweka *central pulperies.*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu mchwa ambao amesema Mheshimiwa Mrema, mimi naomba tuseme tu kwamba, udhibiti pale katika ngazi ya vyombo vya wakulima hasa Vyama vya Ushirika, huko ndiko tunatakiwa kudhibiti kwa sababu huyo mchwa yuko kwenye Vyama vya Ushirika na hilo siyo jambo la Soko la Dunia ni jambo letu wenyewe.

Na. 46

**Vigezo Vinavyotumika Kutoa Mkopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu**

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI** aliuliza:-

Ipo Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu nchini:-

Je, ni vigezo gani vinavyotumika na Bodi hiyo ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwapatia mikopo wanafunzi wa Vyuo Vikuu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Haji Ali, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vya utoaji mikopo kwa mwaka wa masomo wa 2011/2012 vilivyotumika na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kuwapatia mikopo wanafunzi ni kama ifuatavyo:-

(i) Mikopo inatolewa tu kwa waombaji waliodahiliwa na Vyuo vya Elimu ya Juu na ambao wanatoka shuleni moja kwa moja (*Direct Entrants)* na wale wenye sifa kupitia mfumo wa mafunzo ya Elimu ya Ufundi *(TVET)*.

(ii) Utaratibu wa kubaini wahitaji wa mkopo unazingatia vigezo vinavyopimika kwa urahisi kama vile shule aliyosoma, uyatima, ulemavu na uwezo wa kiuchumi wa mzazi.

(iii) Kiwango cha mkopo kwa wale wanaostahili kukopeshwa kinategemea matokeo ya tathmini ya uwezo wa kiuchumi wa mwombaji na mzazi/mlezi kwenye vipengele vya ada ya mafunzo na mahitaji maalumu ya vitivo.

(iv) Kwa kuzingatia kuwa wahitaji ni wengi, umuhimu utapewa kwa wahitaji wanaochukua fani za kipaumbele za kitaifa ambazo kwa sasa ni Ualimu, Sayansi za Tiba, Uhandisi, Sayansi za Kilimo na Sayansi za Mifugo.

(v) Waombaji katika fani zifuatazo watapatiwa mikopo kwa asilimia mia moja: Ualimu wa Sayansi na Hisabati na Sayansi na Tiba.

(vi) Waombaji wa ualimu ambao si wa fani ya sayansi na hisabati wanapewa mkopo kwa asilimia isiyopungua hamsini.

(vii) Waombaji wenye sifa linganishi *(equivalent qualifications and mature entry)* katika fani za ualimu wa sayansi na hisabati na sayansi za tiba watapata mkopo kwa asilimia mia moja.

(viii) Mikopo inatolewa kwa wanafunzi waliodahiliwa katika Vyuo vya Elimu ya Juu vyenye usajili kamili *(Full Registration)* tu. Hata hivyo, kwa vile kwa mwaka wa masomo wa 2011/2012 wanafunzi walishaomba udahili, mikopo imetolewa pia kwa vyuo vyenye usajili wa muda *(Certificate of Provisional Registration)*.

(ix) Kwa waombaji kwenye vyuo binafsi, mikopo inatolewa kulingana na ada zinazotozwa na Vyuo vya Umma kwa fani husika. Aidha, katika fani ya tiba ukomo wa mikopo unaendelea kupangwa na Bodi ya Mikopo.

(x) Kigezo cha ruzuku kwa wanafunzi wa sayansi za tiba viko viwili; ruzuku zinatolewa kwa wanafunzi wa sayansi za tiba waliopata udahili kwa ufaulu wa daraja la kwanza na la pili kulingana na ukomo wa bajeti; na ruzuku pia itatolewa kwa wanafunzi wa sayansi za tiba wenye ufaulu wa daraja la tatu unaotokana na kushindwa somo la *General Studies* katika mitihani yao ya Kidato cha Sita.

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu fasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Je, ni njia zipi zinazotumika kuvitambua vigezo hivyo?

(ii) Kwa kuwa wanafunzi wote wa Vyuo Vikuu wasiopata mkopo wa asilimia 100 hulazimika kumega fedha zao za kujikimu kulipia masomo jambo ambalo huwasababishia maisha magumu vyuoni kiasi kwamba hufikia hatua ya kuombaomba na wasipofanya hivyo huzuiliwa matokeo yao; na kwa kuwa fedha inayotolewa siyo sadaka, siyo ruzuku, wala siyo msaada ni mkopo kwamba hatimaye wanafunzi wote…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, swali lako ni la moja kwa moja au?

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** Ni la moja kwa moja!

**NAIBU SPIKA:** Unapitia kwenye karatasi au?

**MHE. ABDALLAH HAJI ALI:** *No, no!*

**NAIBU SPIKA:** Basi uliza kwa kifupi.

**MHE ABDALLAH HAJI ALI:** Haya. Hatimaye wanafunzi hutakiwa kulipa kwa utaratibu uliowekwa. Ili kuondoa migogoro ya kila siku isiyokuwa ya lazima; je, Serikali haioni ni busara kutoa viwango sawa vya asilimia mia moja kwa wanafunzi wote? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anasema ule utofauti wa ada zinazotumika kwa vyuo mpaka inasababisha wanafunzi wengine wanachukua fedha ya kujikimu kulipia ada ni kweli kabisa suala hili linatokana na ukomo wa bajeti. Baadhi ya vyuo hasa vya binafsi vinatoza ada tofauti na ile ada ya vyuo vya umma. Hata hapa juzi juzi tumetambua wote kwamba, Chuo cha IMTU kinatoza ada kwa Dola na kinatoza ada mpaka shilingi milioni saba, jambo ambalo tayari Serikali imeingilia kati na tunaendelea kulifanyia kazi na hii ndiyo imesababisha utofauti mpaka wanafunzi wanaanza hata kuchukua fedha za chakula kwa ajili ya kulipia ada.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kuhusu vigezo vya mikopo; utakumbuka jana ililetwa *miscellaneous amendment* hapa kwa ajili ya mabadiliko ya mambo kama haya. Ninaomba tu Waheshimiwa Wabunge mtuvumilie, mtupe muda kama mlivyopendekeza jana kwamba, Bunge lijalo la mwezi Aprili tuje hapa na vigezo kamili muweze kuchangia ili kwa pamoja sote tuendane na vigezo ambavyo Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla watalielewa suala hili vizuri sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyoamua jana, moja kati ya mambo ambayo tuliyaamua ni kwamba, jambo hili litazamwe vizuri. Mimi ningeliomba tuwe na subira.

Na. 47

**Kusuasua kwa Ujenzi wa Barabara – Tabora**

**MHE. ISMAIL A. RAGE** aliuliza:-

(a) Je, kwa nini ujenzi wa Barabara za Tabora za Nzega – Tabora, Tabora –Manyoni na Tabora – Urambo unasuasua?

(b) Je, Serikali inaweza kuwahakikishia Wananchi wa Mkoa wa Tabora kwamba na wao watapata barabara za lami?

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba radhi sana, sauti yangu ina matatizo kidogo, nafikiri imeingiliwa na watani zangu Wagogo wakiongozwa na wewe, lakini nitajitahidi nijibu vizuri. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mbunge wa Tabora Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kusuasua kwa ujenzi wa Barabara ya Nzega – Tabora, Tabora – Manyoni na Tabora – Urambo, zinazojengwa kwa jumla ya shilingi bilioni 453, kumechangiwa na mambo mengi yakiwemo kuchelewa kwa Mkandarasi kufanya *mobilization* na kuchelewa kupatikana mapema fedha za *advance payments* zilizotakiwa kulipwa na Serikali. Hata hivyo, hivi karibuni Serikali imefanikiwa kupata fedha na kuwalipa wakandarasi malipo ya awali *(advance payments),* kulingana na mikataba iliyopo. Hivyo, makandarasi kwa sasa wasitafute kisingizio chochote. Aidha, Serikali inaendelea na juhudi ya kutafuta fedha za kutosha ili kuendelea kuwalipa makandarasi wanaojenga barabara hizi na nyingine nchini. Serikali inapenda kuwahakikishia Wananchi wa Mkoa wa Tabora kuwa, ujenzi wa Barabara ya Nzega – Tabora yenye urefu wa kilomita 115 na Tabora – Manyoni yenye urefu wa kilomita 250 na Tabora – Urambo yenye urefu wa kilomita 94 kwa kiwango cha lami utaendelea kutekelezwa na kukamilika kama ilivyopangwa. Aidha, nampongeza sana Mheshimiwa Rage kwa kufuatilia masuala yanayohusu Barabara za Mkoa wa Tabora.

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa. Wananchi wa Mkoa wa Tabora wamekuwa wavumilivu kwa muda mrefu sana na wamekuwa na imani kubwa sana kwa Serikali yao ya CCM:-

(i) Je, Waziri anaweza akatoa tamko rasmi hapa Bungeni barabara hizo zitakwisha kwa wakati kwa mujibu wa mkataba ulivyotakiwa? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa makandarasi wako watano; je, mpaka sasa ni kiasi gani cha pesa kimeshatolewa na bado kiasi gani? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Ismail Aden Rage kwamba, Wananchi wa Tabora, waendelee kuwa na imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa sababu ndiyo iliyopanga mkakati wa kuamua kujenga hizi barabara zenye jumla ya kilomita 459 na mikataba ikasainiwa na makandarasi wote wako kwenye *site*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika kufafanua kwa ufupi sana, Barabara ya Nzega – Puge yenye jumla ya kilomita 65, *cost* ya *contract* yake ni shilingi bilioni 66 na hadi sasa mkandarasi ameshalipwa *advance payment* ya shilingi bilioni nene. Barabara ya Puge – Tabora yenye jumla ya kilomita 56.1 *contract* yake ni ya shilingi bilioni 52.7 na hadi sasa mkandarasi pamoja na *consultant* wameshalipwa *advance payment* ya shilingi bilioni tisa. Katika Barabara ya Tabora – Nyahua yenye jumla ya kilomita 85, *contract value* yake ni shilingi bilioni 93.4 na *consultant* ni shilingi bilioni tatu na hadi sasa *contactor* pamoja na *consultant* wameshalipwa *advance payment* ya shilingi bilioni 13.5. Barabara ya Tabora – Ndono yenye jumla ya kilomita 42, *contract sum* yake ni shilingi bilioni 51.3 na hadi sasa wameshalipwa shilingi biloni saba. Barabara ya Ndono – Urambo yenye jumla ya kilomita 52, *contract sum* yake ni shilingi bilioni 59.1 na hadi sasa *contactor* ameshalipwa shilingi bilioni 7.1. Kwa hiyo, jumla ya *advance payment* ambazo zimeshalipwa hadi sasa ni shilingi bilioni 45 katika Mradi mzima. Siyo huo tu hata ule Mradi wa kutoka Manyoni – Itigi – Chunya wenye jumla ya kilomita 89, *contract sum* yake ni shilingi bilioni 109 na *contractor* hadi sasa hivi ameshalipwa shilingi bilioni 15. Kwa hiyo, nataka kumthibitishia makandarasi sasa hawana kisingizio na sisi tutaendelea kuchukua hatua za kuwasimamia kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa taarifa yako hadi hivi sasa tumeshafukuza makandarasi 2,900 katika nchi hii. Kwa hiyo, tutaendelea kuwafukuza makandarasi ambao hawa-*perform* kazi zao na makandarasi wa Tabora wajiandae, wahakikishe barabara hizi wanazikabidhi katika mwaka 2013/2014 kulingana na mkataba ulivyopangwa. *(Makofi)*

*(Hapa Wabunge kadhaa walisimama kutaka kuuliza maswali)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawaona lakini mnajua sauti ya Mheshimiwa Waziri imeishia kwenye barabara za vumbi huko. Tunaendelea na Wizara ya Nishati na Madini.

Na. 48

**Wananchi Kuhamishwa na Kulipwa Fidia Kupisha Uchimbaji Madini**

**MHE. ESTHER N. MATIKO** aliuliza:-

Serikali ina mamlaka ya kutwaa na kubadilisha matumizi ya ardhi na hivyo kuwajibika kulipa fidia kwa Wananchi wanapopisha matumizi mapya ya ardhi na kuwapa maeneo mbadala:-

(a) Je, kwa nini uchimbaji wa madini katika eneo la Nyabigena unaofanywa na Kampuni ya Barrick umeruhusiwa bila kwanza kuwahamisha wakazi wa maeneo hayo ambao wanapata madhara makubwa?

(b) Je, Serikali imeshindwa kusimamia zoezi la ulipaji fidia wenye tija stahiki kwa wakazi wa vijiji vinavyozunguka Mgodi wa North Mara maana wamekuwa wakipewa fidia ndogo kuliko uhalisia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Esther Nicolaus Matiko, Mbunge wa Viti Maalum, lenye semeu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji wa madini ya dhahabu katika eneo la Nyabigena unaofanywa na Kampuni ya *African Barrick Gold* ulianza baada ya kukamilika na kupitishwa kwa tathmini

ya athari ya mazingira na jamii *(environmental and social impact assessment)* iliyoshirikisha wadau wote wa Mgodi wa dhahabu wa North Mara. Wale walioonekana kutakiwa kupewa fidia ili kupisha shughuli za uchimbaji madini, walilipwa fidia baada ya uthamini wa mali zao kufanyika kwa mujibu wa sheria ya ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na tathmini ya Serikali, Kampuni ya *African Barrick Gold (ABG)* imekuwa ikitoa fidia kulingana na mali zilizopo kwenye eneo husika. Kwa mfano; hekta moja ambayo ni ardhi tu fidia yake ni Dola za Marekani 23,000, hekta moja yenye kuendelezwa kwa maana ya kuwa na mazao ni Dola za Marekani 35,000 na ambapo kuna nyumba, fidia yake ni kwa mujibu wa tathmini ya Serikali ambapo itahusisha uhamisho na makazi mapya kwa maana ya kujengewa nyumba ambayo ni bora kuliko ya awali. Pamoja na kufanyika tathmini kwa kaya zinazozunguka mgodi, kumejitokeza matatizo mbalimbali; mfano, kaya tano hazijaridhia kufanyika kwa tathmini hiyo ya fidia. Majadiliano yanaendelea kwa kushirikisha Kijiji cha Nyangoto. Familia 40 ziliamua kurudi katika maeneo waliyokwishalipwa na kwa sasa wanadai fidia upya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kulipa fidia kwa Wananchi wanaotakiwa kupisha shughuli za Mgodi wa North Mara linasimamiwa na Serikali katika ngazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Tarime. Utaratibu unaotumika ni kuthaminishwa kwa mali na ardhi ya Wananchi wanaotakiwa kuhamishwa kwa viwango vilivyowekwa na Serikali kupitia Sheria ya Ardhi. Kimsingi, Mgodi wa Dhahabu wa North Mara umekuwa ukitoa malipo ya fidia kwa viwango vikubwa kuliko viwango vinavyotolewa na Serikali.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nasikitishwa na majibu ya Naibu Waziri kwa kusema kwamba kulifanyika tathmini ya athari ya mazingira na kijamii. Nimekuwa nikizungumzia Shule ya Nyambigina kwamba inaathirika na mazingira kwa maana ya vumbi na kelele *(industry pollution and noise pollution),* ambayo inapelekea kutokuwa na usikivu kati ya wanafunzi na walimu; lakini pia ni mwaka jana mwezi wa kumi na moja kulitokea mvutano kati ya Polisi na ma-*intruder* na wakapelekea kupiga mabomu wanafunzi wa *nursery* ambao walitolewa meno na macho. Ninasikitika kwamba kulifanyika athari ya mazingira na kijamii na ikaridhia machimbo katika Kijiji cha Nyambigina yaendelee:-

Nataka kujua; Naibu Waziri ameeleza kwamba waligoma kuhama na Serikali iligoma kuihamisha Shule ya Msingi ya Nyambigina kutoka katika sehemu ile na kuipeleka sehemu mbadala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, kabla sijaruhusu swali hilo kujibiwa, una hakika na hili kwamba watoto wa shule za msingi waling'olewa meno na macho?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika ndiyo, ushahidi upo na hilo swali nilimwuuliza pia Waziri Mkuu kipindi kilichopita.

**NAIBU SPIKA:** Majibu Naibu Waziri wa Nishati na Madini.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mhehsimiwa Naibu Spika, bado swali la pili la nyongeza!

Naibu Waziri ameeleza kwamba kumekuwa kukitolewa fidia nzuri na kujengewa nyumba bora. Kwa jinsi jamii ya Wakurya ilivyo ...

**NAIBU SPIKA:** Hebu nikuombe uyaorodheshe vizuri maswali yako, nakupa muda tena maana naona kama yanazidi; anza tena.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeuliza kama ifuatavyo:-

(i) Nilitaka kujua kwamba tathmini iliyofanyika ya athari ya mazingira na ya kijamii na ikapelekea kuruhusu Mgodi wa *North* Mara kuendelea na uchimbaji ambapo kuna athari nimezitaja kama athari ya vumbi na kelele, ambayo inapelekea kutokusikilizana wanafunzi na walimu wanaofundishana pale.

Nikaainisha kwamba kupelekea kuwepo kwa shule ile kukawa na kupigana mabomu kati ya *police* na ma-*intruder* ambapo wanafunzi waliathirika. Nikauliza sasa Serikali imeainisha kwamba waligoma

kuhamishwa, Serikali nayo iligoma Shule ya Msingi ya Nyambigina kuhamishwa kutoka pale kwenda sehemu mbadala?

(ii) Ameainisha kwamba kuna ujenzi mzuri wa nyumba bora na kwa jinsi ilivyo jamii ya Wakurya familia moja ina zaidi ya wake wawili lakini ujenzi ni vyumba viwili, jiko na sebule. Je, Serikali haioni kwamba pamoja na fidia hizo ni wakati mbadala kuwafanya wanavijiji wale kuwa na hisa ili waweze kuwa na maisha bora? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Swali la kwanza mahali pake hasa ni Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, naomba nilisemee hili kidogo kwa sababu lina uzito kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunasema hivi; kabla wale mabwana hawajafanya *any mining activity* siyo *mining activity* tu hata *energy activity* ya aina yoyote ni lazima pawe na *environmental and social impact assessment*. Kabla sheria haijasema hivyo, mtu alikuwa anafanya kwa hiari lakini sasa hivi siyo suala la hiari. Kwa hiyo, kwenye *impact assessment* ile kuna mambo mengi; sasa ukiniambia kuna *noise and dust pollution* mimi ninasema kuna vigezo vya kitaalam ambavyo kama kuna *noise and dust pollution* iko pale, Wananchi wenye mazingira yale wanatakiwa wahamishwe kwa gharama za mgodi. *And that is not a favour,* hilo siyo suala la mgodi kufanya kama ni jambo la kuwazawadia wananchi, hapana. *If you want to mine,* wahamishe Wananchi wapeleke kwenye mazingira yenye ubora zaidi kuliko yale uliyoyakuta pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hili la shule kama pana *dust and noise pollution* ambayo imethibitika kwa Nyambigina wanatakiwa kuhamishwa, lakini hiyo inakwenda kwa vigezo vya kitaalam siyo kwa vigezo vyangu mimi na wewe Mheshimiwa Esther.

Kwa maana hiyo, mimi nasubiri kupata vigezo vya kitaalam na kusema kweli kama hawajahamishwa siyo jambo la hiari ni kwamba, *as long as environmental impact assessment* inasema wale wahame, wanatakiwa wahamishwe na gharama iende kwa mgodi; *otherwise,* hawatapewa ruhusa ya kuendelea kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimuahidi Mheshimiwa Esther kwamba, tutakwenda pale na tutalifanyia utaratibu wa ku-*verify* kwamba *impact assessment* inasema shule ihamishwe na kama haijahamishwa ninakuhakikishia kwamba, Serikali itatoa maagizo ya mara moja kwamba wajengewe shule mpya yenye mazingira bora kuliko hiyo shule waliyokuwa nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili tunasema hivi; kwenye suala la nyumba bora, siyo nyumba bora kwa sababu wewe ulikuwa una kibanda chako cha chumba kimoja sasa unataka wakujengee vyumba vinane hapana. Mheshimiwa amesema kwamba, mtu ana wake watatu, kwa hiyo, sasa kama alikuwa na mazingira ya wake watatu na kila mmoja ana nyumba yake, akihamishwa kila mmoja apewe nyumba yake tena nzuri zaidi kuliko ile iliyokuwepo; lakini kama wake watatu wote alikuwa amewaweka kwenye nyumba moja basi wata…

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, suala tunalolizungumzia hapa ni kwamba, wanapokuja pale kuna ile ya kwanza ambayo ni pesa zinazolipwa kwa eneo ambalo halina chochote.. *Grade* ya pili ni pesa ambazo zinalipwa kwa mazao, lakini pale pana nyumba, ile nyumba inafanyiwa tathmini na hiyo tathmini tunaifanya sisi watu wa Halmashauri, kwa maana ya mimi na wewe kwa sababu sisi ndiyo wenye Halmashauri, tukishajua kwamba hii nyumba thamani yake ni milioni kumi na tano au ishirini, wenye mgodi wakitaka kuhuhamisha wakujengee nyumba nzuri kuliko ile uliyokuwa nayo. Kama ulikuwa una nyumba ya kibanda kimoja unataka wakujengee vyumba sita, itakuwa kidogo haipo sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii, kuna fidia mpya inayokuja kulipwa kwenye hayo maeneo ya Nyangabi kwa hii *expansion* inayofanywa. Tuhakikishe kwamba, wanakwenda kwa utaratibu wa Sheria Mpya ya Ardhi na Sheria Mpya ya Madini inayotoa vigezo bora zaidi kuliko sheria zilizokuwepo zamani.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali bado ni mengi na muda karibu unakwisha; niseme kidogo tu kuhusu hili la Shule ya Nyambigina. Mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, katika Bunge la Tisa, tuliwahi kwenda pale na Waziri Ngeleja; ni kweli kabisa kwamba, shule hii ipo *next* kabisa na mgodi. Kwa hiyo, *pollution* iliyopo pale ni kubwa. Kwa hiyo, ni jambo ambalo Serikali ichukue hatua tu haina haja ya kuwa na ubishani huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, muda sina kabisa, naomba tuendelee na swali la arobaini na tisa la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa.

Na. 49

**Matumizi ya Madini ya *Uranium***

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA** aliuliza:-

Matokeo ya tafiti nyingi yameonesha kuwa kuna Madini ya *Uranium* nchini:-

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kutoa elimu kwa Wananchi kuhusu athari za kiafya zinazoambatana na uchimbaji na utumiaji wa madini hayo?(b) Je, kuna Mikataba ya Kimataifa inayoweka wazi vigezo vya nchi gani iruhusiwe na ipi ikatazwe kuendeleza nishati hiyo nchini mwao?

(c) Je, Serikali ina uhakika gani kuwa kama tukitumia nishati itokanayo na *uranium* nchi yetu haitawekewa vikwazo vya kiuchumi na Jumuiya ya Kimataifa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa David Homeli Mwakyusa, Mbunge wa Rungwe Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti za kijiolojia zilizofanywa miaka ya 1979 hadi 1982 zilionesha uwezekano wa kuwepo kwa mashapo yenye madini ya *uranium* katika baadhi ya maeneo hapa nchini. Maeneo hayo ni pamoja na Mkuju, Namtumbo Mkoani Ruvuma, baadhi ya maeneo yaliyo kwenye hifadhi ya Selous, Bahi Mkoani Dodoma, Kondoa, Itigi Wilaya ya Manyoni, Milima ya Uluguru katika Wilaya ya Morogoro na Gallapo katika Wilaya ya Babati.

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwemo Wananchi wanaoishi maeneo ambayo utafiti wa madini hayo unaendelea ili kuondoa hofu ya madhara ya madini hayo. Kwa mfano, Waziri wa Nishati na Madini akiongozana na Wataalam wa Madini na Wataalam wa Mazingira, walifanya ziara ya kutembelea eneo linalokusudiwa kuanzisha Mgodi huko Mkuju, Wilaya ya Namtumbo, tarehe 19 Juni 2009 na kuzungumza na Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa na Wananchi katika Wilaya hiyo na kuwaelimisha juu ya faida, madhara na namna Serikali inavyojiandaa kukabiliana na madhara ya uchimbaji, uchenjuaji, usafirishaji na biashara ya madini ya *uranium*. Pia mwezi Septemba 2009, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, akiongozana na Wataalam wa Madini, alitembelea Wilaya za Bahi na Manyoni kwa ajili ya kutoa elimu juu ya mpango wa Serikali katika utafutaji, uchimbaji na matumizi ya madini ya *uranium* nchini. Madini ya Uranium kama *ore* inavyopatikana ardhini, hayana madhara kwa binadamu kwa kuwa madini yameungana kikemikali na elementi ya *oxygen* kuwa *uranium oxides* kama vile *uranite* na *pitchblende*. Endapo *uranium oxide* itatenganishwa kupata metali ya *uranium* ndiyo yanaanza kuwa ya hatari kwa kutoa mionzi inayosababisha Ugonjwa wa Kansa kwa binadamu. Aidha, Serikali imetunga Sheria na Kanuni kwa ajili ya kusimamia shughuli za utafutaji, uchimbaji, utunzaji, usafishaji na biashara ya madini ya mionzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Mikakati ya Kimataifa inayoweka wazi vigezo vya nchi gani iruhusiwe kuongozwa na sheria na taratibu za nchi husika; ni lazima pia uzingatie taratibu zilizowekwa

na Taasisi ya Kimataifa ya Kusimamia Masuala ya Mionzi, yaani *International Atomic Energy Authority* (*IAEA*), ambapo Tanzania ni mwanachama.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeridhia Mikataba ya Kimataifa kuhusu utafutaji, uchimbaji, utunzaji, usafirishaji na biashara ya madini ya mionzi. Hivyo, endapo Serikali itaamua kutumia nishati itokanayo na *uranium,* nchi yetu haitawekewa vikwazo vya kiuchumi na jumuiya hizo iwapo itazingatia taratibu na sheria zilizoainishwa katika Mkataba wa Kimataifa.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo ya nyongeza na vilevile namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu kwamba, Waziri pamoja na Wataalam wake wanajua kwamba katika kushughulikia masuala ya *uranium* hasa uchenjuaji, mahitaji ya maji ni makubwa sana. Kwa mfano, utafiti uliofanyika kwenye Mgodi wa Namibia unaonesha kwamba mahitaji ni lita milioni moja kwa siku. Sasa, kwa uelewa wangu maeneo ambayo tunataka kuanzisha hii migodi kama Bahi, Manyoni na Namtumbo ni maeneo kame kabisa ambako hawana maji. Ina maana kwamba, wakianza kuchimba maji yatabubujika pale kwa wingi sana:-

(i) Nilitaka kujua kama Serikali ina miradi mingine ya kuweza kuwapelekea maji wanavijiji wa vijiji ambavyo vinazunguka au wao watabaki kuwa watazamaji wakiona maji yanabubujika katika mgodi?

(ii) Uzoefu wetu hapa nchini ni kwamba; ukizungumza habari za uwekezaji unaoanisha na migogoro kati ya wawekezaji pamoja na Wananchi wanaokaa kwenye vijiji vinavyozunguka huo uwekezaji; kwa mfano, tumeshuhudia katika migodi, ranchi na mashamba. Nilitaka kujua kama Serikali ina mikakati iliyoiweka au hatua ambazo zinaendelea za kuepusha hiyo migogoro pindi hiyo migodi itakapoanza kufanya kazi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI**: Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, kwenye masuala ya uchenjuaji wa *uranium* kuna mahitaji makubwa ya maji. Katika *Business Plan* ambayo *especially* hawa watu wa Mkujo, kwa sababu hawa wapo kwenye hatua ambayo ni ya mbele zaidi, kila aina ya uendelezaji wa Mradi ule wa Mkujo unaofanyika pale inabidi uzingatie pia na yale maeneo ya vijiji vya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyokubaliana, tulisema Waziri amekwenda na mimi mwenyewe nimekwenda pale, tumeongea na Wananchi tumekubaliana kwamba maendeleo yoyote pale siyo ya maji tu mpaka nishati za umeme, barabara na kadhalika, vitu vyote hivi vizingatie maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatokana na kuboreshwa kwa sheria mpya ambayo inatoa vitu hivi kwenye *cooperate social responsibility* na kuweka kama sehemu ya mkataba mahususi wa uendelezaji wa mgodi. Kwamba, kama ninyi kwenye mgodi mnajiwekea vitu vyote hivi na maji yote haya basi na Wananchi wa maeneo yote yale yanayozunguka yapate maji ya kutosha, maji safi na salama na kwa maana hiyo kwa nishati, kwa barabara na kwa mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili tunalifahamu na tumeliweka katika uendelezaji wa mgodi huo lipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la migogoro *especially* ya Namtumbo, kwa sababu huku Manyoni bado Uranex bado hawajafikia sehemu ya kukubaliana kuhusu *commercial viability* ya Mradi ya Manyoni, lakini kule Mkujo niseme tu kwamba, katika hatua zote za mara kwa mara tunazokwenda, Wananchi wanashirikishwa sana ili kuhakikisha kwamba, tunaepukana na migogoro hiyo isiyokuwa na sababu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa ridhaa yako niseme tu katika lile swali la Mheshimiwa Esther Matiko, nimekubaliana na Waziri sasa hivi kwamba, tukimaliza hapa tukitoka Bungeni tutakwenda kulifanyia tathmini pamoja na Wataalam wa *Barrick* pamoja na wewe mwenyewe na Mbunge wa maeneo yale na wenzako ili kama *NEMC* wakituthibitishia kwamba eneo la Shule ya Nyambigini lipo kwenye *a dust polluted area,* tuwahamishe wale watoto mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie kwamba, hili tunakwenda kulifanyia kazi mara moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tuhamie Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed.

Na. 50

**Chanzo cha Maradhi ya Kisukari, Presha, Kansa na Moyo**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Maradhi ya Kisukari, Shinikizo la damu, Kansa na Moyo yanazidi kujitokeza kwa wingi katika nchi yetu:-

(a) Je, Serikali haioni kwamba huenda kuna kitu kinachosababisha maradhi hayo?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuchunguza chanzo cha maradhi hayo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zinazosababisha maradhi ya kisukari, presha, kansa na moyo, zinajulikana Duniani kote kwamba zinahusiana na mabadiliko ya mtindo wa maisha *(Life Style)*. Baadhi ya sababu hizo ni kama zifuatazo: Lishe isiyozingatia misingi ya afya kama kutumia sukari, mafuta na chumvi kwa wingi na kutokula matunda na mbogamboga; matumizi ya tumbaku; uzito kupita kiasi na kiribatumbo; kutokufanya mazoezi; matumizi ya vilevi kupita kiasi; kutokuwa na utamaduni wa kupima afya zetu na kupata ushauri wa kitaalam ili kujikinga na maradhi haya; na ukosefu wa elimu sahihi kuhusu maradhi haya.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari na inaendelea kutoa huduma za uchunguzi wa maradhi kwa nia ya kugundua mapema na kuzuia athari kwa kutoa ushauri na tiba stahiki mapema. Pia Serikali imeendelea kuwezesha watafiti wa maradhi ya binadamu kupitia taasisi za utafiti ili kufahamu visababisho vya maradhi pamoja na namna bora ya kuzuia na kutibu. Mfano, Taasisi ya Utafiti wa Maradhi ya Binadamu (*NIMR*). Aidha, nawapongeza wadau wote wanaoshughulika na uchunguzi wa maradhi ya binadamu kama vile Taasisi za *NIMR* na *Ifakara Health Institute* na wadau wengine kama *MEWATA* na *AMREF,* kwa mchango wao mkubwa wanaoutoa katika kutafuta mbinu madhubuti za kuzuia na kutibu maradhi sugu.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Naomba kuuliza maswali yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa wagonjwa wengi wanaougua maradhi haya ni maskini sana na wapo vijiji na taasisi zinazofanya uchunguzi wa maradhi haya zinafanya kazi zaidi mijini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba Wananchi wake wanapata huduma hii ya uchunguzi mapema kabla maradhi haya hayajaathiri zaidi?

(ii) Kwa kuwa sababu mojawapo inayosababisha maradhi haya ni uvutaji wa tumbaku na Serikali huku ikijua kuwa tumbaku ina madhara kwa binadamu inahimizi kilimo hiki cha tumbaku. Je, Serikali haioni kufanya hivi ni kupunguza nguvukazi ya Taifa hili?

**NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge, anataka kujua kwamba, Serikali itakuwa na mikakati gani ya kuhakikisha kwamba taasisi hizi ambazo zinafanya utafiti wa maradhi ya binadamu hasa maradhi sugu zinakwenda pia vijijini ili wanavijiji waweze kufaidi kutokana na utafiti huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ni rahisi kufika vijijini lakini naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, *AMREF* pamoja na *Ifakara Health Institute,* hata *NIMR* wana mikakati na *project* ambazo wanafanya zaidi vijijini. Tatizo ni kwamba; ni pale ambapo tunakuwa na utafiti wa *MEWATA* wanapotoa ushauri na kufanya utafiti, inabidi waende vijijini kwa sababu ndiko ambako wanapata miundombinu ya kuweza kuchukua vipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha tunahamasisha zaidi tafiti zifanyike vijijini ili tuweze kupata pia mwelekeo wa kuwasaidia Wanavijiji wa Kitanzania.

Swali la pili amesema kwamba, tumbaku inajulikana kwamba ndiyo inasababisha maradhi mengi; maradhi ya moyo, maradhi ya kansa na maradhi mengine, lakini Taifa hili linahamasisha ulimaji wa tumbaku. Naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna Watanzania ambao kipato chao kinategemea tumbaku na matumizi ya tumbaku siyo kwenye kuvuta sigara tu, inatumika pia kutengeneza *antiseptics.* Ninaomba niwahakikishie kwamba, kwa sababu tumeweka sheria na *regulations* kwamba anayetengeneza sigara ni lazima aandike kwamba tumia *at your own risk,* kwamba tumbaku ina maradhi; kwa hiyo, mimi ninaamini kwamba katika uvutaji tutaendelea kupunguza lakini kwa matumizi mengine ya kutengeneza *antiseptics* na dawa za wadudu, tutaendelea kupata faida kwani wakulima wetu wanapata kipato kupitia hiyo.

Namshukuru Mheshimiwa Rukia Ahmed, kwa kujali sana afya za Watanzania. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda haupo kabisa upande wetu.

Na. 51

**Chuo cha Wauguzi Wilayani Mpanda**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Serikali ilianzisha ujenzi wa Chuo cha Wauguzi Wilayani Mpanda, mahali kilipokuwa Chuo cha Maafisa wa Afya eneo la Hospitali ya Wilaya ya Mpanda:-

(a) Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo hicho?

(b) Je, Serikali haioni kuwa kama itakamilisha ujenzi huo na kuanza kwa mafunzo ya wauguzi kutasaidia kuondoa tatizo la upungufu wa wauguzi kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mpanda, Vituo vya Afya na Zahanati za Vijijini kwenye Wilaya ya Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa ukarabati wa Chuo cha Mpanda ulianza kutekelezwa mwezi Agosti mwaka 2008. Mradi huu ambao unatekelezwa na mkandarasi mmoja anaitwa *Ngole Engineering*, haukuendelea kama ilivyotarajiwa kwa kuwa ulikumbwa na tatizo la kutokuwa na fedha za malipo. Hatimaye katika Mwaka wa Fedha wa 2011/12, ukarabati wa mabweni ya wanafunzi, jengo la utawala, madarasa, maktaba na bwalo la chakula ulianza. Mkandarasi anatarajia kuwasilisha Wizarani Hati Na. 2 kwa ajili ya malipo katika wiki ya tatu ya mwezi Februari 2012. Ukarabati wa majengo haya unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Mei, 2012 endapo fedha zitapatikana kama inavyotarajiwa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kukamilisha ujenzi wa majengo ya Chuo cha Mpanda ili Chuo hicho kianze udahili wa wanafunzi ifikapo Septemba 2012. Chuo hicho kitaanza kutoa mafunzo ya Tabibu Wasaidizi *(Rural Medical Aid)* na baadaye kitatoa mafunzo katika fani za Uuguzi,

Maabara, Afya ya Mazingira na Famasia ili kukidhi mahitaji ya Wataalam katika vituo vya afya na zahanati katika Halmashauri zilizopo katika Mkoa mpya wa Katavi na Mikoa mingine hapa Tanzania.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mradi huu umechukua muda mrefu karibu miaka minne iliyopita; na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameahidi kwenye majibu yake kwamba Mradi huu utakamilika endapo fedha zitapatikana. Je, Wizara ina mpango mkakati gani kuhakikisha fedha hizo zinapatikana ili iweze kukamilisha Mradi katika muda uliopangwa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso, kama ifuatavyo:-

Ni kweli nimesema kwamba, kama fedha zitapatikana. Sisi tunakwenda kwa *cash budeget* na hizi ni hela ambazo zinatokana na fedha za maendeleo. Ninaamini kwamba, kwa sababu tumeshaanza kumlipa mkandarasi na tutamlipa tena mwezi Februari, Serikali itaendelea kutupa fedha kwa sababu sisi wote tuna nia na madhumni ya kuhakikisha kwamba, chuo hiki kinajengeka kwa sababu tunahitaji Wataalam ili tuweze kufanikisha Mradi wetu wa Mpango wa Afya ya Msingi (MMM). Bila kufanya hivyo hatutaweza kupata Wataalam wa kufanya kazi kwenye zahanati zinazojengwa vijijini pamoja na Vituo vya Afya.

Naomba nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba, awe na amani, tutajitahidi Chuo hicho kitajengeka. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaomba majibu ya uhakika kwa swali namba 52 kwa sababu ni muhimu sana.

Na. 52

**Mmiliki wa *Jambo/Jamii FORUM***

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MHE. MCH. DKT. GETRUDE P. RWAKATARE)** aliuliza:-

*Jambo Forum/Jamii Forum* imekuwa ikisambaza habari za uwongo kwa watu mbalimbali bila kuchukuliwa hatua:-

Je, ni nani mmiliki wa *Jambo/Jamii Forum?*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mch. Dkt. Getrude Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, *Jambo/Jamii Forum* ni mtandao wa kijamii ambao haujasajiliwa Tanzania bali umesajiliwa nje ya nchi. Mmiliki wa mtandao huu wa kijamii anaweza kuwa Mtanzania au Mwananchi yeyote ambaye siyo Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* inatoa leseni mbalimbali za kusimamia mawasiliano nchini, ikiwa ni pamoja na leseni ya huduma za matumizi ya mtandao *(Application Service License)* na leseni za utangazaji *(Content Service License).*

Katika usimamizi wa TEHAMA, Mamlaka inatoa leseni inayotambulika kama leseni ya huduma ya mtandao kwa watoa huduma wakubwa na kuwawezesha kuhakikisha kuwa huduma ya mtandao inapatikana nchini. Wenye leseni za aina hii hutoa huduma ya kuhifadhi (*hosting*), mitandao mbalimbali ikiwemo ya kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa huduma za mtandao hupelekea watu mbalimbali kuanzisha tovuti za kijamii. Uanzishwaji wa tovuti za kijamii haulazimishi mtu kujisajili wala kujitambulisha na huanzishwa na mtu yeyote aliye popote duniani.

Kutokana na asili na miundo na Tovuti za kijamii, mamlaka haijasajili wala kutoa leseni kwa tovuti hizo. Kimsingi, maudhui yanayoandikwa katika tovuti hizo za kijamii ni maoni ya mtu binafsi na yasiyoangaliwa iwapo ni ya kweli au la.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri aliyoyatoa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Kwanza kabisa tukubaliane baadhi ya ujumbe unaoandikwa katika mitandao hii kwa kweli ni maudhi, tena maudhi makubwa. Wakati mwingine ni matusi hata matusi ya nguoni ambayo ni kinyume kabisa na utamaduni wa Mtanzania:-

(i) Je, Serikali iko tayari kuleta sheria hapa Bungeni ili kuweza kuwabana basi hao Watanzania ambao wanajitokeza kuandika maneno ya matusi na mengine ya uchochezi katika mitandao hii ili kukomesha tabia hii?

(ii) Katika huduma za *internet café* ambazo zinatolewa hapa Tanzania nyingi zinaruhusu hata watoto wadogo kuingia kutumia *internet café* hizo. Kwa kiwango hicho basi huwa na *access* ya kuweza kusoma hata mitandao ambayo inafundisha ngono kabla ya wakati. Je, hilo nalo Serikali ipo tayari kuleta sheria hapa ili kuelekeza wenye *internet café* kuangalia ni umri gani ambao unahurusu watu kuingia katika mitandao hiyo? Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, ukizingatia swali la msingi hasa kuhusu *Jamii Forum* na matatizo yake makubwa. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ngoye, kama ifuatavyo:-

Kwanza, kuhusu Sheria; ipo katika mchakato na imefikia katika ngazi ya juu ya kuweza kuleta Muswada wa Sheria ya Habari hapa Bungeni. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, awe amejiandaa na awe katika wakati mzuri wa kuweza kuangalia na kuchangia katika sheria hiyo itakayozungumzia mambo ya habari hasa tukizingatia kwamba, habari inapatikana mahali popote; habari inapatikana kwa *television*, habari inapatikana kwa redio, habari inapatikana kwa gazeti na habari inapatikana kwa mitandao. Kwa hiyo, tuangalie hizi *media* zinazoweza kutoa habari mbalimbali ni kwa namna gani habari zote hizi zinazopatikana katika maeneo yote haya zitaweza kuleta tija katika Taifa letu.

Kuhusu *internet café* vilevile amezungumzia kuweza kuona vitu ambavyo tunadhani siyo maadili kwa watoto. Nizungumzie hili kwamba, anayemruhusu mtoto na anayetoa hela kwenda *internet café* ni sisi wazazi. Kwa hiyo, ni wazazi sisi ambao tunaruhusu watoto wetu kwenda ku-*access internet*. *Internet* siyo tu kwenye *internet café*, siku hizi simu zetu, *IPOD* zetu na *laptop* zetu katika nyumba zetu zinaweza kuchukuliwa na watoto wetu na wanaweza ku-*access*. Kwa hiyo, sisi wazazi tuchukue wajibu wetu kama wazazi kuhakikisha kwamba tunawaelekeza watoto wetu waweze kuangalia vitu ambavyo vina maadili na vinalijenga Taifa letu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, kama mnavyoona ninyi wenyewe ni mashahidi, nimwombe radhi Mheshimiwa Abdul Marombwa, kwa swali lake namba 53, inabidi libaki tutalitafutia utaratibu mwingine wiki ijayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni mbalimbali ambao wametufikia hapa Bungeni nao ni wageni sita wa Mheshimiwa Anna Abdallah kutoka Bodi ya Korosho Tanzania. Naomba niwatambulishe wageni hao ni Mama Karamagi; sidhani kama Bodi ya Korosho wapo. Naomba niwaruka na wale wengine. Bodi ya Korosho mpo? *Okay!* Basi yupo Mrs. Karamagi, baada ya yeye yupo Mrs. Hanifa

Karamagi, naona imejirudia, Mr. Ayub Mohamed Mbawa, Mrs. Teophora Nyoni, Mrs. Twahir Nzarawahe na Profesa Haji Semboya. Ahsanteni; karibuni sana ndugu zangu wa Bodi ya Korosho Tanzania.

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Magdalena Sakaya, ambaye ni Ndugu Adha Aboti Nyansuni; karibu sana kama upo simwoni.

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni Wananchi 15 wa Asasi ya *Youth Empowerment and Support* ya Dodoma; karibuni sana Vijana wa *Youth Empowerment and Support* na tunawatakia kila la kheri katika shughuli zenu mjifunze Bunge linavyofanya kazi.

Pia tuna wanafunzi 30 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; karibuni sana vijana wetu wa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma; mnakaribishwa tena na tena, hili ni Bunge lenu.

Matangazo mengine; tangazo la kikao kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, Mheshimiwa January Makamba, anawatangazia Wajumbe wake kwamba, leo tarehe 3 Februari 2012, kutakuwa na kikao muhimu cha Kamati kuanzia saa tano katika Ukumbi wa Msekwa B. Hapana, kutaneni kuanzia saa saba, kuna mambo muhimu ambayo yanaendelea hapa ni vizuri tuwe pamoja.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Angellah Kairuki, anawatangazia Wajumbe wa Katiba, Sheria na Utawala kwamba, leo tarehe 3 Februari 2012, saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati kitakachofanyika Ukumbi Namba 219, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Kaimu Katibu wa Wabunge wa CHADEMA, Mheshimiwa David Silinde, anawaomba Wabunge wote wa Chama hicho wakutane saa saba mchana katika ofisi yao ya Kambi ya Upinzani.

Katibu wa *Bunge Sports Club* anatangaza kwa wanamichezo kwamba, wanamichezo wote wanatangaziwa kwamba wale wanamazoezi wa Kikundi cha KITAMBI NoMA kutoka Zanzibar watawasili leo jioni. Kesho tarehe 4 Februari 2012 watakuwa Uwanja wa Jamhuri na wataendesha mafunzo ya mazoezi ya viungo kama mlivyotangaziwa awali. Mgeni rasmi anatajiwa kuwa Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Jumapili tarehe 5 Februari 2012 watakuwepo pia uwanjani hapo kwa ajili ya mazoezi; ni kikundi kinachoitwa Vijana NoMA. Kwa hiyo, wale wenzangu mimi tunakaribishwa sana wote na hasa kesho Jumamosi kwa ajili ya mazoezi maalum.

Mwisho nilikuwa nimepewa taarifa kwa Mheshimiwa Stephen Masele kuwa, amebarikiwa kupata mtoto wa kiumu tarehe 1 Februari 2012; hongera sana bwana. Kumbe na Wasukuma nao wanaweza. (*Makofi*)

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 5(1), naomba ninukuu: "Katika kutekeleza majukumu yake yaliyotajwa katika ibara ya 84 ya Katiba, Spika ataongozwa na Kanuni hizi na pale ambapo Kanuni hazikutoa mwongozo, basi Spika atafanya kazi kwa kuzingatia Katiba, Sheria nyingine za nchi, Kanuni nyingine zilizopo, maamuzi ya awali ya Maspika wa Bunge, pamoja na mila na desturi za Mabunge mengine yenye utaratibu wa Kibunge unaofanana na utaratibu wa Bunge la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna mambo mawili ambayo naomba kuyawekea mkazo; la kwanza ni kuongozwa kwa mujibu wa Katiba; na pili kuongozwa kwa mujibu wa mila na desturi na maamuzi ya awali ya Bunge. Nitaomba kwa ufupi ninukuu ibara ya 63(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayosema kwamba, sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho Chombo Kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya Wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.

Mheshimiwa Spika, tumekabidhiwa Orodha ya Shughuli za leo na moja ya shughuli zilizoorodheshwa ni kupokea kauli ya Serikali. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kauli hii ni ya jambo linaloihusu Serikali, kauli hii ni la jambo lisilozua mjadala.

Jambo ambalo linataka kutolewa kauli hivi sasa la mgomo wa Madaktari ni jambo ambalo Serikali ama Wizara inayohusika ni sehemu ya watuhumiwa. Mgogoro huu umefikia hapa kutokana na udhaifu na kutowajibika ipasavyo kwa Waziri wa Afya, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Wizara kwa ujumla wake katika utendaji kazi kuhusiana na kushughulikia madai ya Madaktari na masuala mengine yanayohusiana na Sekta ya Afya. Sasa ikitolewa kauli ya Serikali ambayo haijadiliwi, sisi kama Wabunge tutakosa fursa ya kuweza kuisimamia ipasavyo Serikali kuwawajibisha Mawaziri wenye dhamana na kadhalika, kwa kutaka uwajibikaji unaostahili na kuwawakilisha Wananchi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo basi, ningekuomba utumie mamlaka yako kwa maana kwa kutumia Kanuni niliyoisoma, Kanuni ya 5, uweze kutoa mwongozo kwa kuzingatia vilevile maamuzi ambayo Bunge hili limewahi kuyafanya huko nyuma ya kauli za Mawaziri wa Serikali kuruhusiwa kujadiliwa ili baada ya kauli hii kuwasilishwa, tuweze kupatiwa wasaa wa kuijadili ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa kuwaokoa Wananchi na vilevile kuwawajibisha waliohusika na kulifikisha Taifa hapa tulipofika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nimeombwa mwongozo nitautoa hapo baadaye kidogo.

## KAULI ZA MAWAZIRI

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea mgogoro wa Madaktari nchini mwetu. Jambo hili limeleta usumbufu mkubwa kwa Watanzania waliohitaji huduma za kitabibu katika Hospitali za Serikali na Hospitali Binafsi zinazopata ruzuku kutoka Serikalini. Serikali inapenda kutoa taarifa ya namna ilivyoshughulikia mgogoro huu kwa mujibu wa Kanuni ya 49 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro huo ulianza na Wataalam mbalimbali wa Afya; Madaktari, Madaktari wa Meno, Wauguzi, Wafamasia, Wataalam wa Maabara na kadhalika, walio katika mafunzo kwa vitendo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na katika baadhi ya hospitali hapa nchini, wakidai posho zao za mwezi Novemba na Desemba 2011. Kutokana na hali hiyo, Wataalam hao waliamua kutoingia kazini mpaka madai yao yatakapotekelezwa na Serikali. Katika kuepuka athari zaidi, Serikali ililipa kiasi cha shilingi 876,961,000 ambacho ndiyo ilikuwa madai ya posho hizo.

Pamoja na Serikali kufanya malipo hayo, Wataalam hao waliendelea na mgomo. Katika hatua ya kushangaza, tarehe 11 Januari 2012, Madaktari kupitia Chama cha Madaktari Tanzania *(MAT)*, nao waliingia katika mgogoro kwa kuunga mkono mgomo huo na kutoa madai mengine mapya. Hata hivyo, wakati Serikali ikiendelea na mazungumzo na *MAT,* Jumuiya ya Madaktari Tanzania iliingilia kati nafasi ya *MAT* na kutoa madai mengine mapya. Jumuiya hiyo iliunda Kamati ya Mpito chini ya Bwana Ulimboka Steven. Hali hii ilifanya mazungumzo baina ya Serikali na Madaktari kuwa magumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichukua hatua zifuatazo katika kukabiliana na hali hii:-

- Vilifanyika vikao mbalimbali kati ya Viongozi wa Wizara, Wawakilishi wa *Interns* na Taasisi walizokuwa wanafanyia mazoezi kwa vitendo Wataalam hao ili kuwafahamisha jitihada za Wizara katika kutatua tatizo lillilojitokeza. Jitihada hizo ni kama ifautavyo: Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, walikutana na Viongozi wa Madaktari hao tarehe 27 na 28 Desemba 2011 na kuwaomba waendelee na kazi wakati jitihada za kuwapatia posho zao zikiendelea.

- Tarehe 2 Januari, 2012 Mganga Mkuu wa Serikali alikutana na wawakilishi 21 wa Wataalam walio katika mazoezi kwa vitendo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Tanga, Arusha na Hospitali za Rufaa za Mkoa wa Dar es Salaam (Amana, Mwananyamala na Temeke), ambapo aliwaeleza kuwa Wizara imeshafanikiwa kupata pesa ya kuwalipa *Interns* hao. Hivyo basi, aliwasihi wawaeleze wenzao kuhusu taarifa hiyo.

- Mnamo tarehe 3 Januari 2012, Viongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Serikali kutoka Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, walifanya mkutano wa pamoja na *Interns* wote katika Ukumbi wa *Central Pathology* – Muhimbili na kuwafahamisha kuwa tatizo la posho zao limeshatatuliwa; hivyo basi, warudi wodini waendelee na kazi wakati taratibu za malipo zikiendelea.

- Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kulipa posho hizo tarehe 5 Januari 2012 na imetumia kiasi cha shilingi 876,961,000 kwa ajili ya kuwalipa *Interns* wote 756 katika vituo vyote. Hata hivyo, baada ya malipo haya baadhi ya *Interns* waliokuwa Hospitali ya Taifa Muhimbili hawakurudi kazini mara moja. Kitendo hiki kiliilazimisha Wizara kupeleka *Interns* wengine 41 waliokuwa wakisubiri kuanza mazoezi kwa vitendo mwezi Januari 2012 ili kuchukua nafasi za *Interns* waliokuwa katika mgomo. Kutokana na uamuzi huo, Uongozi wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, ulilazimika kuchukua hatua ya kuwarudisha Wizarani *Interns* wote waliogoma kwenda kazini ili wapangiwe vituo vipya. Hatua hii ilichukuliwa ili kuzuia athari ambazo zingeweza kujitokeza kwa wagonjwa.

- Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hii, Wizara ilifanya tathmini ya suala la idadi ya *Interns* wanaotakiwa kuwepo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Tathmini hiyo ilionesha kuwa ni *Interns* 150 tu ndiyo wanaohitajika kufanya mazoezi kwa vitendo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ili kupata uzoefu wa vitendo utakaowawezesha kwenda kutoa huduma bila usimamizi wa karibu. Hata hivyo, kwa sasa kuna *Interns* 174 katika Hospitali hiyo, waliobaki walisambazwa katika hospitali nyingine za Dar es Salaam kama ifuatavyo:-

(i) Hospitali ya Taifa Muhimbili – Madaktari 86, Wafamasia 35 na Wataalamu wa Maabara 13; jumla yao ni 134.

(ii) Hospitali ya Rufaa ya Temeke – Madaktari 9, Wafamasia 2 na Mtaalamu wa Maabara 1; jumla yao ni 12.

(iii) Hospitali ya Rufaa Amana – Madaktari 13, Wafamasia 3 na Wataalamu wa Maabara 3; jumla yao ni 19.

(iv) Hospitali ya Rufaa ya Mwananyamala – Madaktari 10, Wafamasia 2 na Wataalamu wa Maabara 4; jumla yao ni 16.

(v) Hospitali ya Jeshi Lugalo – Madaktari 7.

(vi) Hospitali ya Aga Khan – Madaktari 5 na Wafamasia 2; jumla yao ni 7.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Interns* hao waliichukulia hatua hii kama ni adhabu na hivyo kutotekeleza mpangilio huo mpya. Kati ya Madaktari wa *Intern* waliogoma Hospitali ya Taifa Muhimbili, hakuna waliopangwa nje ya Dar es Salaam. Wizara iliwapangia wote katika Hospitali za Dar es Salaam ili kuwapunguzia usumbufu ambao ungeweza kutokea kama wangepangwa nje ya Dar es Salaam. Aidha, hakuna *Intern* aliyefukuzwa kufanya mazoezi kwa vitendo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Interns* waliokuwa wakifanya mazoezi kwa vitendo katika Hospitali za KCMC, Mount Meru, Bombo, Bugando na Manispaa za Dar es Salaam, walitambua jitihada za Wizara za kushughulikia tatizo hili na waliendelea na ratiba yao ya mazoezi kwa vitendo. Tunatoa shukrani zetu kwao kwa kuonesha ujasiri na moyo wa uzalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushiriki wa Chama cha Madaktari Tanzania *(MAT)* katika mgogoro: Ilipofikia tarehe 11 Januari 2012, suala la *Interns* hao lilichukuliwa na Chama cha Madaktari Tanzania *(MAT)*, ambapo Chama hicho kiliongeza madai mengine ambayo yanahusiana na maslahi pamoja na marupurupu mengine ya Madaktari wote kama ifuatavyo:-

(i) Madaktari kupewa nyumba za kuishi.

(ii) Kuongeza Posho ya Kuitwa Kazini Baada ya Saa za Kazi (*On Call Allowance)*.

(iii) Rufaa za wagonjwa, hasa Viongozi, wanaopelekwa kutibiwa nje ya nchi kutokufuata taratibu.

(iv) Malipo kwa ajili ya udhamini kwa Madaktari wanaochukua Mafunzo ya Uzamili.

(v) Posho ya Mazingira Hatarishi (*Risk Allowance*).

(vi) Kuhamisha Madaktari Bingwa wenye mikataba ya ajira na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Uongozi wa Chama cha Madaktari *(MAT)* kutoa madai mapya, Wizara iliwasiliana na *MAT* na kuwaomba kukutana na Uongozi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili wajadiliane kuhusu hoja zilizotolewa na Chama hicho.

Mkutano huo ulifanyika tarehe 21 Januari 2012 kati ya Uongozi wa Wizara na ule wa *MAT*. Wizara ilitoa maelezo ya kina kuhusu madai yao.

Uongozi wa *MAT* ulielezwa kuwa Wizara ilikwishashughulikia suala la nyumba kwa Madaktari kwa kuwasiliana na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu – Hazina, kuhusu kurekebisha Waraka wa Utumishi Na. 3 wa Mwaka 2010 Kuhusu Posho za Nyumba kwa Viongozi wenye Stahili. Aidha, Wizara ilikwishapeleka mapendekezo ya kuboresha viwango vya posho wanavyolipwa Wataalam wa Afya wanapoitwa baada ya saa za kazi. Mwenyekiti wa Mkutano huo alikuwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kikao cha *MAT* na Uongozi wa Wizara, iliafikiwa kuwa Madaktari na Wataalam wengine waendelee na kazi wakati Wizara ikiendelea kutafuta ufumbuzi wa madai yao mengine. Mnamo tarehe 22 Januari 2012, Kamati ya *MAT* iliondolewa katika usimamizi wa madai hayo na nafasi yake kuchukuliwa na Kamati ya Mpito ya Jumuiya ya Madaktari chini ya Uenyekiti wa Bwana Ulimboka Steven.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa taarifa za Serikali, Bwana Ulimboka Steven siyo Mtumishi wa Umma na wala hajasajiliwa kama Daktari. Bwana Ulimboka Steven ni miongozi mwa Madaktari waliogoma mwaka 2005 na kuomba radhi kwa Mheshimiwa Rais. Inashangaza kuona namna alivyoingilia mgogoro huu na kupata uongozi wa Kamati hiyo!

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 26 Januari 2012, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, alikutana na vyombo vya habari ili kuufahamisha umma kuhusu hoja zilizotolewa na *MAT* pamoja na zilizoongezwa na Kamati ya Mpito chini ya Uongozi wa Bwana Ulimboka Steven.

Vilevile alielezea jitihada zilizochukuliwa na Serikali katika kutafuta ufumbuzi wa hoja hizo. Wizara ilitoa maelezo kuhusiana na hoja zao na ufumbuzi wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu haki ya Madaktari kupata nyumba: Serikali kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wizara ya Fedha, inarekebisha

Waraka Na. 3 wa Mwaka 2010 ili Madaktari waendelee kupatiwa nyumba bila kujali ngazi zao za mishahara. Vilevile pamoja na juhudi zinazofanywa na Mikoa na Halmashauri kuwapatia nyumba Madaktari, Serikali imepata fedha kutoka Mfuko wa Dunia *(Global Fund)*, kwa ajili ya kujenga nyumba 700 za Madaktari na kwa kuanzia, Wilaya 18 zilizo pembezoni zimechaguliwa kujengewa nyumba kumi kila Wilaya.

Ujenzi umeanza kwa baadhi ya Wilaya hizo kama sehemu ya kuboresha hali ya upatikanaji wa nyumba kwa Wataalamu wa Afya na Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza Posho ya Kuitwa Kazini Baada ya Saa za Kazi *(On Call Allowance):* Wizara imefanyia kazi maboresho ya Posho hiyo ya Kuitwa Kazini Baada ya Saa za Kazi *(On Call Allowance)* na imewasilisha mapendekezo kwa mamlaka husika kwa ajili ya kupata kibali. Mapendekezo hayo yanatofautisha posho hiyo kulingana na ngazi za Madaktari na Watumishi wengine. Hata hivyo, viwango vilivyopendekezwa havikuwa vinazingatia asilimia ya mshahara kama wanavyodai.

Mheshimiwa Naibu Spika, rufaa za wagonjwa hasa Viongozi wanaopelekwa kutibiwa nje ya nchi: Malalamiko mengine ya Madaktari hao ni kwamba, baadhi ya Viongozi wa Kisiasa na wa Serikali, hushinikiza Madaktari wanaowahudumia kuwapa rufaa ya kwenda kutibiwa nje ya nchi hata kwa magonjwa yanayoweza kutibiwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utaratibu uliopo, mgonjwa hupata rufaa kwenda nje ya nchi baada ya Jopo la Madaktari Bingwa wa fani husika wasiopungua watatu kuthibitisha kuwa ugonjwa husika hautibiki nchini na hivyo mgonjwa huyo apelekwe nje ya nchi. Madaktari hao wana uhuru wa kuandika katika fomu ya rufaa kama mgonjwa anastahili kupelekwa nje ya nchi au la.

Baada ya mapendekezo hayo, Wizara hugharamia matibabu hayo bila kujali hali ya kijamii au kisiasa ya mgonjwa ilimradi vigezo vimetimizwa. Aidha, Madaktari hao walieleza pia kwamba, katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi wa Oktoba hadi Desemba 2011, jumla ya wagonjwa 223 walipelekwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu. Kati ya wagonjwa hao ni 19 tu (8.5%), walikuwa Viongozi wa Serikali na Wanasiasa (Waheshimiwa Wabunge na Viongozi Waandamizi Serikalini).

Mheshimiwa Naibu Spika, malipo kwa ajili ya udhamini kwa Madaktari wanaochukua Mafunzo ya Uzamili: Malalamiko mengine ya Madaktari ni kwamba, baadhi ya Madaktari waliopata nafasi ya kuchukua Mafunzo ya Uzamili mwaka 2011/2012 katika vyuo mbalimbali walikosa udhamini wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya mwaka 2005/2006, Madaktari 50 tu kwa mwaka ndiyo waliokuwa wakipata udhamini kwa Mafunzo ya Uzamili. Baada ya kuanza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), idadi imeongezeka maradufu.

Kuanzia mwaka 2006/2007, waliongezeka na kuwa Madaktari 132, mwaka 2007/2008 Madaktari 146, mwaka 2008/2009 Madaktari 170, 2009/2010 Madaktari 265, mwaka 2010/2011 Madaktari 250 na mwaka 2011/2012 Madaktari 90.

Udhamini wa Serikali katika mwaka 2011/2012 umepungua kutokana na ukweli kwamba, bado Madaktari wengine wanaendelea na mafunzo hayo vyuoni na kupungua udhamini wa Wadau wa Maendeleo. Hata hivyo, Wizara inafanya jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya udhamini wa Madaktari zaidi kwa mwaka huu. Tayari baadhi ya Wadau wa Maendeleo wapo tayari kusaidia au kuchangia gharama za mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko mengine ni kuhusu Wizara kuwahamisha Madaktari Bingwa iliyoingia nao mkataba wa udhamini wa Mafunzo ya Uzamili na wakati huo huo wakiwa na mikataba ya ajira na Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya kuhamisha madaktari hao bingwa ni kusogeza huduma za ubingwa kwa wananchi kutokana na kupandishwa hadhi Hositali za Mikoa kuwa Hospitali za Rufaa. Utaratibu huu umezua mgogoro kubwa na madaktari hao kwa kuwa hawapo tayari kwenda mikoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu posho ya mazingira hatarishi *(risk allowance),* Serikali ilijumuisha posho mbalimbali kwenye mishahara ya watumishi, posho ya mazingira hatarishi ikiwa ni mojawapo ya posho hizo. Hata hivyo, Serikali imetambua umuhimu wa kutenganisha posho hizo na mishahara kwa watumishi wa kada za afya wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka husika wanalifanyia kazi suala hili. Hata hivyo, madaktari wanataka ongezeko la asilimia 30 na lianze kutekelezwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ongezeko la kima cha chini cha mshahara wa madaktari, mishahara ya watumishi wa umma hufuata miundo ya utumishi *(scheme of service)* iliyopo. Aidha, Serikali imeboresha muundo wa watumishi wa sekta ya afya. Baada ya kuboreshwa kwa muundo huo, kwa hivi sasa, watumishi wa afya wanapata mishahara mikubwa kuliko watumishi wengine Serikalini. Hata hivyo, madaktari wanataka mshahara kwa daktari anayeanza kazi kutoka shilingi 957,700/= anazolipwa sasa mpaka shilingi 3,500,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa madaktari niliotoa siku ile nilivyoongea na vyombo vya umma, Wizara ilitoa wito kwa madaktari wote kurudi na kuendelea kufanya kazi za utabibu ili kuokoa maisha ya Watanzania, kama tulivyokubaliana katika kikao na viongozi wa *MAT* waliokuja Wizarani tarehe 21 Januari, 2012. Ni vyema madaktari wakatambua juhudi zinazofanywa na Serikali za kuboresha maslahi ya watumishi wa sekta ya afya, kama ilivyoelezwa hapo juu na kuziunga mkono. Hata hivyo, Serikali ilitamka kuwa milango iko wazi kwa majadiliano zaidi na viongozi husika.

Mheshimiwa Naibu spika, mkutano kati ya viongozi wa Serikali, *TUGHE* Taifa na madaktari waliokuwa kwenye mgomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maagizo ya Waziri Mkuu, tarehe 27 mwaka huu mimi Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Hadji Hussein Mponda (Mbunge) nikiongozana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Mheshimiwa Hawa Ghasia, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na viongozi wa *TUGHE* Taifa na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili walikutana na madaktari chini ya uongozi wa Bwana Ulimboka Steven katika ukumbi wa *Starlight.*

Baada ya kujitambulisha kwa madaktari, kiongozi wao Bwana Ulimboka Steven alieleza kuwa hawako tayari kufanya mazungumzo na ujumbe uliotumwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na badala yake walitoa madai yao ambayo wanataka yawasilishwe kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kimsingi, madai yaliyotolewa hayakuwa na tofauti sana na yale ya *MAT* isipokuwa walitaka utekelezaji huo uanze mara moja, tena kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kupata maelezo ya kina kutoka kwa viongozi ambao alitutuma aliagiza akutane na madaktari hao pamoja na viongozi mbalimbali katika ukumbi wa Karimjee tarehe 29 Januari, 2012. Lengo la kikao hicho lilikuwa kujadili hoja za madaktari hao. Lakini madaktari ambao walikuwa katika mgomo hawakuweza kuhudhuria kikao hicho, hivyo Mheshimiwa Waziri Mkuu akazungumza na wananchi juu ya mgogoro huo kupitia vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda sasa tuangalie sababu zilizowafanya madaktari hao kutokuhudhuria kikao hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku moja kabla ya kikao hicho madaktari waliokuwa kwenye mgomo walimwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba hawakuwa tayari kuhudhuria kikao hicho kutokana na

sababu zifuatazo tena majibu ya barua hiyo walipeleka saa tatu usiku kwenye Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu pale nyumbani kwake.

Kwanza kwamba hawako tayari kukutana naye Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe ile 29 Januari, 2012 kwa sababu walipanga kukutana na wenzao kutoka mikoani tarehe 30 Januari, 2012 kabla ya kukutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Pili, walitaka Ofisi ya Waziri Mkuu iwajibu kwanza madai yao kwa maandishi kabla ya kukutana na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili wapate nafasi ya kujadili hoja moja baada ya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, walitaka wakati wakienda kuongea na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali itoe tamko kwamba hakutakuwepo na adhabu yoyote kwa madaktari au watumishi wa kada yoyote ya afya itakayotolewa kutokana na mgomo au mgogoro unaoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na vikwazo hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu alifika eneo la mkutano na alizungumza na wananchi kupitia vyombo vya habari na katika maelezo yake alifafanua kwa kina suala la ongezeko la mshahara mpya uliopendekezwa na madaktari kama ifuatavyo:-

Kwanza madaktari wanalalamika kuwa daktari anayeanza kazi analipwa mshahara mdogo wa 700,000/= kwa mwezi. Madai hayo si ya kweli kwa sababu katika ajira ya Serikali, madaktari wapya wanaoajiriwa wanalipwa shilingi 957,700/= wakati watumishi wa kada zingine kama wahandisi wanaanza na shilingi 600,000/=. Wahasibu wanaanza na mshahara wa shilingi 469,200/=, hivyo basi, madaktari ndiyo wanalipwa zaidi. Mapendekezo yao ni kuwa daktari anayeanza kazi alipwe shilingi 3,500,000/= kwa mwezi pamoja na asilimia 120 ya mshahara huo kama malipo ya posho mbalimbali wanazodai.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za madai ya madaktari kwa bajeti ya Serikali, ili kuhakikisha kunakuwa na hali ya utulivu katika mazingira ya kazi, utekelezaji wa pendekezo la madaktari la kulipa mshahara wa shilingi 3,500,000/= kwa mwezi kwa daktari atakayeanza kazi, utailazimu Serikali kurekebisha viwango vya mishahara kwa watumishi wote wa kada za afya pamoja na kada nyingine ili kuweka uwiano kufuatana na stahiki za miundo katika utumishi wa umma *(scheme of service)*.

Kwa mujibu wa mapendekezo yao, kiwango cha kuanzia mishahara kwa mhudumu wa afya kitakuwa shilingi 670,316/= na mshahara wa juu kwa kada za afya utakuwa shilingi 8,145,573/= kwa mwezi. Utekelezaji wa pendekezo hili utagharimu jumla ya shilingi 83,508,834,430/= kwa mwezi ambayo ni sawa na shilingi 417,544,172,150/= kwa kipindi kilichobaki cha miezi mitano ya mwaka huu wa fedha tuliokuwa nao.

Mheshimiwa Nainu Spika, kwa mujibu wa mapendekezo ya madaktari ya mshahara pamoja na posho mbalimbali, daktari anayeanza kazi atapata jumla ya shilingi 7,700,000/= kwa mwezi ikijumuisha mshahara na posho zile nyingine ambazo nimetaja jumla ni asilimia 120. Aidha, kwa mujibu wa mapendekezo hayo, Daktari Mshauri Mwandamizi atapata shilingi milioni 17.2 kwa mwezi.

Kwa kuzingatia ukubwa wa gharama hizo utekelezaji wa mapendekezo ya madaktari utakuwa hauwezekani kwa kuzingatia hali halisi ya Bajeti ya Serikali. Madaktari hao wanadai kwamba watumishi wa kada nyingine za afya wapandishiwe mishahara na posho zao. Hivyo basi endapo nao watapewa fedha wanazodai, Serikali itapaswa kulipa shilingi 202,413,397,568.00/= katika makundi haya mawili tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza yao ya mishahara ni sawa na shilingi trilioni moja kwa mwaka, ukijumlisha na nyongeza ya posho zao wanayodai ya shilingi moja karibu na *point* 30.3 unapata karibuni hapa shilingi trilioni mbili ambayo ni karibu na theluthi mbili ya mishahara ya wafanyakazi wote Serikalini ambayo kwa sasa ni shilingi trilioni 3.45. Kwa mantiki hii, kiasi kinachobakia cha theluthi moja ndicho kigawanywe kwa watumishi wengine wote wanaotumikia umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya Serikali kuhusu mgogoro huu ni kama yafuatavyo, baada ya kutoa ufafanuzi wa madai mbalimbali ya madaktari, Mheshimiwa Waziri Mkuu alitamka yafuatayo, siku ile ya tarehe 29 Januari, 2012 pale Karimjee:-

Kwanza katika hatua iliyofikiwa, Serikali imetambua kwamba madaktari wanaongozwa na Kamati ya mpito, hawataki suluhu licha ya juhudi zote ambazo zimefanywa na Serikali za kuwaita ili kushughulikia madai yao.

Pili, kuanzia tarehe ile tarehe 29 Januari, Serikali inawahimiza madaktari wote walio katika mgomo kuacha mara moja na kurudi kazini ifikapo tarehe 30 Januari, mwaka huu na watakaoshindwa kufanya hivyo, watakuwa wamepoteza ajira zao.

Tatu, Serikali tayari imechukua tahadhari ya kukabiliana na hali hii kwa kuagiza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kupeleka baadhi ya madaktari wake katika Hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam ili kusaidia wagonjwa walioko hospitalini. Huduma katika hospitali husika zimeanza kutengemaa. *(Makofi)*

Nne, aidha, Serikali inatoa shukrani kwa *TUGHE* kwa kuwa wametambua hoja za madaktari, lakini wakasema njia wanazotumia na madaktari hawa kuwasilisha madai yao kwa kugoma si sahihi. Hivyo basi, imeendelea kuwashawishi na kuwasihi madaktari kurudi kwenye mazungumzo na Serikali.

Tano, Serikali inasisitiza kuwa mgomo wa madaktari si halali kwa sababu kisheria hawapaswi kugoma. Masharti haya yanaainishwa katika kifungu cha 77(1)(a) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (Na. 6 ya mwaka 2004) ambayo inazuia kugoma watumishi wote walio katika huduma muhimu *(necessary services).*

Sita, vilevile, Serikali inatoa shukrani kwa madaktari na wauguzi wote ambao walikuwa kazini wakiendelea kutoa huduma kwa wagonjwa na kwa kutambua hali ilivyo, walikutana na kuwasihi madaktari wenzao waache mgomo na kurejea kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe taarifa ya tathmini ya huduma ya matibabu nchini baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu Kutoa tamko la kusitisha mgomo kwa madaktari hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika kutekeleza agizo hili, imekuwa ikifanya tathmini kuanzia ile tarehe 30 Januari, 2012 hadi sasa kwa kutembelea Hospitali za Mkoa wa Dar es Salaam na kupata taarifa kutoka mikoa yote juu ya hali ya huduma za afya nchini.

Aidha, Wizara imefuatilia kwa karibu mahudhurio na utendaji wa wafanyakazi katika hospitali zote nchini kama ifuatavyo:-

Kwanza, huduma katika Hospitali za Taifa. Katika Hospitali ya Taifa Muhimbili huduma zimeanza kutengemaa. Tatizo lililokuwepo Kitengo cha Dharura limetatuliwa, kwa kupeleka madaktari 15 kutoka Jeshini (JWTZ). *(Makofi)*

Pili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili *(MOI)* huduma za dharura na wodini zimedorora. Madaktari 21 hawajarudi kazini. Mipango ya kupeleka madaktari kutoka Jeshini inakamilishwa ili huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* zirejeshwe. Hata hivyo, *Interns* wengi bado hawajarudi kwa idadi ya kuridhisha katika maeneo mengi ya Hospitali ya Muhimbili.

Tatu, Taasisi ya Saratani *Ocean Road (ORCI)* huduma zimerudi kama kawaida. *(Makofi)*

Katika Hospitali za Rufaa za Kanda, Hospitali ya Rufaa ya Bugando huduma zinaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Katika Hospitali ya Rufaa ya *KCMC* - baada ya *Interns* wote 81 kurudi kazini, huduma zinaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Katika Hospitali ya Rufaa ya Mbeya baada ya *Interns* wote 65 kurudi kazini, huduma zinaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Katika Hospitali za Manispaa za Dar es Salaam baada ya *Interns* 75 kurudi kazini pamoja na madaktari waajiriwa, huduma zinaendelea kama kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali za Rufaa za Mikoa baada ya *Interns* wote kurudi kazini hali ya huduma katika Hospitali za Dodoma, Morogoro na Tanga zimerudi kama kawaida. Mikoa mingine iliyobaki haikujihusisha na migomo, hivyo basi hali ya huduma haikuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufuatilia kwa karibu utoaji wa huduma katika hospitali zilizokumbwa na migomo ili au mgomo ili kuchukua hatua za haraka kutatua matatizo pale yatakapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zaidi zilizochukuliwa, tarehe 30 Januari, 2012 Serikali iliunda Kamati ya kushughulikia maazimio yaliyowasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ili Kamati hiyo iyachambue na kutoa maoni na mapendekezo yatakayoisaidia Serikali kumaliza mgogoro wa watumishi wa sekta ya afya. Kamati hiyo imeshaanza kazi na inaundwa na wajumbe wafuatao; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Mwenyekiti, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii – Katibu, Wizara ya Fedha- Mjumbe, *TUGHE* – Mjumbe, mwakilishi wa madaktari - Mjumbe na mwakilishi wa wauguzi – Mjumbe.

Kamati hii pia imeongezewa Wajumbe wengine kutoka TAMISEMI, Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba unipe dakika mbili nimalizie hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kulihakikishia Bunge lako Tukufu na Umma wa Watanzania kuwa Serikali imedhamiria kwa dhati kulitatua tatizo lililopo mbele yetu. Kwa mantiki hiyo, tunawasihi madaktari, wataalam wengine wa sekta ya afya na wadau wote wa sekta hiyo kutumia fursa iliyo mbele yetu kutoa maoni yao kwenye Kamati iliyoundwa na Serikali ili kupata namna bora ya kutatua mgogoro uliojitokeza na kuepuka migogoro kama hiyo katika siku zijazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inasikitika kwa athari zilizotokea kwa wananchi kutokana na mgogoro uliotokea. Narejea kusema kuwa ni matumaini ya Serikali kuwa pande zote mbili katika mgogoro huu zitafikia muafaka na kuumaliza mgogoro huu kwa manufaa ya umma wa Watanzania.

Mwisho, napenda kutoa shukrani kwa viongozi wa taasisi na hospitali za mikoa zilizokumbwa na mgogoro huu ambao walisimama kidete kutetea haki za wagonjwa. Vilevile, ningependa kusisitiza wito wa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa madaktari na wataalam wengine wa afya kusitisha mgomo na kurudi kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, Mungu ibariki Afrika, Mungu ibariki Tanzania. *(Makofi)*

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Nilikuwa naomba kutumia Kanuni ya 55 Kifungu kidogo cha (3)(a) kutengua Kanuni ile ya 49 ambayo hairuhusu Kauli za Serikali kutokujadiliwa Bungeni ili Bunge lako liweze kujadili Kauli ya Serikali ambayo imewasilishwa na...

**NAIBU SPIKA:** Soma hiyo 55(3)(a) soma.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, inasema kwamba 3(a) hoja zifuatazo zinaweza kutolewa bila taarifa. Hiyo (a) hapa inazungumzia kutengua Kanuni yoyote kati ya Kanuni hizi. Sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 49 kile kifungu kidogo cha (2) hakiruhusu au hakitoi fursa kwa Kauli za Serikali kutokujadiliwa ndani ya Bunge. Nilikuwa naomba tutengue Kanuni ile kwa kutumia hii, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ambayo imetolewa na Serikali leo ni kauli muhimu sana, ni kauli ambayo inahusu afya za Watanzania, ni kauli ambayo inahusu watu ambao tunatumia fedha nyingi sana kuwafanya wawepo kwenye vituo vya afya na hospitali na hospitali za rufaa kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ambazo tunazipata hivi sasa. Nasema ninachotaka kusema...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa unajadili au? Maana nilishashika Kanuni nataka kujua unajielekeza wapi?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hoja hii ijadiliwe. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Machali ametoa hoja, haikuungwa mkono na mtu yeyote na Mheshimiwa Zitto ametoa hoja, haikuungwa mkono na mtu yeyote, kinachobakia hapa ni ombi la Mwongozo la Mheshimiwa Mnyika, alilolitoa mwanzoni kabla ya Mheshimiwa Waziri kutoa Kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili kupitia utaratibu wa Kauli za Mawaziri. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 49 kwa ajili ya sote hapa na wanaotusikiliza kuweza kufuatilia ambayo ndio Mwongozo wetu katika jambo hili inasema Waziri anaweza kutoa Kauli Bungeni kuhusu jambo lolote linalohusu Serikali.

Kauli za aina hiyo zinaweza kutolewa kwa idhini ya Spika, katika wakati unaofaa kufuatana na mpangilio wa shughuli za Bunge na zitahusu jambo mahususi, halisi na zisizozua mjadala na muda wa kusema utakuwa ni dakika zisizozidi 30. Na ya tatu ile kwa faida ya Waheshimiwa Mawaziri, ni kwamba Waziri mwenyewe mwenye kutoa kauli, atawajibika kutoa nakala za kauli yake kwa Wabunge wote, wakati anapowasilisha Bungeni.

Sasa ni kweli, jambo hili limejitokeza leo siku ya nne mfululizo. Kwa siku tatu zilizopita na leo Waheshimiwa Wabunge, wamekuwa wakisimama na kuomba sana kwamba jambo hili lijadiliwe na Bunge na tukawa tumeshauri kwamba ni jambo bora kuisikiliza Serikali kwanza, kuhusiana na jambo hili; na Serikali ikatujia kwa utaratibu wa Kauli za Mawaziri, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, jambo ambalo tumelisikiliza muda si mrefu uliopita.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyosema katika siku zote nne, suala hili ni suala nyeti, ni suala zito, linalohusu maisha na uhai wa watu wetu wanaohitaji huduma na tiba nchi nzima. Lakini matakwa ya Kanuni yetu ndio hayo, yanatufunga kwa Kauli za Mawaziri, kujadili Kauli wakati huo huo baada ya uwasilishaji wake. Hii inatupa fundisho kwamba huko mbele ya safari tutakapoziangalia Kanuni zetu tena upya, basi Waheshimiwa tujaribu kukumbuka kuiangalia Kanuni yetu hii kama tunapaswa kuendelea nayo hivyo hivyo ilivyo au itahitaji marekebisho ya msingi.

Lakini jambo hili lina unyeti wa kipekee; na unyeti wake unatokana na kwamba ni jambo linalohusu mgogoro, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya, ni mgogoro wa pande mbili na sisi hapa Waheshimiwa Wabunge, kupitia kwetu kwenda kwa wananchi tumepata maelezo ya upande mmoja. Na katika utaratibu wetu wa Bunge, haiwezekani kabisa madaktari wakaja hapa na wenyewe wakatoa upande wao ili unapojadili, Mheshimiwa Mbunge, uwe katika nafasi ambayo wenzetu wanasema uko-*informed* sawa sawa.

Kwa hiyo, tukisema kwa kilichosemwa hapa tujadili wakati hatujui chochote kuhusu upande wa pili, sijui kama tutakuwa tumejitendea haki hata sisi wenyewe! *Unless* kama sisi wenyewe tuko *informed* na upande wa pili. *(Makofi)*

Lakini pia katika *submission* ya Kauli ya Mheshimiwa Waziri ya madai yale yaliyodaiwa na Madaktari, hata Mheshimiwa Waziri Mkuu ambaye tunamshukuru sana alipolishughulikia suala hili alipoenda kule kukutana nao na wao hawakujitokeza, lilikuwepo dai moja ambalo sijalisikia likizungumziwa hapa na ni vigumu kuzungumziwa! Nalo ni kwamba hawa mabwana wanadai kwamba katika Wizara ya Afya kuna baadhi ya watendaji wakuu wenye uwezo mdogo wa utendaji na wa kiuongozi, wasiowajibika ipasavyo. Na hawa watendaji wana kauli za kashfa na dharau kwa madaktari. Kwa kutegemea timu ile iliyoundwa na Serikali itakayoripoti kule kule, itakuwa ni vigumu vilevile kupata ukweli wa upande huu wa pili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, kwa kutumia Kanuni za uendeshaji bora wa shughuli za Bunge na mamlaka ambayo kiti kimepewa, mimi ninaamua ifuatavyo; kulipeleka suala hili kwenye Kamati

ya Huduma za Jamii ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Mama Margaret Sitta na Makamu wake Mheshimiwa Dokta Faustine Ndugulile, ili Kamati hiyo ikae na Serikali, ikae na upande wa madaktari bila kubagua, ikutane na Jumuiya ya Madaktari, ikutane na Chama cha Madaktari, ikutane na Madaktari Bingwa au wadau wengine itakaoyoona yenyewe Kamati wanafaa katika suala hili; kwa haraka iwezekanavyo Kamati hii ifanye kazi hii. Kamati hii itakapokuwa tayari, mimi naamini tunaweza tukafika mahali ambapo tunaweza tukaona namna ya kusonga mbele kwa jambo hili. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huu ndio Mwongozo wangu kuhusu jambo hili. Ahsanteni sana. Katibu. *(Makofi)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu wa Mwaka 2012**
***(The Anti-Money Laundering (Amendments) Bill, 2012)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaingia katika Muswada wa Sheria ya Serikali, *The Anti-Money Laundering Amendment Bill, 2012.* Naomba nimwite Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkulo.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu yaani *The Anti Money Laundering (Amendment) Act, 2012* pamoja na marekebisho yake sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Fedha na Uchumi, chini ya Uenyekiti wake Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, Mbunge wa Handeni kwa kujadili kwa kina Muswada huu na kutoa ushauri thabiti uliotusaidia katika kukamilisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu umezingatia kwa kiasi kikubwa ushauri na mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada ulio mbele yetu una lengo la kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa utelekezaji wa sheria hii ili kuweka mfumo madhubuti na imara wa kudhibiti uhalifu wa fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunavyofahamu Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423 ilipitishwa na Bunge mnamo mwaka 2006 kwa lengo la kwanza, kudhibiti na kuzuia uhalifu wa fedha haramu kwa kutambua kuwa fedha haramu ni kosa la jinai, pili, kuanzisha Kitengo kinachojitegemea cha Kudhibiti Fedha Haramu *(The Financial Intelligence Unit (FIU)*, tatu, kuweka masharti kwa benki, taasisi za fedha na mamlaka za usimamizi kuwasilisha katika Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu taarifa zenye mashaka kuhusu fedha haramu na nne, kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya wataalamu ya Ushauri wa Udhibiti wa Fedha Haramu yenye wajumbe kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar. Aidha, Sheria hii inaorodhesha makosa yanayohusu fedha haramu na kuweka adhabu kwa makosa hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha takriban miaka mitano tangu kutungwa kwa Sheria hii, umejitokeza upungufu katika utekelezaji wake ambao unahitaji marekebisho ili kudhibiti ipasavyo uhalifu wa fedha haramu. Aidha, kwa nyakati tofauti wadau mbalimbali wamebainisha upungufu mbalimbali katika wa utekelezaji wa sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maudhui ya Muswada. Muswada huu unakusudia; kwanza, kuwezesha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu Sura ya 423 kutumika Tanzania Bara pekee isipokuwa kwa maeneo mahsusi yaliyobainishwa ndani ya Muswada, pili kuwa na mfumo imara wa kisheria wa kudhibiti fedha haramu Tanzania kwa kuziba mianya mbalimbali inayowezesha kutendeka kwa uhalifu unaozalisha fedha haramu na ufadhili wa ugaidi kwa kuongeza makosa ya ziada katika orodha ya makosa yanayozalisha fedha haramu, tatu, kupunguza uhalifu nchini na nne, kuwezesha taasisi za fedha kubadilishana taarifa za wateja zinazohusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi endapo zitaona umuhimu wa kufanya hivyo kwa lengo la kudhibiti uhalifu huu kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kuendeleza utulivu wa kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa kuwa na mfumo madhubuti wa kisheria *(legal framework)* unaodhibiti fedha haramu kwa viwango vinavyokubalika Kimataifa.

Sita, kuunga mkono juhudi za Kimataifa katika kuzuia uhalifu huu ili kuimarisha uchumi tulivu na endelevu, saba, kuongeza uwajibikaji kwa taasisi za fedha kutoa taarifa za mashaka *(suspicious transaction reports)* kuhusu fedha haramu na nane, Kitengo cha *FIU* na Mamlaka za Usimamizi kupewa uwezo wa kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa vyombo vinavyosimamiwa na mamlaka hizo na kuchukua hatua za kiutawala kwa watakaokiuka matakwa ya sheria hii. Aidha, kwa kushirikiana na mamlaka za usimamizi, Kitengo cha *FIU* kitaweza kufanya ukaguzi wa utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya mambo muhimu yaliyozingatiwa katika Muswada huu ni yafuatayo:-

Kwanza, kurekebisha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423 ili iweze kutumika Tanzania Bara pekee, isipokuwa kwa maeneo yanayohusu mamlaka na majukumu ya Kitengo cha *FIU* na majukumu ya Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Ushauri wa Udhibiti wa Fedha Haramu ambayo yanatambuliwa na Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mali Athirika ya Tanzania Zanzibar Namba 10 ya mwaka 2009 na pili, kurekebisha Sheria ili kukiwezesha Kitengo cha *FIU* kutekeleza majukumu yake kwa uhuru na ufanisi.

Tatu, kurekebisha Sheria ili kuongeza kifungu cha sheria kinachompa mamlaka Kamishna wa Kitengo cha *FIU* kuzuia kwa muda kuendelea kwa shughuli inayotiliwa mashaka iliyowasilishwa kwa ajili ya uchunguzi Kitengo cha *FIU*.

Nne, kurekebisha Sheria ili kuainisha utaratibu wa ajira, madaraka, ukomo wa ajira na kuondolewa madarakani kwa Kamishna wa Kitengo cha *FIU* na kumtambua Kamishna kuwa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuuli.

Tano, kurekebisha Sheria ili kuwezesha Mamlaka za Usimamizi *(Regulatory Authorities)* kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu kwa vyombo vinavyosimamiwa na mamlaka hizi na sita, kurekebisha Sheria ili kutoa adhabu mbalimbali *(sanctions)* dhidi ya yeyote atakayekiuka Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Kanuni na Miongozo yake.

Saba, kurekebisha Sheria ili kuwezesha Kitengo cha *FIU* kuelekeza watoa taarifa kuwasilisha taarifa na kukusanya taarifa kutoka kwa watoa taarifa *(Reporting Persons)* na vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria *(Law Enforcement Agencies).*

Nane, kurekebisha Sheria ili kuongeza kifungu kitakachoainisha wajibu wa watumishi wa Kitengo cha *FIU* kutunza siri wakati na baada ya ajira. Aidha, marekebisho haya pia yatahusu watu wengine wenye taarifa kuhusu utekelezaji wa sheria hii.

Tisa, kurekebisha Sheria ili kuwezesha Kitengo cha *FIU* au Mamlaka ya Usimamizi kupeleka maombi mahakamani kwa lengo la kuiomba mahakama kuzifungia kwa muda au kuziweka chini ya uangalizi wa Mamlaka ya Usimamizi *(Regulator)* taasisi au makapuni yaliyotiwa hatiani kwa makosa ya fedha haramu na kumi, kurekebisha sheria ili kuongeza orodha ya mamlaka za usimamizi ambazo zitashirikiana na Kitengo cha *FIU* katika utekelezaji wa sheria hii kama watoa taarifa. Mamlaka hizo ni pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii, Wakala wa Usajili wa Makampuni na Majina ya Biashara, Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Msajili wa Vyama Visivyokuwa vya Kiserikali, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Msajili wa Hati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja ni kurekebisha sheria ili kuongeza katika orodha, watoa taarifa wengine kama *pension funds manager, securities market intermediaries, financial leasing entities, micro-financing companies, savings and credit cooperative societies, na housing financing companies.*

Kumi na mbili, kurekebisha sheria ili kuziwezesha taasisi za fedha kubadilishana taarifa za wateja zenye mashaka kuhusu fedha haramu na ufadhili wa ugaidi pale taasisi hizi zitakavyoona inafaa na kumi na tatu, kurekebisha sheria ili kuongeza orodha ya ripoti zitakazowasilishwa katika Kitengo cha *FIU* na

watoa taarifa. Ripoti hizo ni pamoja na *Currency Transaction Reports, Cross Border Currency Reports* na *Electronic Funds Transfer Reports.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na nne, kurekebisha Sheria ili kuongeza mwakilishi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Ushauri wa Udhibiti wa Fedha Haramu na kumi na tano, kuyatambua kwa kuongeza orodha ya makosa yanayozalisha fedha haramu *(Predicate Offences).*

Kumi na sita, kuongeza kifungu kitakachoweka utaratibu na mamlaka ya Mahakama Kuu wakati wa kushughulikia kesi inayomhusu mtuhumiwa ambaye sio raia wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika vifungu 20 kama ifuatavyo:-

Kifungu cha Kwanza kinahusu jina la Muswada na kubainisha kwamba marekebisho ya sheria hii yatasomwa pamoja na sheria mama yaani *The Anti Money Laundering Act, Cap 423.*

Kifungu cha Pili cha Muswada kinarekebisha kifungu cha pili cha Sheria ili kuwezesha Sheria hii kutumika Tanzania Bara pekee, isipokuwa maeneo yanayohusu Kitengo cha *FIU* mamlaka na majukumu yake na Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Ushauri wa Udhibiti wa Fedha Haramu. Masuala haya yanatambuliwa na Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Mali Athirika Namba 10 ya mwaka 2009 ya Tanzania Zanzibar.

Kifungu cha Tatu cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha tatu cha Sheria ili kuongeza na kurekebisha tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika katika Sheria kama ifuatavyo:-

(a) Tafsiri zilizoongezwa ni pamoja na;

(i) Tafsiri ya maneno *Law Enforcement Agency* ambapo itajumuisha Jeshi la Polisi, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, Uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi nyingine za kiuchunguzi zinazoshughulikia masuala ya udhibiti wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

(b)Tafsiri zilizofanyiwa marekebisho ni;

(i) Neno *Regulator* limerekebishwa ili kujumuisha baadhi ya mamlaka za usimamizi ambazo hazikujumuishwa hapo awali katika sheria hii. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Hifadhi ya Jamii, Msajili wa Vyama vya Ushirika, Msajili wa Hati, Mamlaka ya Usimamizi wa Nishati na Maji, Kituo cha Uwekezaji Tanzania, Wakala wa Usajili wa Makampuni na Majina ya Biashara, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na Msajili wa Vyama Visivyokuwa vya Kiserikali.

(ii) Neno *Predicate Offence* limerekebishwa ili kuongeza orodha ya makosa yanayozalisha fedha haramu.

(iii) Neno *Reporting Person* limerekebishwa ili kuongeza idadi ya watoa taarifa.

(iv) Neno *Terrorist Financing* limerekebishwa ili tafsiri yake iwiane na tafsiri iliyopo katika Sheria ya Udhibiti wa Ugaidi, Sura 19 yaani *The Prevention of Terrorism Act, Cap 19.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha Nne cha Muswada kimerekebishwa ili kuongeza aina nyingine za taarifa ambazo zitawasilishwa katika Kitengo cha *FIU*. Taarifa hizo ni pamoja na *Currency Transaction Reports, Cross Border Currency Reports* na *Electronic Funds Transfer Reports* zitakazosaidia upatikanaji wa taarifa katika *database* ya Kitengo cha *FIU*. Aidha, Kifungu kipya cha 4(3) cha Muswada kinatoa uhuru kwa Kitengo cha *FIU* katika matumizi ya bajeti wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tano cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha tano cha Sheria kwa kuongeza vifungu vipya ili kumpa Kamishna wa Kitengo cha *FIU* wadhifa wa Mtendaji Mkuu na Afisa Masuuli, kuweka masharti ya kazi ya Kamishna kwa kubainisha kipindi cha ajira na ukomo

wake pamoja na utaratibu wa kumuondoa endapo atashindwa kutekeleza majukumu yake au atatuhumiwa kwenda kutenda makosa yaliyobainishwa. *(Makofi)*

Aidha, kabla ya kuondolewa kwa Kamishna madarakani Mheshimiwa Rais ataunda ya uchunguzi ili kumshauri hatua za kuchukua. Kifungu hiki kinampa mamlaka Mheshimiwa Rais kumsimamisha kazi Kamishna wa *FIU* wakati uchunguzi dhidi yake ukiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha sita cha Muswada kinarekebisha kifungu cha sita cha sheria ili kitengo cha *FIU* kuwa na uwezo wa kukusanya taarifa kutoka kwa watoa taarifa yaani *reporting persons* na vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria *in law enforcement agencies*. Aidha, kitengo cha *FIU* kitaandaa taarifa za mara kwa mara kuhusu mienendo na mbinu zinazotumika katika kutenda uhalifu wa fedha haramu.

Vilevile kifungu cha 6(k) cha Muswada kinapendekeza marekebisho ili kuwezesha Kitengo cha *FIU* kuwa na uhuru wa kufanya ukaguzi kwa ushirikiano au pasipo kushirikiana na taasisi za usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha sita kimefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu kipya cha pili ambapo Kamishna wa Kitengo cha *FIU* amepewa mamlaka ya kusitisha muamala unaotiliwa mashaka yaani *suspension transaction* kwa kipindi cha siku tano za kazi ili kukiwezesha Kitengo cha *FIU* kufanya uchambuzi na ufuatiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha saba cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha saba cha Sheria ili kuongeza kifungu cha 7(5) kitakachoainisha wajibu wa watumishi wa Kitengo cha *FIU* kutunza siri wakati na baada ya ajira na pia kubainisha adhabu kwa atakayekiuka matakwa ya kifungu hiki cha Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha nane cha Muswada kinarekebisha kifungu cha nane cha Sheria ili kuongeza katika orodha ya wajumbe mwakilishi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Ushauri wa Udhibiti wa Fedha Haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha tisa cha Muswada kinarekebisha kifungu cha tisa cha Sheria kwa kuongeza masuala yanayohusiana na ufadhili wa vitendo vya ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha kumi cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 13 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kipya kitachowezesha Kitengo cha *IFU* au mamlaka ya usimamizi kuwasilisha maombi Mahakamani kwa lengo la kuiomba Mahakamani kuzifungia kwa muda au kuziweka chini ya uangalizi wa mamlaka ya usimamizi au kuzifungia kwa kipindi hicho chote Taasisi ama kampuni zilizotiwa hatiani kwa makosa yanyohusu fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 11 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 16 cha Sheria kwa kuweka utaratibu wa kutunza kumbukumbu mbalimbali za wateja, kuwasilisha kwa wakati kumbukumbu hizo katika Kitengo cha *FIU*. Aidha, mtoa taarifa atakayekiuka matakwa ya Sheria atawajibishwa kwa kutumia adhabu za kiutawala au kushtakiwa kwa kosa la jinai.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 12 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 17 cha Sheria  ili kubainisha kwamba utaratibu wa kutunza kumbukumbu utaainishwa kupitia kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 13 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 19 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kipya cha 19(a); kuwezesha kitengo cha *FIU* pamoja na mamlaka za usimamizi kuchukua hatua za kiutawala kwa watakaokiuka matakwa ya vifungu vya 15, 16, 17 na 18 vya Sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15 cha Muswada pamoja na marekebisho kinarekebisha kifungu cha 21 cha Sheria kwa kuongeza kifungu kidogo cha 21(2) ili kuwezesha mabenki na taasisi ya fedha kubadilishana taarifa na wateja zinazohusu fedha haramu na ufadhili wa vitendo vya ugaidi pale ambapo benki husika itakapoona inafaa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 16 cha Muswada kinafanyia marekebisho kifungu cha 22 cha Sheria ili kuongeza idadi ya watoa taarifa watakaopewa kinga dhidi ya mashtaka ya aina mbalimbali wakati wakitekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 15 cha Muswada, kinafanyia marekebisho kifungu cha 23 cha Sheria; kwanza kuweka masharti kwa wasafiri wanaotoka na kuingia ndani ya nchi, kutoa taarifa yaani ku-*declare* kuhusu kiasi cha fedha walizonazo ambazo zimezidi kiwango kitakachowekwa na Waziri mwenye dhamana ya fedha kupitia tangazo la Serikali.

Pili, kuwezesha, *FIU* kufungua akaunti maalum kwa ajili ya kuhifadhi fedha zitakazotwaliwa na Idara ya Forodha kutokana na ukiukwaji wa masharti yaliyowekwa chini ya kifungu hiki.

Tatu, kifungu kipya cha 23(5) kitakachobainisha kwamba itakuwa ni kosa la jinai kwa mtu atakayetoa taarifa zisizo sahihi yaani *false declaration* na kubainisha adhabu kwa kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 18 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 26 cha Sheria ili kuwezesha taarifa ya ukaguzi wa mahesabu ya kitengo cha *FIU* kuwasilishwa Bunge na Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 19 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 18 cha Sheria kwa kuongeza vifungu vipya vitatu vya 28(a),(b) na (c). Kifungu cha 28(a) kinabainisha kwamba mtu yeyote anayehusika katika utekelezaji wa Sheria hii na kutoa taarifa kwa wasiohusika atakuwa ametenda kosa la jinai.

Aidha, kifungu cha 28(b) kinaainish aadhabu za ujumla; yeyote atakayekiuka matakwa ya sheria yaliyoainisha kupitia vifungu mbalimbali vya sheria ambavyo adhabu zake hazijabainishwa. Kifungu kidogo cha pili kinaruhusu kushtakiwa kwa watendaji na maafisa wa ngazi za juu katika kampuni na au taasisi itakayohusika na ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kipya cha 28(c) kinabainisha kwamba Mahakama kuu itakuwa mamlaka ya kushughulikia kesi inayomhusu mtuhumiwa raia wa kigeni aliyefanya uhalifu nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo pia ni kosa chini ya sheria hii na kukimbilia Tanzania ambapo utaratibu wa kumrejesha nchini kwake kwa ajili ya kumshtaki kwa uhalifu hauwezi kufanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 20 cha Muswada kinarekebisha kifungu cha 29(2) cha Sheria kwa kuongeza maeneo ambayo Waziri mwenye dhamana wa Sheria hii anaweza kuandaa kanuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza hapo awali, kutokana na upungufu mwingi uliojitokeza katika Sheria ya sasa ni dhahiri kuwa marekebisho yaliyobainishwa katika Muswada huu yanahitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo, kwa hoja yako ambayo imeungwa mkono na kwa hiyo sasa tunaweza tukaendelea kwa kumuomba Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, anakuja Mwenyekiti mwenyewe, Mheshimiwa Dokta Abdallah Kigoda, karibu sana Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH O. KIGODA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii kwa mujibu wa kanuni wa 86(5) ya Kanuni za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Toleo la mwaka 2007 niweze kutoa maoni na ushauri kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipewa kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada ambao una lengo la kuondoa upungufu uliojitokeza katika utekelezaji wa Ssheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu, Sura ya 423 iliyopitishwa na Bunge mnamo mwaka 2006:-

(i) Kwa lengo la kudhibiti na kuzuia udhibiti wa biashara ya fedha haramu;

(ii) Kuanzisha kitengo kinachojitegemea cha kudhibiti biashara ya fedha haramu *the financial intelligence unit*;

(iii) Kuweka masharti kwa benki, taasisi za fedha na mamlaka za usimamizi kuwasilisha taarifa zenye mashaka kuhusu biashara ya fedha haramu; na

(iv) Kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Wataalam ya Ushauri wa Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza kazi hiyo kikamilifu kwa kushirikiana na Waziri wa Fedha, pamoja na watendaji wa Wizara yake, taasisi zinazoratibu masuala ya fedha, wanasheria toka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na wadau wa masuala ya fedha. Kamati imezingatia ushauri na maoni ya baadhi ya wadau yaliyotolewa wakati wa kuujadili Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chimbuko la kuleta Muswada huu ni kuwezesha Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, Sura ya 423 kutumika Tanzania Bara pekee, kuwa na mfumo imara wa kisheria wa kudhibiti biashara hii kwa kuziba mianya mbalimbali ya uhalifu, kupunguza uhalifu nchini na pia kuwezesha taasisi za kifedha kubadilisha taarifa za watendaji zinazohusu biashara ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Mwisho, ni pamoja na kuendeleza utulivu wa kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa mfumo madhubuti wa kisheria pamoja na kuunga mkono juhudi za Kimataifa katika kudhibiti biashara ya fedha haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo Kamati ina maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa kwa vile marekebisho ya sheria hii yanajumuisha taasisi nyingi sasa. Jukumu la ushirikishwaji na uratibu wa vyombo vyote, hivi ni muhimu sana ili sheria itekelezeke kwa tija. Kwa vile wigo wa kutafuta taarifa umepanuliwa, mfumo na njia za kutoa taarifa uzingatie utekelezaji wa masuala muhimu pamoja na ufanisi.

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria hii vilevile imeongezea kazi *Financial Intelligence Unit* kuliko ilivyokuwa hapo awali ilipokuwa inashughulikia tu taarifa za mashaka, *suspicions reports*. Kitengo kisipopata taarifa hizi maana yake ni kwamba kilikuwa hakina kazi. Aidha, upanuzi wa idadi ya vyombo vya kutoa taarifa vitakavyoshirikiana na *Financial Intelligence Unit* vitawezesha kazi ya udhibiti ifanywe kwa tija na ufanisi kwa kupata taarifa nyingi na za kutosha.

(iii) Mheshimiwa Naibu Spika, sheria inatoa mamlaka kwa *Financial Intelligence Unit* kufungua akaunti maalum kwa ajili ya kuhifadhi fedha zitakazokamatwa na mamlaka ya mapato kutokana na ukiukwaji wa sheria hii. Kamati inashauri badala ya fedha hizi kuhifadhiwa na *Financial Intelligence Unit* zihifadhiwe Benki Kuu. Aidha, Kamati haijapata mantiki, Kamati iliyoundwa kwenye Sheria, kifungu cha 5(6) kuwa Benki Kuu ni Mjumbe na hapa hapa kuuliza katika Kamati hiyo Mwenyekiti atakuwa ni nani? Eneo hili lipatiwe ufafanuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo haya ya marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu yameongeza tafsiri mbalimbali ya maneno ya vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria pamoja na tafsiri mpya ya mamlaka ya usimamizi kwa kujumuisha vyombo vingine vya usimamizi. Wigo wa tafsiri ya makosa yanayosababisha matumizi ya fedha haramu (*predicate offences)* umekuwa mkubwa, Kamati inatoa angalizo kuwa wananchi wengi hawana elimu ya utekelezaji wa sheria hii, hivyo watakuwa hawajatendewa haki pale wanapotuhumiwa. Hivyo, elimu kwa umma inahitajika ili kuongeza tija ya utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Bunge lako Tukufu kupitisha Muswada huu wa Marekebisho, Kamati inasisitiza kuwa Wizara itayarishe haraka iwezekanavyo kanuni zote muhimu zitakazosimamia utekelezaji wa sheria hii ikiwemo ile ya kuweka ukomo wa kiasi cha fedha ambazo mgeni au mtu yoyote anatakiwa kutoka nazo nje ya Tanzania. *(Makofi)*

Kutokuwepo kwa kanuni hizi hadi sasa zinaleta hisia za utoaji wa viwango vikubwa vya fedha zetu nje ya nchi hii. Hili si jambo jema kwa maendeleo ya uchumi. Pia Kamati inasisitiza kuwa Benki Kuu ihakikishe inasimamia vizuri sheria za fedha ili kuhakikisha inalinda thamani ya shilingi za Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imefikia wakati wa nchi changa kama Tanzania kujiamulia mambo yake yenyewe kwa utaratibu unaofaa na kwa muda unaofaa. Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Madola, ni vyema tukafanya mambo yetu kwa usare na nchi nyingine za Jumuiya ya Madola tukitahadhari shinikizo la Mataifa makubwa au vyombo vya fedha vya duniani. Uundwaji wa Kikosi Kazi cha Fedha Duniani (*Financial Action Task Force),* kinachojumuisha nchi 33 pamoja na *ECAMLAG* vimeshaamua kupambana na uhalifu wa fedha duniani. Uboreshaji wa sheria hii kwa marekebisho yaliyofanyika yataimarisha zoezi zima la kupambana na uhalifu huu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea mema kitengo kinachojitegemea cha kudhibiti biashara ya fedha haramu, *Financial Intelligence Unit* na kuwa huru zaidi. Marekebisho haya yamempa mamlaka Kamishna kusitisha kwa muda usiozidi siku tano shughuli zote zenye taarifa za mashaka ili kufanyia ukaguzi unaostahili wa utekelezaji. Hali hii itasaidia kupunguza uingizaji au usafirishaji wa fedha haramu na kwa kuwa na mfumo imara wa udhibiti wa ufadhili wa shughuli zisizo rasmi pamoja na ugaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho ya sheria hii yatatoa fursa kwa mabenki na taasisi za fedha kuweza kushirikiana kwa ukaribu zaidi pamoja na kubadilisha taarifa muhimu za fedha kuhusu mwenendo wa fedha kwenye akaunti za baadhi ya wateja ambazo zinatia shaka. Hali hii itasaidia utendaji kazi wa haraka kwa kitengo cha udhibiti wa fedha haramu *Financial Intelligence Unit*. Hata hivyo, Kamati imesisitiza kuwa utekelezaji wa sheria hii unatakiwa uwe wa umakini mkubwa wenye kufuata taratibu zilizowekwa ili kuepuka usumbufu kwa wananchi na wageni na kuwafanya kutokuwa huru na biashara wanazozifanya.

Aidha, sheria hii isitumike kama chombo cha kuwagandamiza wananchi, taasisi au wafanyabiashara kwa ujumla wao kwa kuingilia shughuli zao za maendeleo kwa dhana tu ya usafi au uharamu wa fedha husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sheria hii unahusu viwango vikubwa vya fedha hivyo uadilifu na uaminifu wa watumishi wa Kitengo cha Kudhibiti Biashara ya Fedha Haramu unahitajika sana.

Marekebisho ya Sheria hii yamezingatia wajibu wa watumishi wa *Financial Intelligence Unit* kutunza siri watakazozifahamu wakati wakiwa kazini na baada ya kuacha. Aidha, adhabu kali itatolewa kwa mtumishi atakayebainisha kuvujisha siri. Aidha, marekebisho haya yatatoa fursa ya kutoa adhabu ya kiutawala kwa kampuni yoyote itakayokiuka masharti ya sheria hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujadili Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Biashara ya Fedha Haramu, Kamati imegundua kuwa kutakuwepo na mgongano wa kimawazo kati ya mamlaka za usimamizi na watoa taarifa kwa kuwa mtoa taarifa anaweza kuwa ndiyo mwenyewe mamlaka ya usimamizi na hivyo utekelezaji wa sheria hii unaweza kuwa mgumu na kupeleka taarifa zitakazopatikana kutokukidhi mahitaji kwa ajili ya utekelezaji. Suala hili lizingatiwe na lipatiwe ufumbuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwasilisha maoni na ushauri, sasa napenda kuwatambua kwa majina Wajumbe wa Kamati hii walioshughulikia maoni na ushauri wa Muswada huu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Eustas Katagira, Mheshimiwa Maulidah Komu, Mheshimiwa Dokta Binilith Mahenge, Mheshimiwa Devotha Likokola, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Abdulaziz Abood, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mheshimiwa Dokta William Mgimwa, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amour Amina Abdulla, Mheshimiwa Alhaj Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Andrew John Chenge na Mheshimiwa Joel Luhaga Mpina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo na Naibu Waziri, Mheshimiwa Gregory G. Teu na Pereira A. Silima, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa na kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kutoa shukrani kwako na kwa Mheshimiwa Spika, Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashilillah pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Michael Kadebe, Katibu wa Kamati ya Fedha na Uchumi kwa kukamilisha maandalizi ya Kamati kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii inawashukuru wadau wote waliojitokeza mbele ya Kamati kuwasilisha maoni na mapendekezo ambayo yamesaidia sana katika kuandika na kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono Muswada huu. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Fedha na Uchumi, Dokta Abdallah Kigoda, tunakushukuru sana.

Sasa naomba nimuite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Fedha na Uchumi. Namtambua Mheshimiwa Christina A. Mughwai.

**MHE. CHRISTINE L. MGHWAI (K.n.y. MHE. KABWE Z. ZITTO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto na kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 86(6), Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu wa mwaka 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha haramu ni biashara ambayo hufanyika bila kuwepo kwa mteja wa kuinunua biashara hii kwani mteja na mpokea mapato huwa ni mtu mmoja, kwa mujibu wa wataalam wa kushughulikia uhalifu huu wanasema kuwa, huwa inapitia katika hatua tano muhimu kabla ya kukamilika katika mzunguko wake, hatua hizo ni:-

(1) Tendo la kihalifu, hii ni kujipatia fedha kwa njia ambazo sio halali kama vile kufanya biashara haramu kama za madawa ya kulevya, ufisadi, rushwa na kadhalika.

(2) Fedha haramu kuingizwa kwenye mzunguko kupitia taasisi mbalimbali za fedha, hii ni mbinu ambayo hutumika katika kuhalalisha fedha hizo, kwa mfano, mtu kufungua kampuni ambayo inajihusisha na biashara mbalimbali tofauti hivyo kuweza kufungua akaunti benki kulingana na majina ya biashara husika na kwenye mabenki mbalimbali na hivyo hutumia akaunti hizo kuingiza fedha haramu kwa lengo la kuzisafisha.

(3) Fedha haramu husafishwa ili kuficha hatua ya kupatikana kwa fedha hizo kihalifu,hii ni mbinu ambayo hutumiwa na wahalifu katika kuhakikisha kuwa hawawezi kufahamika na vyanzo vya fedha husika, kwa mfano mtu huamua kununua vitu mbalimbali kama magari, kusafirisha fedha nje kwa kutumia mifumo ya kibenki, kuanza kujipatia mikopo, tenda na kadhalika.

(4) Fedha halali kuzaliwa, ni hatua ya mtuhumiwa kuanza kupokea faida kutokana na vitega uchumi mbalimbali alivyojiwekea kutokana na fedha haramu na hivyo kuwa na uwezo wa kuonesha vyanzo halali vya fedha zake.

(5) Fedha hutumika kihalali kwa mujibu wa sheria, mzunguko huishia kwenye hatua ya matumizi kuwa halali na hakuna uwezo wa kuendelea kumfuatilia tena .

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) ya mwezi Mei, 2011, ilionesha kuwa Mataifa yanayoendelea yameathiriwa zaidi kiuchumi na biashara hii ya fedha haramu kwani iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 9.7 bilioni mwaka 1990 na kufikia kiasi cha dola 26.3 bilioni mwaka 2008 kwenye nchi zinazoendelea (*LDCs*) na madhara yake ni makubwa kwani ilichangia kushusha kiwango cha thamani ya fedha za nchi hizo kwa kiwango cha asilimia 6.2 kwa mwaka katika kipindi husika. Hii inaonesha kuwa Tanzania hatuko kisiwani kwani nasi tuliathiriwa kwa kiasi hicho hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa letu limekuwa na sheria nyingi ambazo ziliwahi kutungwa kwa ajili ya kukabiliana ama kujaribu kuondoa tatizo la fedha haramu, rushwa na uhalifu uliopangwa hapa nchini mwetu tangu tupate uhuru na hii inathibitishwa na uwepo wa sheria zaidi ya 15 kuwahi kutungwa tangu uhuru na nitajaribu kuzitaja sheria hizi kama ifuatavyo:-

(1) *The establishment of the Permanent Commission of Inquiry or Ombudsman, 1966;*

(2) *The Foreign Exchange Control Act 1966;*

(3) *The Anti-Corruption Act 1971;*

(4) *The establishment of an anti-corruption squad in 1975;*

(5) *The Economic Sabotage Act 1983;*

(6) *The Economic and Organised Crime Act 1984;*

(7) *The Proceeds of Crime Act 1991;*

(8) *The Leadership Code (Declaration of Assets) Act 1995;*

(9) *The appointment of the Presidential Commission of Inquiry into Corruption, 1996;*

(10) *The BOT Circular to Banking and Non-Banking Financial Institutions, No. 8 of 2000, on Money Laundering;*

(11) *The Drugs and Illicit Traffic of Drugs Act 1995;*

(12) *The Arms and Ammunition Act 1991;*

(13) *The Mutual Assistance in Criminal Matters Act 1991; and*

(14) *The Tanzania Intelligence and Security Act 1998.*

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa pamoja na uwepo wa sheria zote hizi lakini bado kulikuwa na mianya ya biashara haramu ambazo zimekuwa zikifanyika kupitia maeneo mbalimbali.

Kwa mfano, mnamo mwaka 2001 jarida maarufu la Marekani la *Wall Street Journey* liliandika kuwa mtandao wa *Al-qaeda* ulikuwa unanunua *Tanzanite* kutoka Tanzania na kuitumia kibiashara katika kusafishia fedha zao haramu zilizokuwa zinapatikana kutokana na ugaidi.

Hoja hii ilitiwa chumvi zaidi na takwimu za mwaka 1999-2000 kuwa mauzo ya *Tanzanite* ya Tanzania nchini Marekani yalikuwa yamefikia kiasi cha dola 328 milioni, wakati takwimu ambazo zilikuwa Tanzania zikionesha kuwa tuliuza *Tanzanite* nchini Marekani zenye thamani ya dola 31 milioni tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kukosekana kwa mamlaka ya udhibiti wa majengo yaani *Estate Regulatory Authority* (*ERA*) kama ambavyo tuliwahi kusema kwenye hatuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni na kurejewa na ile wa Waziri Kivuli wa Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2011/2012, wakati wa Bunge la Bajeti ni dhahiri kuwa ongezeko la majengo mengi na kupanda kwa thamani ya ardhi kwa kiwango cha kutisha katikati ya Majiji yetu kwa kipindi cha miaka ya karibuni inapaswa kufuatiliwa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na uzoefu wa nchi mbalimbali kuwa katika ujenzi wa majengo mbalimbali huwa fedha hizi haramu huingizwa na kusafishwa ili kuwa kwenye mzunguko halali na wa kisheria na hasa ujenzi huo unapofanywa na watu ambao hawafahamiki wanafanya biashara gani ambayo inawawezesha wengine kujenga majengo marefu kwa kipindi kifupi lakini ya gharama kubwa sana. Hivi fedha wanazopata maharamia wa Kisomali wanapoteka meli huwa wanawekeza wapi? Kwani tunajua sote hali halisi ilivyo huko Somalia ya usalama mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa sheria zote hizi lakini mnamo mwaka 2004/2005 Taifa lilikumbwa na kashfa kubwa ya wizi wa fedha za umma, yaani ndani ya kipindi cha miaka miwili tu ziliibiwa fedha kutoka kwenye Benki kuu zaidi ya shilingi bilioni 288, ambazo ni kutoka akaunti ya *EPA* 133 Bilioni na Meremeta 155 Bilioni. Wizi huu ulifanikishwa kupitia taasisi zetu za fedha pamoja na uwepo wa sheria zote hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 2006 Serikali ikaleta Muswada Bungeni wa Sheria ya Kuzuia Fedha Haramu ili kuweza kutafuta ufumbuzi wa wizi huu na ili kuweza kuzuia usitokee tena, sheria hiyo ilipitishwa na Bunge na tangu wakati huo haijawahi kutungiwa kanuni za utekelezaji na hii ni kusema kuwa haijatekelezwa kwa ukamilifu wake. Kwa mfano, sheria iliyopo kifungu cha 23(1) kiliweka utaratibu wa fedha ambazo zinaingia na zinatoka nje ya nchi, lakini la kustaajabisha tangu wakati huo kwa kipindi cha miaka sita sasa, mipaka ya nchi imekua ikiachiwa holela na fedha nyingi zinatoka bila hata kujulikana, kutokana na kukosekana kwa utekelezwaji wa kifungu hiki cha sheria. Kifungu hiki kilimpa Waziri mwenye dhamana ya fedha mamlaka ya kuamua ni kiasi gani cha fedha kinaweza kusafirishwa nje ya nchi kikiwa kiasi tasilimu ambacho mtu anapaswa kuwa nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo yote hapo juu yanaonesha wazi kuwa tatizo sio sheria bali ni utekelezwaji wa sheria husika na mamlaka zinazopaswa kusimamia utekelezwaji huo kuwa ndio chanzo cha kupotea kwa fedha hizo, kama ambavyo *BOT* waliweza kushiriki kwa kushirikiana na mabenki mbalimbali katika kuhakikisha kuwa fedha haramu zinapitia kwenye mzunguko wote ili kuwa halali na hatimaye kuingia kwenye mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kweli tumedhamiria kuzuia biashara ya fedha haramu ni muda muafaka sheria zetu kuonekana hivyo, kwani sasa hivi hakuna katazo lolote kwa mtu kuondoka hapa nchini na fedha za kigeni kwa kadri anavyoona yeye inafaa. Utoroshaji wa fedha nyingi sana za kigeni umekuwa ndio jambo kubwa linalosababisha thamani ya shilingi yetu kushuka kila mara. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba mtu mmoja asiruhusiwe kuondoka na fedha taslim zenye thamani ya zaidi ya USD 10,000. Hoja ni kwamba je, ni kwa nini marekebisho haya ya sheria hayajaweka kiwango maalum cha fedha anachotakiwa mtu kuingiza au kutokanacho ndani ya nchi? Sambamba na hilo tunaitaka Serikali ilieleze Bunge ni utaratibu gani umewekwa wa kudhibiti mipaka yetu kwa wale wanaotorosha fedha nyingi za kigeni kwenda nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Muswada wa kudhibiti matumizi ya fedha haramu. Kwa ujumla maudhui ya Muswada huu yako wazi na hivyo Kambi ya Upinzani haina pingamizi na hilo. Jambo la kulizingatia ni kwamba uhalifu wa fedha haramu ni mtandao mkubwa sana ambao unahusisha watu wa

kada mbalimbali kutoka katika taasisi mbalimbali. Hivyo, tukumbuke kuwa kada hizo katika taasisi mbalimbali na wengine ndio hao hao wanaotakiwa wasimamie utekelezaji wa sheria hii, lakini inakuwa ndio wahusika katika uharamia huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tukio lililotolewa taarifa Mkoani Mbeya la msamaria mwema kutoa taarifa kuhusiana na mashine ya kutengeneza fedha bandia na Polisi waliukamata mtambo huo na mhusika kukamatwa, lakini baada ya muda mtuhumiwa akaachiwa na hivyo kupelekea maisha ya mtoa taarifa kuwa hatarini. Waziri wa Mambo ya Ndani pamoja na Mkuu wa Jeshi la Polisi wana taarifa na kesi hiyo. Kwa mantiki hiyo, sheria inaweza kuwa ni nzuri, lakini dhamira ya dhati ya wanaotekeleza hiyo sheria likawa ni tatizo kubwa sana kwani imani kwa wananchi katika utekelezaji wa sheria ni jambo la muhimu sana wakishaamini kuwa wakubwa au vigogo hawaguswi na Sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wanazo taarifa nyingi sana kuhusiana na wahusika wakubwa wa fedha haramu kwa ujumla wake, lakini wanaamini kuwa wakubwa au vigogo hawaguswi na sheria hiyo wakati wao ndio wahalifu wakubwa. Mfano mzuri ni wahusika wa madawa ya kulevya kama ambavyo Mheshimiwa Rais alivyokiri kuwa majina yao alikuwa nayo pamoja na wala rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuonesha kuwa dhamira ya kweli ni jambo linaloleta imani kwa wananchi, Bunge hili na Serikali vililikwishapatiwa taarifa rasmi kuhusiana na wizi wa kitaasisi unaoihusu kampuni ya Kagoda na jinsi fedha zilivyokuwa zikiingizwa kwenye benki ya *CRDB* lakini hadi sasa hakuna hatua yoyote iliyokwishachukuliwa kwa wahusika wa wizi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa utangulizi huo, naomba sasa nipitie baadhi ya vifungu ambavyo tunaona bado kuna haja ya kuviweka vizuri au kuvitolea ufafanuzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu kipya cha 4(3) kinaweka Kitengo kipya cha Kuzuia Biashara ya Fedha Haramu na chenye uhuru na kutengewa bajeti yake ili kutenda kazi zake kwa uhuru zaidi. Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kitengo hiki kiondolewe na kisiwe chini ya Wizara ya Fedha ili kiweze kuwa na uhuru wa kutosha kiutendaji na kiweze kufanya kazi zake kwa ufanisi tofauti na pendekezo la sasa kuweka kitengo hiki ambacho kinapewa mamlaka hata ya kuchunguza *(regulator)* wengine ambao wako chini ya Wizara ya Fedha au wanafanya kazi kwa maelekezo ya Wizara. Kumuondoa Mtendaji Mkuu wa Kitengo hiki ni mpaka Rais aunde Tume, sasa kwa nini awekwe chini ya Katibu Mkuu wa Wizara?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 5(6) pamoja na 5(7) kinachohusu jinsi ya kuondolewa kwa Mtendaji Mkuu wa Kitengo, kuwa Mheshimiwa Rais hatokuwa na madaraka ya kumwondoa ofisini Mtendaji Mkuu hadi Rais aunde Kamati itakayochunguza tuhuma na kumshauri Rais. Kamati inayoundwa yote inahusisha wateule wa Rais au watu ambao wanaweza kuwa wanatarajia maslahi ya kikazi kwa kukubaliana na matakwa ya Rais kwani wote ni wajumbe ambao wanapendekezwa kuingia kwa nyadhifa zao na ni watendaji katika vitengo mbalimbali na ambao kiutendaji wanapaswa kutokuwa na masilahi ya moja kwa moja ili waweze kutenda haki bila ya kuwa na mkinzano wa kimaslahi *(conflict of interest)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Kambi ya Upinzani inaona kuwa ingekuwa ni busara sheria ikatamka kuwa pale mtendaji huyo atakapokutwa na hatia ya kuondolewa kazini ni vyema hatua zaidi za kisheria zikatumika kwani ni dhahiri atakuwa amekiuka kanuni na masharti yanayomwongoza katika utendaji kazi wake wa kila siku. Kwa njia hii tutaondokana na tabia iliyozoeleka ya watendaji wa Serikali pale wanapoachishwa kazi kutokana na makosa mbalimbali hawafunguliwi mashtaka hata kama wameliingizia Taifa hasara kubwa. Mifano ni mingi na ni dhahiri kwa kila mtu. Pia wengine wakikutwa na makosa ya kiutendaji adhabu yao ni kuhamishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine na tatizo hili limeota mizizi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani tunataka Sheria iweke utaratibu kuwa kama ikibainika ametenda makosa sheria ichukue mkondo wake kwani huyu ni mtu ambaye ni muhimu katika kusimamia uchumi wetu na kuondoa matumizi ya fedha haramu ambazo zimekuwa zikishiriki kudidimiza uchumi wetu kwa kushusha thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 10 cha Muswada kinachofanyia marekebisho kifungu cha 13 cha sheria kwa kuongeza kifungu kipya cha 10(2) kitakachowezesha kitengo cha *FIU* au Mamlaka ya Usimamizi kupeleka maombi Mahakamani kwa lengo la kuiomba Mahakama kuzifungia kwa muda au kuziweka chini ya uangalizi wa Mdhibiti taasisi au makampuni yaliyotiwa hatiani kwa makosa ya biashara ya fedha haramu. Kwa mujibu wa tafsiri mpya iliyotolewa katika Muswada huu, *regulator* ni pamoja na Benki Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hapa ni kwamba, kutokana na historia ya matukio ya nyuma, *money laundering* imekuwa ikihusisha taasisi za fedha na taasisi hizo kwa kiasi kikubwa fedha zinazohusika zina mkono wa moja kwa moja na Benki Kuu. Sasa kama Benki kuu imekuwa inahusika ni kwa vipi itachukua jukumu la kuwa mwangalizi wa taasisi ambayo inatuhumiwa kuwa inafanya au imejihusisha na fedha haramu. Mfano, Fedha za Meremeta zilitoka Benki Kuu na Akaunti ya *Deep Green* ikafunguliwa *NBC* siku ya mapumziko bila ya kufuata utaratibu. Je, kwa hili Benki Kuu inapata wapi uhalali wa kuwa *regulator*? Je, kwa hili Benki Kuu inapata wapi uhalali ama usafi wa kuwa mdhibiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 28B kinapendekeza adhabu ya jumla kwa mtu kuwa faini ya juu ni shilingi milioni 500 na kiwango cha chini ni shilingi milioni 100 au kifungo kisichozidi miaka mitatu, wakati kwa kampuni au taasisi kiwango cha adhabu ni kuwa faini isiwe chini ya shilingi milioni 500 .

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu wa kutoza faini ni dhahiri kuwa haukufikiwa kwa kuzingatia kigezo chochote kile kwani haijabainisha kuwa ni kiwango gani cha fedha kitapaswa kulipiwa faini hiyo na hivyo kinaweza kutumika kama kishawishi katika kuvutia wahalifu na hasa makampuni kutumia mwanya huu kupitisha fedha nyingi haramu kwani wanajua kuwa wakibainika wana uwezo wa kulipa faini hiyo na kuendelea na biashara zake kama kawaida.

Kambi ya Upinzani, inaona faini hizi haziko kiuhalisia, hivyo tunaona faini ziwekwe kwa kutumia asilimia ya fedha atakazotuhumiwa nazo na kiwango hiki kiwekewe jedwali kuwa kama mtu binafsi atakuwa amehusika katika kutenda kosa, basi kiasi cha fedha ambazo zimepatikana kutokana na uhalifu huo kitozwe faini ya asilimia 50 na kwa upande wa taasisi zitozwe kiasi cha asilimia 65 ya fedha zote zinazohusishwa pamoja na kupewa adhabu ya kufungiwa kuendelea na biashara kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja .

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya Bunge lako kukubaliana na pendekezo hili la Serikali la kupitisha mabadiliko haya, yafaa kwanza likapewa majibu kwenye mambo yafuatayo:-

(1) Kwa nini Sheria ya mwaka 2006 ambayo leo inatakiwa kubadilishwa haikutungiwa kanuni za utekelezaji? Je, nini kitatufanya tuamini kuwa hii itatekelezwa kikamilifu?

(2) Je, Mabadiliko haya yanatosha katika kukabiliana na changamoto mbalimbali za biashara ya fedha haramu?

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunakushukuru Mheshimiwa Christina Mughwai Lissu, kwa kutoa maoni hayo ya Kambi ya Upinzani. Sasa Waheshimiwa Wabunge tumeshasikia hoja, tumeshasikia maoni kutoka Kamati iliyochambua jambo lenyewe na maoni ya Kambi ya Upinzani. Tunaingia kwenye wachangiaji wetu. Ninao wachangaji saba na nimeshafunga orodha. Kwa hiyo, naomba msinilitee tena maombi mapya. Nafasi ya sasa itakuwa ya mchangiaji mmoja tu halafu jioni ya leo tutaendelea tena na kuhitimisha hoja hii.

Sasa naomba moja kwa moja nimuite mchangaji wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kwanza katika kuchangia Muswada huu. Lakini pili, niishukuru Serikali na Kamati na vilevile nimpongeze Msemaji,

Naibu Waziri Kivuli wa Fedha, kwa kuwasilisha maoni ya Kambi kwa usahihi kabisa na kwa namna ambayo imeeleweka vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana katika biashara ya fedha haramu na ni tatizo ambalo bado hatujaweza kuonesha dhamira ya dhati ya kulishughulikia. Utakumbuka kwamba, tulitunga sheria hii ambayo tunaifanyia marekebisho sasa mwaka 2006. Mwaka 2007 kitengo cha *Financial Inteligency Unit* cha Wizara ya Fedha kikawa kimeanzishwa, lakini kwa kiasi kikubwa bado hatujaweza kulieleza tatizo hili na kumekuwa na taarifa mbalimbali ambazo zimekuwa zikiripotiwa ndani ya nchi na nje ya nchi kuhusiana na tatizo la fedha haramu hapa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilikuwa nasoma ripoti moja ambao imeandikwa na ndugu Prince Bagenda na ilikuwa *published* mwaka 2003 katika Jarida la *Monography* ambapo anaelezea *extent* ya *money laundering* Tanzania. Ripoti imeandikwa miaka minne kabla hatujatunga sheria ile na inaonesha namna gani ambavyo watu wanafanya *money laundering* kupitia njia mbalimbali zikiwemo njia ambazo ni vigumu sana kuweza kuzigundua. Kwa mfano, imegundulika kwamba kuna watu ambao wanauza bidhaa nje ya nchi. Hapa Tanzania wana *under price invoice*s ambazo zinakwenda *TRA* kuonesha kiwango cha bidhaa ambacho kinapelekwa nje. Zinaonesha kwamba ni kidogo lakini kule nje wanapata fedha nyingi sana. Kwa maana hiyo ni kwamba, kuna watu ambao wanachukua fedha haramu, wanakuja nazo, wananunua bidhaa, wanaziuza nje lakini hapa Tanzania kiwango cha kodi ambacho kinalipwa kinakuwa ni kidogo kwa zile bidhaa ambazo zina-*export levy*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo ambalo hata baada ya kutunga sheria bado hatujaweza kulitatua. Mfano mzuri sana hivi sasa ni kwenye *export* ya bidhaa za ngozi (*hides and skins*) ambapo unakuta na nimeona taarifa hizo, kwamba bidhaa ya ngozi ambayo katika soko la dunia labda imepelekwa kama ni Pakistan (mara nyingi sana wanapeleka Pakistani) au India na kadhalika, kule unakuta imeuzwa kwa mfano, kilo moja dola 80, lakini hapa Tanzania inaoneshwa ingeuzwa kwa dola tatu (3) au nne (4) tu. Kwa hiyo, unakuta hawa wauzaji wanatorosha kwa njia hii fedha nyingi sana za kigeni nje ya Tanzania, kwa sababu mamlaka ya mapato inakuwa haipati fedha ambazo zinatakiwa. Kwa hiyo, tatizo hili ambalo limeandikwa, limefafanuliwa mwaka 2003, tumetunga Sheria mwaka 2006 lakini mpaka sasa bado linafanyika, ni kwa sababu hatujaweza kudhibiti njia kama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia nyingine ambayo inatumika na Naibu Waziri Kivuli ameieleza vizuri hapa ni kwenye *foreign exchange*. Watu wanachukua fedha, wanachukua shilingi ya Tanzania wananunua fedha za kigeni ama Dola au *Euro* au *Pounds* wanaondoka nazo. Mtakumbuka kwamba, mwaka 2011 mwezi wa Tisa, Kumi na Kumi na Moja tulikuwa na tatizo kubwa sana la shilingi yetu kuporomoka thamani. Sasa watu wengi walikuwa wanadhani kwamba hili ni tatizo la sera yetu ya uchumi au tatizo la kutouza bidhaa nyingi na za kutosha nje na kupata fedha nyingi za kigeni. Hapana! Ukiangalia miezi hiyo ndiyo miezi ambayo dhahabu ilikuwa inauzwa kwa bei kubwa zaidi, ndiyo miezi ambayo Tanzania ilipata fedha nyingi zaidi za kigeni kwa kuuza dhahabu. Lakini ndiyo miezi ambayo tulikuwa tuna-*export* kahawa na pamba ilikuwa inaondoka sasa kwenda kwenye maeneo ambayo inayopaswa kwenda. Korosho bado kwa sababu mwaka huu hatujaweza kupeleka korosho nje kwa sababu wanunuzi wa korosho wametugomea kidogo na waendelee kugoma tu, tutarekebisha mambo yetu hapa hapa na tutauza wenyewe huko nje. Ni bora waendelee kugoma ili tujenge Viwanda vya Kukoboa sisi wenyewe tuweze kuuza kwa thamani kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kilichokuwa kinatokea ni kwamba, watu ambao wanashirikiana na mabenki wanajua Benki Kuu itatoa dola kiasi gani kwenye soko. Wanachukua shilingi wanazinunua zile dola wanaondoka nazo kwa sababu Sheria pamoja na kwamba, imezuia kuondoka na viwango vya fedha nje ya nchi, au Kanuni zimezuia, lakini bado hatu-*enforce* na ni kitu ambacho tunakisema kama Kambi kwamba, unaweza ukawa na sheria nzuri sana lakini kama huitekelezi, kama hakuna *enforcement* ya Sheria hamna haja ya kuandika hiyo sheria. Mfano mzuri sana ni Sheria hii. Mwaka 2006 tumeipitisha, ilikuwa inatakiwa Waziri wa Fedha atangaze kwenye Gazeti la Serikali kiwango cha fedha ambacho mtu unaruhusiwa kutoka nacho nje ya Tanzania au mtu unaruhusiwa ku-*declare* nje ya Tanzania. Kiko kwenye Sheria ya sasa kifungu cha 23.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo *regulation* haijatoka. Tunakuja kufanyia *ammendments* sheria ambayo *regulation* kwa ajili ya kutuwezesha kudhibiti uporaji na utoroshaji wa fedha nyingi za Tanzania hatujaitekeleza. Sasa tunaaminije kwamba, leo tukimruhusu tena Waziri wa Fedha aende atoe *regulation* ya kiwango cha fedha ambacho kinapaswa kuwa *declared* katika *borders,* Waziri wa Fedha atafanya hivyo? Kwa sababu katika kipindi cha miaka sita toka mwaka 2006 mpaka sasa hajafanya hivyo na iko *provided* kwenye sheria na kifungu hicho tunakuja kukirekebisha leo. Tunarekebisha nini, kitu ambacho tumeshindwa hata kukifanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani kuna haja kwamba, badala ya kuacha iwe ni *discretion* ya Waziri kutenga kiwango cha fedha ambacho Mtanzania au mtu ambaye siyo Mtanzania atapaswa kuki-*declare* anapotoka nje ya mipaka yetu tukiweke kipengele hicho kwenye Sheria. Tusikiweke kwenye *regulation* kwa sababu kama ni suala la kwamba, fedha zitakuwa zimebadilika, Bunge hili lipo, Bunge halifi. Muda wote sisi tunaweza tukatoka, lakini Bunge litaendelea kuwepo. Kwa hiyo, tuhakikishe kwamba tunaweka *provision* ya sheria kama jinsi ambavyo imependekezwa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba, tuweke *provision* ya Sheria mtu asiruhusiwe kuondoka na fedha *cash* zaidi ya dola 10,000 nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya hivyo mtaona namna ambavyo fedha yetu itabakia kuwa ni *stable* kwa sababu watu ambao wanaiba fedha hizo kwa kutumia shilingi kununua na kusababisha *scarcity* ya dola kwenye soko watakosa namna ya kuondoka nazo, lakini muhimu ni kwamba, ni lazima tuweke *enforcement* ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni *political will*. Mwaka 2007 tumetunga sheria, mwaka 2009 kulikuwa kuna mkutano wa Mawaziri wa Fedha wa Nchi za *SADC* kule Maseru. Kulikuwa kuna ripoti kuhusu *illicity money transfer na money laundering* katika nchi zote za *SADC*, Tanzania ikiwemo. Ripoti ile ikaonesha kwamba, katika nchi za *SADC*, Tanzania na Malawi ndiyo zinaongoza kwa kuwa nchi ambazo zinapokea fedha haramu na zinatumika kuzisafisha fedha haramu kuzipeleka nje. Kwamba, mtu anaingia na fedha haramu Tanzania akanunua majengo, akanunua nyumba ndiyo maana mnaona viwanja Dar es Salaam bei ni kubwa sana, ni *artificial* price. Ndiyo maana mnaona nyumba Dar es Salaam bei ni kubwa sana, ni *artificial price* kwa sababu watu wanatoka na fedha (dola) kutoka nchi mbalimbali wanakuja kuzisafisha Tanzania.

Kwa hiyo, siku ambayo *bubble* hii ikipasuka tutaona namna ambavyo *it was very very artificial* kutokana na fedha chafu ambazo zinaingia ndani ya nchi kusafishwa na kutoka. Lakini Tanzania ilikuwa ni ya kwanza pale Maseru kupinga ripoti ile kuwa *adopted* na kikao cha Mawaziri wa Fedha wa Nchi za *SADC*, kwa sababu tu Tanzania imekuwa *painted badly*. Kwa hiyo, inaonesha dhahiri nia ya dhati ya nchi yetu, nia ya dhati ya Taifa letu kupambana na fedha haramu haipo kwa sababu hata kwenye ripoti ambazo tunapaswa tukae na wenzetu tuweze kujadili na kupitisha tunagoma. Hili limetokea Maseru miaka mitatu iliyopita mwaka 2009 Mwezi Agosti na Waziri wetu wa Fedha kama alikwenda yeye au alikwenda Naibu wake anafahamu, akapinga kwa sababu tu nchi imekuwa *painted badly*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuoneshe ile dhamira kwamba, tunataka nchi yetu iwe safi. Tunataka tuzuie fedha zinazotokana na rushwa, ufisadi, uuzaji holela wa madini yetu na vilevile tuweze kuzidhibiti fedha ambazo zinatoka nje. Nadhani Serikali inafahamu kwamba, mwaka jana mwezi wa pili, Polisi walimkamata mfanyabiashara ambaye alikuwa ameiba benki zaidi ya shilingi milioni 500 akawa amezinunulia vocha za simu. Alikwenda sijui *Shivacom*, akaenda kwa hawa *super dealers* wa kampuni za simu, akanunua vocha za thamani ya shilingi milioni 500 kwa sababu alikuwa ameziiba kwa lengo la kuzisafisha na ndiyo utamaduni ambao unafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, unachofanya unaiba, wenyewe wanaita kupiga 'unapiga benki' unapata fedha ama utakwenda kuziingiza kwenye *real estate* na kama tulivyoeleza kwenye hotuba yetu hatuna *real estate regulator* au utakwenda kuziingiza kama hivyo huyo mfanyabiashara alivyofanya mwaka jana mwezi wa Pili na Polisi wanayo taarifa. Sijui kesi yake imefika wapi, akaenda kununua vocha za simu na kwenda kuzisambaza nchini. Kwa hiyo, unaponunua vocha, wewe unajua unanunua kutoka kwa muuza vocha, kumbe unamtajirisha mtu ambaye amefanya wizi katika mfumo wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu likubaliane na mapendekezo yetu ambayo tumeyatoa. Mapendekezo ya kwanza kuhakikisha kwamba kunakuwa na *enforcement* ya uhakika. Bila kuwa na *enforcement* sheria hii itabakia kama jinsi ilivyo. Bila kuwa na *enforcement* nchi yetu itaendelea kutumika kama eneo la kupitisha dawa za kulevya, kama eneo ambalo watu watakuja kuchukua madini yetu na kuyanunua kusafisha fedha zao chafu na kuziondoa, kama eneo la *tax evasion* kwa sababu *tax evasion* pia inatumika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia inatumika kama eneo la *capital flight*, wawekezaji wanaokuja kuwekeza nchini wanatorosha fedha nyingi sana kupitia *profits*, kwa kutumia *mispricing*, kupitia kutudanganya kwenye *invoices* mbalimbali. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iwe makini sana kuhakikisha kwamba, kitengo hiki ambacho leo tunataka tukiimarishe kinaimarishwa zaidi, kinakuwa *independent*. Hata ile kusema tu kwamba, ni *operationl independence*, hapana kiimarishwe zaidi. Kama tunampa *security of tenure* huyu *CEO* wa hiki kitengo na kwamba, Rais asiweze kumfukuza kazi, tunamlinda ili aweze kufanya kazi yake kwa uhuru zaidi, ni vizuri basi kukifanya kitengo chake kiweze kuwa kikubwa zaidi, kiweze kuwa na *powers* zaidi ya kuweza kudhibiti aina yoyote ya fedha ambazo zinatoroshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi za *Sub-Saharan Africa* zina tatizo kubwa sana la fedha nyingi sana kutoka. Tanzania peke yake kati ya mwaka 2000 na mwaka 2010 ndani ya miaka 10 jumla ya dola bilioni 2.9 zimetoroshwa nje ya nchi kwa njia mbalimbali, kama ni kwa *through export*, *burea de changes, corruption* na kadhalika. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunapaswa kuona namna gani tutakavyoweza kuyadhibiti ili kuifanya nchi yetu iweze kuwa safi, tuweze kuwafanya Watanzania wafaidike na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, kwa mchango wako na tutaendelea jioni na Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Leticia Nyerere na wengine wale sita kama nilivyoeleza, wote mtapata nafasi.

Sasa Waheshimiwa Wabunge nifafanue tu hapa kwamba kufuatia yale maagizo ya suala letu lile la mgogoro wa Madaktari na Serikali kwa Kamati, nifafanue tu kwa faida ya wananchi na Bunge letu kwamba, kwa kawaida ya Mabunge karibu mengi ya Jumuiya ya Madola, kwa kweli kauli za Mawaziri huwa hazizui mjadala wa moja kwa moja ndani ya Bunge. Huo ndiyo utaratibu na sababu yake ni kwamba, tunaweza kujikuta tunakuwa na kauli tofauti tofauti kuhusiana na jambo ambalo si la kutofautiana sana.

Sasa nielekeze kwamba, Waheshimiwa Wabunge yeyote mwenye nia ya kushiriki kule kwenye Kamati ile anaruhusiwa kushiriki, kusikiliza, kuchangia na kadhalika. Kamati ile ikiishasikiliza pande zote mbili, (upande wa Serikali na upande wa Daktari), itatolewa taarifa hapa Bungeni juu ya yaliyojiri na ushauri kwa Bunge kutoka kwa pande zote mbili. Kwa hiyo, mwisho wa siku sisi tutakuwa na ushauri kwa pande zote mbili na *not necessarily* maagizo, ili kama Mbunge atataka mjadala baada ya hapo, basi anaweza kuleta hoja mahususi.

Hapa mwisho, niwaombe sana Waheshimiwa Madaktari kama ambavyo viongozi wetu wamefanya na kwa niaba yenu Waheshimiwa Wabunge niwaombe Madaktari wote nchi nzima warudi kazini. Natoa wito Madaktari wetu tunawapenda sana warudi kazini, wazingatie viapo vyao. Pili, nawaomba sana Madaktari na Serikali watoe ushirikiano kwa Kamati yetu ya Huduma za Jamii. Ahsante sana. (*Makofi*)

Baada ya maelezo hayo kwa kuwa muda sasa hauruhusu kuendelea na shughuli nyingine yoyote, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa kumi na moja jioni ya leo.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Sylvester M. Mabumba) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Felix Mkosamali na baadaye Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kuleta Muswada huu na pia kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuzungumza kwa mwaka huu. Naomba niwape wote kheri ya mwaka mpya pamoja na wananchi wote wa Jimbo la Babati Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika Muswada huu. Kwanza kabisa, naomba elimu zaidi itolewe kwa wananchi wote ili waielewe sheria hii vizuri kwa sababu Watanzania wengi bado hawajaelewa vizuri suala la fedha ambayo ni haramu, pesa ambayo haipitii kwenye mkondo kwa sheria ambayo siyo halali. Fedha zote ambazo zinapita nje ya mkondo halali, yaani nje ya mkondo wa kibenki au maduka ya fedha halali, pia inahesabika kuwa ni fedha haramu ambayo Serikali haijui huwa inapaswa ipite ili Serikali iendelee kupata mapato yake. Kwa sasa hivi asilimia kubwa ya fedha hizo zinapita njia hizo za panya ambayo ni fedha haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kuwa na fedha hizo ni kwamba hakuna mabenki maeneo mengi ya huko vijijini. Labda kuna mtu ambaye anataka ku-*transfer* fedha zake kutoka sehemu moja kwenda nyingine, unakuta huduma za kibenki hakuna. Sasa inabidi atumie watu binafsi ambao anaweza kupeleka hizo fedha, anatoa hapa anapewa huko maeneo ambapo hakuna hizo huduma.

Kwa sasa hivi tunashukuru kwamba hizi Kampuni za Simu kwa mfano *Voda-Pesa, Zain, Tigo* zinafanya hiyo kazi, lakini pia lazima tuwe waangalifu kwamba: Je, hizo Serikali ina namna yoyote ya kuangalia ni fedha kiasi gani inatumwa huko na inapitia huko na ni mapato kiasi gani ambayo Serikali inaweza kupata kutoka huko na inaweza kuwa ni njia moja, yaani kutuma fedha hizo haramu na watu wakawa wanaendelea kupata kwa sehemu mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali iangalie upya na ikae na hizi Taasisi za fedha, hizo gharama wanazotoza ni kubwa sana. Kwa mfano, Sh. 100?= wanatoza asilimia tatu. Sasa hizo gharama ni kubwa. Hiyo ni ya kutuma tu na ndio maana watu wanashawishika kutumia njia mbadala, wanatuma kwa kupitia njia binafsi ambayo inakuwa siyo kwenye mkondo rasmi.

Pia hata katika hizi Kampuni za Simu bado gharama zao ni kubwa ingawa wamesaidia sana huko vijijini, lakini bado hizi gharama ni kubwa mno. Lakini pia tuangalie kwa mfano mtu labda ana fedha zake za kigeni ukiweka katika benki yoyote ya kwetu, ukitaka kutoa fedha yako ambayo wewe umeiweka pale, saa ya kutoa wanakutoza asilimia moja *withdraw fee,* mbali na zile tozo nyingine. Hiyo pia inasababisha watu wengi wasipite kwenye mkondo wa benki na wanaamua kupitisha hizo fedha kwa njia ya watu binafsi. Lakini pia ku-*transfer* fedha, labda hawa watu wanao-*import* wakitaka ku-*transfer* fedha, unakuta kwa kupitia benki gharama ni kubwa na ndiyo maana wanapitia kwa watu binafsi, na ndio inachangia sasa hizi fedha ziweze kupita nje ya mkondo halali wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Serikali iangalie upya haya maduka yetu ambayo yanafanya biashara ya fedha za kigeni (*Bureau de change*). Ni asilimia kubwa unakuta zinafanya biashara, ni sawa na mtu anauza nguo au karanga au pipi hapo kwa sababu hakuna udhibiti wa aina yoyote. Leo hii ukiangalia bei ya Dola haiko *stable*. *Currency* yetu haibaki kuwa *stable* kwa sababu mtu anaweza kutoka Kenya ana fedha zake haramu za kutosha, anatoka Nairobi asubuhi, anakuja Arusha anabadilisha fedha zake na kurudi tena Nairobi siku hiyo hiyo, na unakuta fedha za kigeni hapa kwetu zinaendelea kuwa haba. Ndiyo maana bei ya Dola inaendelea kupanda, unakuta fedha zetu nyingi zinaendelea kwenda nje ya nchi ambapo zingekuwa hapa na fedha yetu ya Tanzania ingekuwa ni *stable*. Kwa hiyo, hata haya maduka ya fedha za kigeni, Serikali ingeangalia namna ya kuzidhibiti vizuri na *transaction* zao ziwe *monitored* kila wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tuwe waangalifu. Sasa hivi tumeambiwa kwamba Waziri atakuwa na mamlaka na atatoa kiwango maalum cha chini ambapo ukiwa na fedha kiasi fulani utaruhusiwa kwenda na *cash* zaidi ya hapo. Kwa mfano, kama ni Dola 10,000: Je, Mtanzania ambaye anakwenda nje anahitaji fedha kwenda kutibiwa au anakwenda kwa safari yoyote ile? Hivi asiporuhusiwa kuwa na hizo fedha, akitakiwa kuwa na fedha zaidi ya hapo, ninaomba ule urasimu usije ukarudi tena, ikaanzisha tena mianya ya rushwa ambayo tunaendelea kuwaongezea masuala ya rushwa. Lakini tunaposema hiyo Dola 10,000 anakwenda nayo, mahitaji yake ni zaidi. Leo hii *travellers cheques* kutoka Tanzania hazikubaliki katika sehemu nyingi zilizoko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiangalia *Master Card, Visa Card* hizi zote ni gharama. Tozo zake ni asilimia tatu mpaka saba. Sasa kwa nini Mtanzania aumie wakati anakwenda labda kutibiwa au anakwenda masomoni? Kwa nini atumie gharama kubwa ya asilimia tatu mpaka saba kwa gharama hiyo wakati angeweza kuidhinishiwa tu kwa njia ya urahisi kama ni kitu halali? Serikali iwe na mpango mwingine kwamba mtu ambaye ni *genuine case* apate basi kibali bila urasimu wowote, bila ya kuleta mianya ya rushwa aweze kurahisishiwa aweze kwenda na hizo fedha. Lakini kwa yule ambaye hatakuwa na sababu yoyote, wale ambao wanaondoka na Dola laki moja, laki mbili bila sababu yoyote, hao basi wazuiwe. Lakini kwa wale ambao wana sababu maalum, pia tuwe waangalifu katika suala hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali wakishapitisha hii sheria ni muhimu sana tuendelee kutoa elimu kwa sehemu mbalimbali. Viwango vya kodi ambavyo tunatoza kwa upande wa Serikali kwa mfano kwenye mambo ya *importation* na mambo mengine, Serikali iangalie upya. Mimi naamini kwamba bei zetu za baadhi ya kodi zingepunguzwa, *compliance* ingekuwa ni kubwa, watu wasingekuwa na sababu ya kupitisha katika njia za panya au tunasema hizi fedha kwa njia za haramu wangekuwa wanapitisha kwenye mkondo wa kawaida, mkondo wa kibenki na Serikali ingepata kodi yake labda mara mbili au tatu ya hiyo ya fedha yote, tungejua kwamba ni halali, haitumiki katika mambo ya ugaidi au mambo yoyote, lakini ingekuwa inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha nyingi kutoka nje zinaletwa Tanzania, zinasafirishwa fedha haramu kuwa fedha halali kama walivyotaja mwanzoni kwamba *Tanzanite* ilianguka bei kwa sehemu kubwa kwa sababu waliunganisha na ugaidi. Lakini hizo hizo fedha zinaletwa zinanunua dhahabu huku kwetu, zinanunua madini mbalimbali ya vito, inanunua mazao na hiyo fedha baadaye inakuwa *under declared*. Kwa sababu wakati wa kusafirisha, yule *custom officer* ambaye yuko pale ni mtu mmoja tu ambaye anawajibika pale, vitu vyenye thamani labda ya Dola laki tano hata akiandika au Dola 10,000 hakuna namna ya kudhibiti, unakuta fedha zile zinarudi kule ni mali halali iliyotoka Tanzania, imekuwa fedha hiyo imesafishwa na ni njia moja ya kugeuza fedha zile haramu kuwa halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia nchi nyingi hapa Afrika viongozi wetu wengi walituma fedha nyingi sana huko nje, ziko katika mabenki kipindi hicho. Nchi hizi za Ulaya zinapokea hizo fedha tena kwa mikono miwili, wanazifurahia kwa sababu zinakwenda kuwekeza kule kwao. Lakini pindi wanapowachoka hao viongozi unakuta zile fedha zinabanwa na sisi tunaendelea kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitakiwa tuwe na mikataba ya Kimataifa ambapo zile fedha zote za nchi zinazoendelea zirudishwe katika nchi zao zije zifanye kazi ya maendeleo. Lakini pia suala hili ni pana sana. Tusifikirie suala la hii fedha haramu ni ndogo, hata hii fedha ambayo inatoka kwa sehemu moja kwenda nyingine hapa nchini, Shilingi milioni 10, au 20 bado ile haiko kwenye mkondo rasmi. Serikali inakosa kodi. Hivyo iangaliwe upya. Serikali iangalie dhana nzima ya kodi ili watu waweze kuingia katika biashara halali ambapo kila mmoja atakuwa anaona ni sahihi kulipa kodi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, hata katika *importation* ya magari, leo hii watu wana-*under declare* kwa sababu ukishaleta pale bandarini unakuwa *customs,* wanapandisha kitu hata kama ni halali ya Dola 2,000 watakupandishia inakuwa Dola 5,000 wanai-*up lift* bila sababu yoyote na ndiyo maana watu wanaingia katika mtandao wa kupitisha fedha usio halali. Serikali ingeangalia *compliance* iwe kubwa, iteremshe kodi.

Hata ukiangalia kwenye haya majengo yote ambayo yapo, wageni wanakuja hapa, Mtanzania umesota, umehangaika, wewe una biashara yako ya miaka mingi, huwezi kununua gari mpya. Lakini unashangaa watu wanajenga maghorofa 10, 15 kwa muda mfupi. Haya yote tunayosema Taasisi

ambayo inatakiwa kuangalia *Financial Intelligence Unit* ifanye kazi yake vizuri. Ningeomba Watanzania wapewe elimu, sisi wenyewe ambao tunaweza kusema kwamba tuanze kuhoji na tusaidiwe. Mimi naamini kwamba ni suala zuri sana. *Money laundering* ikidhibitiwa Serikali itapata kodi kwa sehemu kubwa, lakini pia gharama nyingi zitapungua. Bei za vitu vyetu vitapungua na fedha ya Tanzania itakuwa ni *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nishukuru. Naomba wote tuchangie, lakini muhimu kuliko yote isije ikaishia kama ilivyokuwa mara ya kwanza mwaka 2006, mpaka leo hii hakuna kilichotekelezwa. Safari hii tukipitisha ianze kufanya kazi mara moja, kanuni zitungwe na Tanzania iendelee kupata maendeleo. Ahsanteni. Mungu ibariki Tanzania, Mungu ibariki Afrika. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Jitu Soni. Sasa namwita Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa Dkt. William Mgimwa ajiandae.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu sana ambao umeshaonyesha namna gani fedha zetu zimeshaliwa huko nyuma kwa mianya ya sheria. Tumesikia hotuba nzuri ya Kambi ya Upinzani imeeleza namna gani watu walikuwa wanahamisha fedha *(BoT)* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusikitika sana kwa sababu Muswada kama huu hatukupashwa kupewa kwa haraka kiasi hiki. Huu ni Muswada muhimu kweli kweli. Ni Muswada ambao unasomwa pamoja na Muswada wa Kuhujumu Uchumi *(Economic and Organise Crimes Act.)* Huu ni Muswada ambao ukipita haraka haraka, matokeo yake yatakuja makubwa sana na nitaeleza baadhi ya vifungu ambavyo nimeviona kabisa kwamba kama tukipitisha Muswada huu na vifungu hivi vikapita tu hivi hivi, tutakuwa tunatengeneza mianya ya watu kujipatia fedha ambazo siyo halali.

Mojawapo ni kifungu ambacho kinatoa adhabu. Kama mtu akikamatwa na *money laundering* alipe kati ya Shilingi milioni 100 au 500. Sasa mtu amefanya *money laundering* ya Shilingi trilioni mbili, akinipa Shilingi milioni 500, hiyo adhabu inasaidia nini? Ni adhabu ambayo haitoshi wala haitatui tatizo hili lililoko mbele yetu. Biashara hii ya *money laundering* inafanywa na watu ambao wana fedha nyingi! Shilingi milioni 500 siyo fedha kwao! Mabilioni yaliyokuwa yanaibwa *BoT* na maeneo mengine ni watu ambao Shilingi milioni 500 wanazilipa kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningeomba kabisa kwamba kama hatutengenezi mfumo mzuri wa kutoa adhabu kwa sheria hii tukapitisha kama ilivyo, maana yake tunatoa mianya ya watu kutafuna fedha wakijua kwamba wakienda Mahakamani watatozwa Shilingi milioni 500 na kushuka chini au kufungwa miaka mitatu. Miaka mitatu ni sawa na kukaa mwaka mmoja na nusu gerezani. Kwa hiyo, tutapitisha bomu hapa, tutapitisha tatizo. Sheria hii inapaswa kuwa na *punitive punishment,* adhabu ambayo ni kali, siyo adhabu ya kumfunga mtu mwaka mmoja na nusu wakati ameiba Shilingi trilioni 10. Mimi sitaunga mkono hoja mpaka hicho kifungu kifanyiwe marekebisho kwa sababu ni *loop hole* ambayo itafanya watu waendelee kupata fedha zisizo halali kwa kutoogopa faini inayoweza kutozwa na Mahakama. Hilo ni eneo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ukisoma kifungu cha 28(c) cha hii inayofanyiwa marekebisho kinasema kwamba *foreigner,* mtu ambaye sio Mtanzania, ili aweze kushtakiwa kama amefanya *money laundering* lazima *DPP* a-*consent*. Asipo-*consent,* huyo mtu hatashtakiwa. Ndio kifungu kinavyoeleza na ndiyo maana nimeleta *schedule of amendment* na nitawaomba Wabunge waniunge mkono kwa sababu hii itakuwa kama kifungu cha 90 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. *DPP* akiamua anasema siwezi kuendelea, na hii kesi na hatoi sababu kwa sheria zetu za Tanzania.

Sasa tukisema hapa kwamba ili mtu ashtakiwe, lazima *DPP* akubali, ajiridhishe, yaani tumpe *discreation DPP,* yeye ndio aamue kwamba huyu mtu amefanya *money laundering.* Sasa tumpe yeye ndio akijisikia ashtakiwe au asishtakiwe. Nakwambia haya Makampuni ambayo yanawekeza nchi hii hayatashtakiwa! Makampuni yenye fedha, yatafanya *money laundering,* yatawashawishi watu kwa fedha kidogo sana na hao hawatashtakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sheria hii naomba tuiangalie kwa makini sana. Hii ni sheria ya msingi sana, ni sheria ambayo tunapaswa kuipanua zaidi ya marekebisho haya. Leo watu wanaweka fedha za wanafunzi kwenye *fixed account* wanazichelewesha zaidi ya miezi mitatu, hiyo ni *money laundering* kwa sababu unanufaika na fedha ambayo siyo ya kwako.

Hivyo, vifungu vimo kwenye sheria hii, tunapaswa kufanya marekebisho makubwa. Watu wanajipatia fedha haramu, leo hatuwatozi watu kodi kwenye minara ya simu, watu wanafanya *transaction* zao huko, hivi hao mnaong'ang'ania kwamba mnawatoza kodi ya jumla kwenye minara ya simu, hizi huduma sijui za M-Pesa, Tigo Pesa na nini hamwatozi kodi, wao hawapati faida kwenye hizo biashara? Hii sheria tunapaswa kuiangalia kwa mapana sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna fedha nyingi kwenye mitando ya simu, hatuwatozi kodi na wala hayaonekani kama hayo ni makosa. Lakini sasa hivi mpaka watu hawaweki fedha kwenye mabenki. Wanaweka kwenye *M-Mpesa* na watozwi kodi! Wanaweka kwenye *Tigo Pesa* na hatuwatozi kodi. Je, hawa watu hawapati faida? Hiyo siyo *money laundering*? Kwa hiyo, Sheria hii tusiipitishe kwa haraka.

Waheshimiwa Wabunge, haya ninayo yazungumza, mimi nimeyafanyia utafiti. Msidhani nazungumza tu! Haya mambo ni mazito. Sheria hii ikipita, tutakuwa tumekwisha ndugu zangu! Kwa hiyo, nimeleta *schedule of amendment*, vifungu hivi ninavyovieleza ni vya msingi kweli kweli!

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tumekuwa tunaona ubora wa fedha ambazo tumekuwa tunazitengeneza. Fedha zetu ni fedha ambazo hazina viwango. Fedha ambayo kwanza mimi mpaka sasa hivi nimekuwa nashangaa. Ni nchi moja yenye noti mbili zinazotumika kwa wakati mmoja. Kuna noti ya Shilingi 10,000 ya zamani na kuna noti ya Sh. 10,000 ya sasa hivi, zote zinatumika. Sasa hao watu waliokwenda kuchapisha hizi fedha huko halafu tunaendelea kutumia noti za zamani, sio kujipatia pesa kwa namna nyingine? Sio pesa haramu hiyo? Hiyo ni *money laundering*. Kwa hiyo, Sheria hii ni ya msingi sana. Ina vifungu ambavyo vimeletwa kwa ajili ya kuwakwepesha watu wasishitakiwe na hili nalilisitiza, watu hawatashtakiwa. Mtu ameiba pesa zake BoT atakuwa haibi yeye anashirikiana na Benki ya Kigeni halafu *DPP* ha-*consent* mashtaka. Sheria ndivyo inavyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ni mambo tunapaswa kuyaangalia, ni mambo ambayo yanaweza yakaongeza uhujumu uchumi, yanaweza yakaongeza ufisadi kwenye nchi na yanaweza yakatusababishia matatizo makubwa sana baadaye kama tutaacha tu yakae hivi hivi. Ukisoma katika Sheria hii, Kamati ile inavyoundwa, Rais anateua Kamati. Kwanza, Kamishna anateuliwa na Rais. Ukisoma kifungu cha (5), Anachaguliwa tu, Kamishna ambaye ana-*deal* na mambo makubwa ya namna hii ya watu ambao wameiba pesa za Serikali hatutakiwi kumwachia Rais peke yake. Jambo hili linapaswa Bunge li-*approve* mtu huyu. Lakini pia ukiangalia, licha ya Rais kumteua kama Kamishna, yule akiwa na makosa ni Rais huyo huyo ndiye ambaye anaunda Tume ambayo inamchunguza huyu Kamishna. Lakini ile Tume wameandika kwamba kutakuwa na *Senior Police Officer.* Ni wa ngazi ipi? Ni wa *level* ipi? Kuna Mwakilishi wa Benki Kuu na wengine.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru, muda wako umekwisha.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mengine nitaeleza kwenye *schedule of amendment.* Nashukuru sana.

**MHE. DKT. WILLIAM A. MGIMWA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie. Awali ya yote, naomba ku-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Kamati iliyofanyia kazi Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufinyu wa muda nina mambo manne nitayasema. Lakini awali ya yote nachikua nafasi hii kumshukuru kabisa Mheshimiwa Waziri kwa kulifanyia kazi suala hili na kulileta mapema. Baada ya kusema hiyo, naomba nianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni *regulations*. Kamati yetu ilitoa ushauri kwamba Sheria hii ya *Anti-Money Laundering* tumekuwa nayo tangu mwaka 2006. Kwa bahati mbaya Wizara ilichelewa kutengeneza Kanuni, yaani *regulations* na tukaomba Wizara, basi kwa sasa ihakikishe kwamba *regulation*

zinakuwa tayari mara tu baada ya Sheria hii itakapokuwa tayari ili utekelezaji wa Sheria hii uwe mwepesi na wa ufanisi kwa kuwepo *regulations*. Tunashukuru Mheshimiwa Waziri alituunga mkono na amelichukulia hili *seriously*.

Lakini la pili niende sasa kwenye Sheria yenyewe iliyopo. Tumekubaliana na mabadiliko yaliyowasilishwa katika Kamati kwa sababu nyingi, lakini zipo sababu kubwa ambazo tumeona ni muhimu. La kwanza, Sheria hii inampa mamlaka makubwa na mpenyo wa ufanisi Kamishna wa *FIU* ukilinganisha na ilivyokuwa zamani. Sheria inapompa mtekelezaji nafasi ya kutekeleza kiufanisi zaidi, Sheria inakuwa nzuri kwa sababu tunataka Sheria inayotekelezeka kiufanisi na kwa manufaa, na sababu iliyowekwa na Sheria hii tulivyoitizama kwa undani, mabadiliko haya tumeona yanakidhi mahitaji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, lilikuwa suala la umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu za watoa taarifa. Hii iko chini ya Ibara ya (6) ya Sheria iliyopo. Sheria iliyopo haifafanui kinagaubaga ni taarifa zipi zitunzwe na kwa kiwango gani zitunzwe. Kwa hiyo, inampa mwanya mtoa taarifa kutokuwa na kumbukumbu sahihi pale atakapohitajika kuthibitisha yale aliyoyasema. Kwa upungufu huo, badiliko la Sheria chini ya ibara hii linafafanua ni mambo gani anatakiwa mtoa taarifa ayawekee kumbukumbu, na Sheria inamtaka aweke kwa muda gani. Kwa hiyo, hii inakuwa ni *record* ambayo itakuwa na manufaa kwa *reference* baada ya muda.

Kwa hiyo, sisi kama Kamati, tukaona uzito huo ni wa muhimu kwa ajili ya kuifanya Sheria iwe na nguvu. Lakini la tatu, ni suala la uwezo kisheria wa watoa taarifa kubadilishana taarifa za msingi juu ya fedha za mashaka, yaani fedha zenye mashaka ya uharamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa vyombo vya fedha havina nafasi ya kuwa na Sheria yenye uwazi ya kuvilinda vyombo vya fedha mpaka kubabaisha kwenye Sheria nyinginezo ambazo hazimo ndani ya *Anti-money Laundering*. Kwa hiyo, sheria ilikuwa ina *gap* ya kutoa kinga kwa vyombo vya fedha kutoa taarifa kwa chombo kingine juu ya mashaka yanayohusu fedha ambazo zimeingizwa ndani ya chombo cha fedha.

Sasa ibara hii ya 21, kwa maana ya *financial institutions* inavipa vyombo vya fedha kinga na uwezo wa kuwasiliana na vyombo vingine ambavyo vimeleta pesa. Mathalan mimi nikiwa katika Benki 'A' na mteja fulani, nikaletewa fedha labda Shilingi milioni 100 kuziweka katika akaunti yake na mimi nikawa na shaka juu ya uwezo wa yeye kuwa na kiwango cha namna hiyo. Dakika hii sina mamlaka ya moja kwa moja ya kuiuliza Benki huko hela ilikotumwa, inakotoka.

Kwa hiyo, Sheria hii itanipa nafasi *instantly* mimi kuuliza Benki ambayo imetumiwa kuniletea hizo fedha kwa ajili ya mteja wangu bila kutafuta Sheria nyingine za kunikinga. Kwa hiyo, sheria hii itanipa nafasi moja kwa moja kufanya kazi kiurahisi na kwa *speed*. Kwa hiyo, ina *add value* kwenye utendaji ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namna ya kutunza fedha za mashaka. *FIU* wakati wanafanya kazi, Sheria ilikuwa mpaka dakika hii haifafanui. Fedha zile walizo na mashaka nazo ambazo zinakamatwa au zinazuiwa dakika ile waziweke wapi? Unajua kuna vyombo vya *lawfully enforcement agencies* ambapo unaweza ukaambiwa kithibiti kimepotea kwa sababu tu Sheria haiko wazi kwamba watakapokamata kile kithibiti kilichopo, kitunzweje? Kiwekwe wapi kwa mujibu wa Sheria iliyo wazi? Sasa hapa tunazungumza mapesa mengi, mabilioni yatakuwa pengine yametiliwa shaka. Sasa *FIU* anapapata nafasi kisheria ya kuzuia au kukamata zile fedha, lazima Sheria iseme akishafanya hivyo, fedha hizo aziweke wapi.

Sasa Sheria hii imefafanua kwamba *immediately FIU* kutumia Sheria hii kukamata au kuzuia fedha hizo, basi azifungulie akaunti kwenye Benki ambayo itakuwa inaaminika na kuziweka fedha hizo kwa usalama wa jambo lenyewe. Kwa maana hiyo, zisiwekwe tu kwa mujibu wa mawazo ya Kamishna. Iwekwe kisheria kwa usalama wa kidhibiti na kwa usalama wa usahihi wa mwenye pesa ikiwa itathibitika siyo fedha haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Kamati, tumetizama mambo haya na tukayaona ni ya msingi na yanafaa kuungwa mkono na tukamwunga mkono Mheshimiwa Waziri kwamba haya yanafaa.

Jambo lingine la msingi, la tano, ni juu ya Sheria kuwa na kipengele kitakachosaidia kuwabana wale wafanyakazi *Financial Intelligence Unit (FIU),* wakati wakiwa wanafanya kazi na wakati watakapokuwa wameondoka kufanyia kazi kitengo hicho. Kuna msingi mmoja mkubwa wa kuiunga mkono ibara hiyo. Ni kwamba inawezekana kwa upungufu wa ubinadamu, mmoja wa wafanyakazi kwa bahati mbaya au kwa kudhamiria aka-*disclose* taarifa hizi, na kwa kuwa itakuwa Sheria haimbani, basi kutakuwa na athari ya kazi yenyewe kwa watu mbalimbali.

Kwa hiyo, kipengele hiki cha kumzuia mfanyakazi anapokuwa akiifanyia Taasisi hiyo au *immediately* atakapokuwa ameondoka kumzuia uwezo wa kutangaza na kusema alichokikamata na alichokiona, basi inafanya usiri na usalama wa kazi yenyewe. Sisi tuliunga mkono tukaona inasaidia Sheria na wahusika wote watakaokuwa wanashughulikiwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo na mambo mengine tuliyoyatazama kwa ujumla jumla, haya niliyoyasema kwa haraka haraka ni mambo makubwa ambayo yamekuja na kubadilisha vipengele mbalimbali vinavyoongeza nguvu ya utekelezaji wa sheria, nguvu ya kufanya kazi ile iwe imara na yenye usalama zaidi kwa manufaa ya walengwa wote na kwa manufaa ya sababu iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sina sababu ya kuendelea kusema mengine, haya naona ni ya msingi ambayo nimeona niyajadili na niyawasilishe na nimuunge mkono Mheshimiwa Waziri kwa Muswada huu. *(Makofi)*

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia kwenye Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu. Ni kweli Sheria ilikuwepo tangu mwaka 2002, lakini cha kushangaza au mimi mwenyewe binafsi ninashangaa wahusika wamewezaje ku-*enforce* hii Sheria ambayo haina hata viwango, haina *limit* ya kusema kwamba mtu haruhusiwi kutoka nje ya nchi na pesa kiasi fulani wala haizungumzii kiasi gani cha pesa mtu anaruhusiwa kuingiza nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuzungumzia suala la *reporters,* watu wanaotoa taarifa wakiwemo *financial institutions* kama ilivyobainishwa na Mheshimiwa Waziri wakati alipokuwa anatoa taarifa yake. Benki hutegemea wateja ili iweze kufanya biashara. Kama tunavyofahamu, Benki hufurahia zaidi wafanyabiashara au wateja ambao wana pesa nyingi.

Sasa unapomwambia huyu *Banker* kwamba ashirikiane na *Financial Intelligence Unit* kutoa taarifa kuhusu mteja wake, hapo mimi sielewi ni kitu gani kitafanyika, ama wateja watamkimbia huyo *Banker* ama yeye mwenyewe pia atakuwa amejiingiza katika kukiuka Sheria za kibenki ambazo zinamtaka alinde na kutunza siri za wateja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuiangalia kwa makini Sheria hii, nimegundua kwamba itakuwa *enforced* kwa kushirikisha Sheria nyingine zikiwemo Sheria za Kuzuia na Kupambana na Rushwa. Ingekuwa ni vyema basi wahusika wabainishe ni aina gani za rushwa ambazo zitahusishwa na Sheria hii ya Fedha Haramu ukizingatia kwamba tuna aina nyingi za *corruption* ikiwemo *bribery* ambayo ni hongo ya kawaida, ikiwemo *fraud* ambayo ni udanganyifu kwa ajili ya kujipatia kitu fulani, ikiwemo *imbursement* ni kuhamisha mali kutoka mahali pake na kupeleka sehemu ambayo mtu anataka, ikiwemo pia na *nepotism* ambayo inabeba pia rushwa ya ngono.

Kwa hiyo, ni jambo la muhimu sana vyombo husika vitoe elimu ambayo inastahili na vitoe maelezo ya kina kwamba haya makosa ambayo yapo kwenye Sheria za *Corruption* ni yapi yatahusishwa kwenye Sheria ya Fedha Haramu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kipengele ambacho mimi kwa mtazamo wangu naona kina utata. Kuna fedha safi ambayo inaweza ikafadhili matendo machafu. Sasa hiyo fedha ambayo labda imepatikana kihalali kabisa, mfanyabiashara ana kiwanda, ana pesa nyingi tu, lakini akafadhili vitendo vya kigaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui hili litawekwa vipi ili tuweze kwenda sawa katika sheria hii! Natambua wahusika hasa *Financial Intelligence Unit* wanajua taratibu za kufanya *investigation* kwenye *financial crimes*. Lakini nilikuwa nataka nitoe angalizo. Pamoja na kwamba kuna *methods* (njia)

zinazotumika kufanya *investigation* katika *crimes* zote ambazo zinahusika na mambo ya fedha, ni lazima tukumbuke kwamba tunapofanya *investigation* kwa nchi kama Tanzania, nchi ambayo inaendelea, hatuwezi kutumia *methods* ambazo zinatumika nchi kama ya Marekani. Pamoja na kwamba hizo *methods* zipo, zimekwa, siwezi kuzitaja kwa manufaa ya wanaofanya hii kazi, lakini ni jambo la kuzingatia kwamba itabidi wafikie wakati wa kubadilisha hizo *methods* wakati wa kufanya *investigations* Tanzania, wanapofanya upelelezi kuhusu makosa yanayohusishwa na fedha haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira yetu ni tofauti kabisa na ya Ulaya au Amerika, lakini kwa bahati mbaya Watendaji wetu wamekuwa wakitumia ama tafiti zilizofanyika Marekani ama *methods* za uchunguzi au za upelelezi zilizotungwa kuzingatia nchi zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba walizingatie hilo kwa sababu nimegundua kwamba sisi Watanzania tunapenda sana makabrasha na ni mafundi sana wa kutumia na ku-*refer* kwenye *theories* za wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwanza kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia katika Sheria hii ya Kudhibiti fedha Haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu nafikiri umekuja mahali pale kwa sababu mimi katika maisha yangu nakumbuka siku za nyuma kidogo wakati sheria hii haifanyi kazi, ukiwa unatoka nje au unaingia ilikuwa ni lazima una-*declare* kile ulichonacho, hasa pesa. Mimi nakumbuka mwaka 1989 natoka Ujerumani, pale *Airport* nilikuwa naambiwa kwamba lazima una-*declare* ni kiasi gani cha pesa unazo? Lakini unapotoka pia unaeleza. Nchi zote ndivyo hivyo hivyo wanavyofanya. Kwa hiyo, kuletwa kwa sheria hii, mimi naishukuru Wizara na Waziri pamoja na watumishi wengine wa Wizara hiyo kuleta Muswada huu ambao kwa kweli umekuja mahali pake kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu kabisa kwamba kwa wakati huu, Muswada kama huu ufanye kazi yake. Lakini kitu ambacho kidogo nilikuwa na mashaka nacho ni udhibiti wake. Utakuwaje? Kwa mfano, ni namna gani kwa kweli Kamishna au *system* hii inaweza kufanya kazi? Kwa sababu nchi hii ni kubwa na kila mahali kumekuwa na wajanja ambao wanajaribu kuingiza pesa kwa namna ambavyo wao wanajua, hasa kwangu ambaye natoka mipakani au Mikoa ya Mipakani, kumekuwa na shida kubwa sana ya pesa haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kwamba tunaongelea pesa haramu kwa ukubwa wake, lakini kama tulivyosikia mara ya kwanza kwamba huko Mbeya kulitokea watu ambao wana mashine ambazo walikuwa wanachapishia hela na zinaingia katika mfumo na hii ilikuwa ni mbaya sana. Unajaribu kuangalia kwamba: Je, vyombo hivi vinashughulika na nini? Kuna *PCCB*, kuna kila aina ya *system* ambayo ipo inashughulikia kuangalia usalama wa pesa zetu. Kwa hiyo, imekuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka kwa miaka michache iliyopita, wakati mwingine nilikuwa najaribu kwenda kuomba hela katika Benki, lakini kama alivyosema msemaji mwingine, anasema kwamba *charges* ya hela katika Benki imekuwa ni kubwa mno kiasi ambacho wanafanya hata hao watu ambao walikuwa na nia nzuri ya kutaka kuingiza hela kwa njia nzuri au kutoa hela kwa njia nzuri, lakini wanalazimika kufanya ujanja kwa sababu Benki nazo zina-*charge* hela nyingi sana. Mfano mmojawapo, ukichukua hela katika Benki, ukichukua hela nyingi zaidi au Shilingi milioni 20, Shilingi milioni 30, makato yake ni makubwa mno kiasi ambacho kinafanya hata watu wengine ambao wana pesa wanalazimika kutunza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbeya liliungua soko kubwa sana pale Mwanjelwa, hela ambayo walikuwa wamesema pale, wengine wameunguziwa Shilingi milioni 200, Shilingi milioni 300, Shilingi milioni 400. Unaanza kuuliza, kwa nini hawa watu hawaweki hela kwenye mfumo wa Benki? Hii ni kwa sababu *charge* ya Benki kwa ajili ya wafanyabiashara imekuwa ni kubwa sana au kwa ajili ya hela ambazo zinatoka au zinatolewa imekuwa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwamba gharama za Benki ambazo wana-*charge* kwa watu ambao wanataka hela au wanataka kutoa hela imekuwa ni kubwa mno kiasi ambacho inawafanya hawa watu ambao wangekuwa na nia nzuri, kuweza kutafuta njia za panya na kuweza kusafirisha hela. Kwa hiyo, naomba sheria hii ijaribu kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sheria bila kanuni zake pia haifanyi kazi. Sasa sheria imewekwa na nimeona hapa Bungeni tumetunga sheria nyingi sana, lakini nafasi ya kuulizia kwamba: Je, Kanuni zake ziko wapi? Inakuwa ni finyu sana. Kwa hiyo, naomba kwamba sheria hii ambayo sasa inatungwa na tunapitisha, mimi naiunga mkono kwa asilimia 100. Naomba kanuni zake ziwe *in place* haraka sana ili iweze kufanya kazi. La sivyo, itakuwa tunafanya kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu ambao tunatoka mipakani, tunaona jinsi ambavyo pesa nyingi zinavyoingia. Zinaingia pesa nyingi kutoka maeneo mbalimbali. Wafanyabiashara wanafanya kazi hiyo, kuna watu ambao kazi yao ni kuingiza hela hivyo hivyo tu. Lakini sheria ya kuwabana ilikuwa ni ndogo sana. Hebu fikiria, mtu anaiba ng'ombe anafungwa miaka saba, lakini mtu anayeingiza mabilioni ya fedha anafungwa miaka mitatu au miaka michache namna hii. *Fairness* iko wapi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba hii sheria iwe ni sheria ambayo kwa kweli inafanya kazi kwa uhakika, kuhakikisha kwamba mtu yeyote atakayepatikana anatorosha hela, adhabu yake iwe ni kali sana. Kama walivyosema wazungumzaji wengine, lazima tuweke katika *percentages* kwa sababu mtu anaweza kuchukua mabilioni ya pesa, wewe ukasimamia kwenye Shilingi milioni 500 au milioni ngapi. Ni hela ndogo sana. Kwa hiyo, naomba kwamba tuweke katika *percent*. Mtu ameiba Shilingi bilioni ngapi, atakatwa Shilingi bilioni kadhaa. Haiwezekani mtu anaiba ng'ombe anafungwa miaka saba, halafu huyu afungwe miaka mitatu. Haiji! Kwa hiyo, hilo ndilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kingine ambacho ninaomba nichangie ni kuhusu *TRA*. Kuna hela nyingi sana jamani zinazubaa, ziko nje huko, zingetakiwa zilipe kodi. Kwa bahati mbaya utamaduni wa Mtanzania kulipa kodi umekuwa ni mdogo sana. Anakimbia! Wenzetu Ulaya kulipa kodi ni hiari. Anakwenda kwa hiari, maana hawezi kuiba. Sisi hapa unatafuta kila njia. Kuna mianya mingi sana ambayo watu hapa hawalipi kodi. Watu wanaagiza *spare*, wanaagiza nini, kila kitu huko Ulaya, lakini kodi hailipwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba *TRA* kuwe na kitengo maalum cha kufanya utafiti kwenda mpaka huko chini na juu na kila mahali, kazi yao iwe ni kuangalia kwamba: Je, kodi ambayo inatolewa ni sahihi au siyo sahihi? Hii nchi ina hela nyingi sana. Kama kweli tungedhamiria kila mmoja akawajibika kutoa kodi, nafikiri bila shaka tungekwenda mbali zaidi kuliko hapa tulipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ndugu zetu wa *TRA* kuhakikisha kwamba kunakuwa na kitengo maalum ambacho watashirikiana na watu kadha katika *system* kuhakikisha kwamba wanatafuta mbinu zote za kutafuta hela ambayo mtu analazimika kulipa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nataka kusema hapa ni wizi katika benki. Huko *South Africa* na nchi nyingine Kusini mwa Afrika, mfumo wao wa kujenga majengo yao ya benki, hapa miaka michache nyuma ilitokea wakati Awamu ya Nne inaingia katika *power*, kulikuwa na wizi mkubwa sana katika benki. Watu wanaingia, wanafumua Benki na bunduki, lakini ile *design* ya nyumba tulizonazo za benki imekuwa tofauti na wenzetu huko Kusini. Huko Kusini unaingia, kunakuwa na mtu mmoja tu anafungua mlango kule ndani, anaingia mtu mmoja mmoja.

Kwa hiyo, namna ya kuweza kuiba inakuwa ni ngumu sana kwa sababu unapoingia, unaingia peke yako, ni kama *traffic lights*, inakupa *green light*, kwamba ingia na hujui ni nani anayefunga mlango ule.

Sisi hapa mtu anaingia kiholela, ndiyo maana wizi ulikuwa ni mkubwa sana, ingawa sasa hivi kidogo umepungua. Kwa kweli tunamshukuru Mungu kwa sababu hapo nyuma kwa kweli, hatujui, labda wanakwenda kufanya semina nyingine namna ya kuingia tena. Lakini, ni vizuri tuanze kufikiria namna ya kuweza kuweka benki zetu kama wenzetu wanavyofanya huko Kusini mwa Afrika au hata Ulaya ambako mtu anaingia kwa mahesabu kweli kweli. Hata ukiamua kwamba unataka kuiba pale, uwe umeshafanya

kazi nzito na ngumu sana, maana siyo unaingia kiurahisi, unaingia tu mara moja, unapiga bunduki yako, watu wameshatoka. Paa! Unaiba hela. Lakini kwa wenzetu ni vigumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *South Africa* wamedhibiti kweli kweli! Mimi nakumbuka siku moja nasafiri, nimeingia benki, nimeingizwa peke yangu pale. Lakini bahati mbaya nikiwa nataka kutoka nje, *bus* inaondoka inataka kuniacha. Namwambia jamaa, nifungulie mlango kwa sababu siwezi kufungua, siwezi kutoka kama tunavyotoka katika benki zetu hapa. Kule kunakuwa na utaratibu maalum wa kudhibiti hata ujenzi wa majengo ya benki zetu hizi, kuzuia watu wasiingie hovyo na kuanza kuiba hela mle ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nafikiri Muswada huu umekuja mahali pake. Ninachoomba, kama walivyosema wenzangu, ni kuhakikisha kwamba kanuni zake zinaanza kufanya kazi haraka sana ili kuwe na *limit*, ni shilingi ngapi utatoa hela nje. Kuingiza hatuwezi kusema, maana zinaingia. Lakini kutoa, mtu anakwenda kuomba hela benki ajue kwamba ni Shilingi ngapi anatoa. Kama ni Dola milioni 10 au chini ya hapo, basi sheria iseme wazi ili kuweka usalama mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zetu hizi ndogo zinazoendelea, kwa kweli zinaathirika sana na wizi wa pesa kama hizo. Wenzetu wanajaribu kudhibiti, lakini sisi hapa bado tunaendelea. Ninaomba tujitahidi kuhakikisha kwamba kwa kweli tunafuatilia hii sheria na kanuni zake zinatungwa haraka sana iwezekanavyo. Ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimefarijika sana kuona kwamba sheria hii imeweka wazi, ina uwezo wa kupata taarifa za benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika benki zetu hizi tulizonazo, mtu anaweza kuwa kafungua akaunti yake ana Shilingi milioni mbili, Shilingi milioni tatu, *suddenly* ile akaunti inakuwa na Shilingi milioni 10 au milioni 100. Lakini kwa kuwa benki ni biashara, hawamwulizi zile pesa zimetoka wapi au amezipata kwa njia gani. Kwa hiyo, kuwepo na sheria hii kutaweza kuzuia hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuna *transfer*. Inakuja *transfer* kutoka nje, *amount* kama ya milioni *200 USD*. Lakini, ikija hapa benki, yule mteja haulizwi hizi pesa zimetoka wapi? Zinaingia kwenye akaunti moja kwa moja. Ilikuwa sharti kupata barua ya Mahakama tu ndiyo unaweza kumwuliza mteja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kuwepo sheria hii, mimi nimefarijika sana kwa sababu itazuia kuingiza pesa chafu. Lakini, hapo hapo, siyo mwende kupata taarifa tu, wale *bankers* pia wakiona hapa pana harufu ya pesa chafu, watoe taarifa, ziwe zinakwenda huku na huku, siyo mpaka waje waulize kwamba kuna pesa zimekuja haramu au vipi. Lakini iwe kazi yao hao *bankers* wao kufuatilia kila wakati. Wakimwona mtu kaingiziwa pesa nyingi hawajui za kazi gani, waiarifu *FIU*, siyo mpaka wao waje waulize hizi pesa huyu mteja kazipata namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sheria hii imeweka wazi hizi pesa chafu zitakapopatikana tu zifunguliwe akaunti benki. Mimi napendekeza kama ilivyopendekeza Kamati, zifunguliwe akaunti Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu sheria hii imeweka wazi, hawa ma-*Intelligence Officers* wao ni kazi yao kutunza siri, inajulikana wazi. Lakini sheria hii tayari imeshaweka wazi, yeyote atakayetoa siri, atapata adhabu kali. Hii kuna sababu iliyojitokeza hata ikawekwa wazi kwa sababu hawa ma-*Intelligence* waliowekwa kuchunguza haya mambo, wanapokea pesa, halafu wanaharibu ushahidi. Kwa hiyo, hii sheria imewekwa wazi ili kuwakumbusha na kuwafunga wasiweze kufanya mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kuhusu adhabu, mimi nasema adhabu iangaliwe, isiwe Shilingi milioni 500. Adhabu hiyo ni ndogo sana kwa sababu wanaofanya mambo hayo ni watu wanaokuwa na *billions of shillings*. Mtu mwenye pesa kidogo kama hizo, hawezi kufanya mambo kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia nachangia kidogo katika sheria hii kwamba elimu ya kutosha itolewe kwa wananchi ili wajue sheria hii inambana mtu gani. Kwa sababu hapa ki-*finance* mpaka kipite kifungu cha pesa ndiyo sheria hii inapofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kidogo hapa nataka kugusia kwamba sheria zetu kila siku zinatungwa, lakini matokeo yake hazifuatwi. Kwa hiyo, nataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri, sababu gani zimemfanya aweze kuchukua uamuzi wa kubadilisha baadhi ya vipengele vya sheria hii? Kuna kitu kimejitokeza hapa huwezi tu ukakurupuka ukasema unaongeza vipengele. Kwa hiyo, naomba atupe sababu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, huyu Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa nini awe Mjumbe wa Bodi hii? Maana hatachunguza huku, na kule pia inamsubiri yeye. Hizi taarifa nahisi kama zitapotoshwa. Kwa hiyo, nataka nijue kwa nini Mkurugenzi wa TAKUKURU ni Mjumbe wa Bodi? Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru sana Mheshimiwa. Kwa vile walioomba kuchangia wameshamalizika, naomba sasa nitoe nafasi hii kwa Naibu Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Pereira Silima atoe mchango wake kwa dakika 15, baadaye mtoa hoja aje kuhitimisha hoja. Mheshimiwa Pereira karibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Fedha - Mheshimiwa Mustafa Haidi Mkulo, wakati akiwasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Udhibiti wa Matumizi ya Fedha Haramu ya mwaka 2012 *(The Ant-Money Laundering Act, 2012)* kwa kuzungumza hapa Bungeni na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuchangia baadhi ya hoja kama ifuatavyo:-

Kulikuwa na hoja kwamba: Je, marekebisho yaliyotolewa katika Muswada huu yatatosha kutatua matatizo yaliyojitokeza?

Kwa kweli, kwa kiasi kikubwa mapendekezo ya Muswada huu yamezingatia upungufu uliojitokeza na ambao ulionekana wakati wa utekelezaji wa Sheria ya mwaka 2006, ukiacha ubinadamu, marekebisho haya yakipitishwa na Bunge hili yatasaidia kwa kiwango kikubwa kuondoa matatizo yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mwaka 2006 mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja kwamba ni vema tukatoa elimu ya kutosha ili Watanzania waongeze matumizi ya hundi, *credit card, traveller check* na kadhalika. Huu ni ushauri mzuri ambao umeanza kufanyiwa kazi lakini tutaendelea kutoa elimu ili suala hili liimarike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine kwamba tuangalie utaratibu wa kutoza kodi kwenye fedha haramu na baadaye kesi kuendelea kama ilivyo katika baadhi ya nchi zilizoendelea kama Marekani na tuangalie faida na hasara zake kwa uchumi wa Tanzania. Huu nao ni ushauri mzuri ambao tutauchukua na kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na hoja kwamba Kamati ya Kitaifa ya Ushauri wa Fedha Haramu ijumuishe mjumbe kutoka Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Kamati ya Kitaifa ya Watalaam ya Ushauri wa Fedha Haramu imeundwa na wajumbe wenye utaalam wa masuala ya fedha haramu na ufadhili wa ugaidi. Aidha, Sheria imetoa mamlaka kwa Kamati kujumuisha wajumbe wengine wenye utaalam kuhusu suala linalojadiliwa. Endapo mjumbe kutoka Jeshi la wananchi atahitajika, Kamati na Sheria imetoa uwezekano wa kumwalika na kushiriki katika masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja iliyotolewa kuhusu suala la kabla ya kumshtaki mtu ambaye amefanya kosa chini ya Sheria hii ambaye si Mtanzania na kulikuwa na wasiwasi kwamba ikitakiwa *consent* ya *DPP* itakuwa ni tatizo. Nafikiri kwenye Sheria zetu za nchi, hili ni jambo ambalo hatuwezi kulikwepa labda tuamue kubadilisha Sheria nyingine za nchi, lakini kama tulivyo sasa suala hili itabidi lifanyike. Kubwa hapa ni kwamba huyu ambaye tunamshtaki atakuwa amefanya kosa kwenye nchi nyingine kwa hiyo sisi baada ya kupata idhini ya *DPP* ndiyo tunaweza tukafanya yale mawasiliano ili kuhakikisha kwamba msaada wetu unatumika katika kumshtaki kule ambako anahitajika ashtakiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya fedha za sasa na za zamani kutumika kwa pamoja kwa maana ya sarafu, hili nafikiri ni suala lingine nje ya fedha haramu lakini nafikiri ni muhimu kuwa na noti za kubadilisha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapewa muda katika ku-*phaseout* aina moja ya sarafu ili wasianze kubabaika na kuanza kwenda kupanga foleni kwenye mabenki kwa kuogopa *deadline*. Kwa hiyo, hili jambo ni zuri na linafanyika kwa utaratibu na kila siku fedha za zamani zinapungua kwenye mzunguko na siku za karibuni tutakuwa na fedha aina moja ambazo zitatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na wachangiaji wengi sana waliozungumzia suala la Kanuni, naomba nitoe taarifa kwamba katika Sheria ambayo ilitungwa mwaka 2006 na ambayo ilikuwa inatumika kabla ya mabadiliko haya, Kanuni ilitengenezwa mwaka 2007 tofauti na taarifa ambayo imetolewa hapa na imekuwa ni taarifa ambayo watu wengi imewatia mashaka. Serikali ilikuwa makini na ilikuwa *serious* kwenye hilo na mwaka mmoja tu baada ya kupitisha Sheria ile ilipitisha Kanuni na ninayo hapa. Kwa hiyo, mtu ambaye anataka kulithibitisha hili, tutamuonesha na kwa sababu Kanuni ipo ambayo ilikuwa inatumika kwenye Sheria hii hatuoni shida wala hatuna wasiwasi kwamba tutakosa utaalam wa kutengeneza Kanuni ya haraka kwa ajili ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja pia kuhusu utunzaji wa taarifa, nafikiri Sheria imeeleza haja ya kuweka kumbukumbu. Hili pia litawekewa utaratibu mzuri sana katika Kanuni ili kuhakikisha kwamba masuala haya yanakwenda vizuri na kuhakikisha kwamba Kanuni inaeleza uwekaji wa kumbukumbu hizi unafanywaje kwa ajili ya kuhakikisha kwamba shughuli za kitengo na shughuli za nchi katika taratibu za kuhakikisha kwamba fedha haramu hazipati nafasi kuharibu uchumi zinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba kuunga mkono hoja, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Naibu Waziri, sasa naomba kumwita mtoa hoja, Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya mwaka 2012 *(The Anti- money Laundering (Amendment) Bill, 2012)* kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwatambue Wabunge hawa kwa majina kama ifuatavyo:-

Waliochangia kwa kuzungumza humu ndani ni pamoja na Mheshimiwa Dkt. Abdallah Omary Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Christina Lissu Mughwai, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Kabwe Zuberi Zitto, Mheshimiwa Jitu V. Soni, Mheshimiwa Felix Mkosamali, Mheshimiwa Dkt. William A. Mgimwa, Mheshimiwa Leticia M. Nyerere, Mheshimiwa Luckson N. Mwanjale na Mheshimiwa Amina Abdallah Amour. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni pamoja na Wabunge wafuatao:-

Mheshimiwa David Z. Kafulila, Mheshimiwa John J. Mnyika, Mheshimiwa Augustino L. Mrema, Mheshimiwa Athuman R. Mfutakamba, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Waride Bakari Jabu, Mheshimiwa Christina L. Mughwai, Mheshimiwa Eng. Ramo M. Makani, Mheshimiwa Mariam N. Kisangi, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Namelok E. Moringe Sokoine, Mheshimiwa Betty E. Machangu, Mheshimiwa David E. Silinde, Mheshimiwa Gosbert B. Blandes, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, Mheshimiwa Modestus D. Kilufi, Mheshimiwa Moshi Seleman Kakoso, Mheshimiwa Benedict N. Ole-Nangoro, Mheshimiwa Angellaj J. Kairuki na Mheshimiwa Salvatory N. Machemli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Wabunge ambao nimewasahau, naomba tu niletewe na nitawatangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi, kwa maoni na ushauri wao na pia kwa kuunga mkono Muswada. Aidha, napenda pia kutoa shukrani zangu kwa Kambi ya Upinzani, kwa maoni na ushauri wao pia, ninaahidi kwamba Serikali itayafanyia kazi maelekezo na maelezo mazuri yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi na pia Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtambue Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Naibu Waziri wa Fedha ambaye naye alichangia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nianze kujibu baadhi ya hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Hoja kadhaa zimechangiwa na Naibu Waziri, hoja ya kwanza inahusu fedha zitakazotwaliwa na Idara ya Forodha zihifadhiwe na Benki Kuu. Wizara ya Fedha inakubaliana na ushauri uliotolewa na Kamati kuhusu fedha zitakazotwaliwa na Idara Forodha kuhifadhiwa Benki Kuu, hatuna tatizo na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ilihusu Kamati ya kumshauri Rais itaongozwa na nani, tunasema kwamba kwa mujibu wa kifungu cha 5(8) cha Muswada, mara baada ya Rais kuunda Kamati hiyo ya kumshauri, utaratibu wa jinsi itakavyofanya kazi utaandaliwa na Kamati hiyo. Hatukupenda kumpa Rais madaraka makubwa mno, kwa hiyo tumeona kwamba wenyewe watakapokutana kwa mara ya kwanza watamchagua wanayefikiri kwamba awe Mwenyekiti wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu inahusu elimu kwa umma itolewe ili kuongeza tija ya utekelezaji wa Sheria, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na *National Inteligency Unit* imekuwa ikitoa elimu kwa umma na itaendelea kufanya hivyo. Kuanzia mwaka 2007-2012 wadau wafuatao walipewa elimu kuhusu masuala ya fedha haramu ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari, Watoa Taarifa *(Reporting Persons*), Mawakili wa Serikali, Mahakimu, Wahasibu, Makampuni ya Bima, Wakaguzi na Wasimamizi *(Regulators)*. Baada ya mabadiliko haya, tunakusudia kwamba hawa wote watapewa tena mafunzo lakini pia maeneo mengine ya wananchi yataelimishwa ili Sheria hii iweze kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutangaza pia Mheshimiwa Dkt. Fenella Mukangara, Naibu Waziri wa Habari na yeye alichangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilikuwa utayarishaji wa Kanuni chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, tunapenda kulitangazia Bunge lako Tukufu kwamba Waziri wa Fedha kupitia Tangazo la Serikali Na. 195 lililochapishwa tarehe 14 Septemba 2007, alitoa Kanuni ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu, nakala ya Kanuni hiyo nitaiwasilisha kwa Spika ili Wabunge wote waweze kuipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni hizo hazikubainisha viwango vinavyotolewa taarifa na msafiri anayevuka mipaka ya nchi kwa kuwa Serikali ilikuwa ikifanya mashauriano na wadau mbalimbali kuhusu suala la viwango vya fedha vinavyopaswa kutolewa taarifa kwa nchi yenye *cash base economy* kama Tanzania. Kufuatana na mjadala ndani ya Kamati ya Fedha na Uchumi na pia mjadala kama ulivyojitokeza ndani ya Bunge lako Tukufu, napenda kukuahidi kwamba Wizara yangu itahakikisha kwamba Kanuni hizi zinarejewa upya na zinatolewa mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilisema kwamba ndani ya Sheria itamkwe wazi kuwa dola elfu kumi kiwe ni kiwango ambacho msafiri anatakiwa kutoa taarifa anapoingia na kutoka nje ya nchi. Napenda kusema kwamba utaratibu uliobainishwa ndani ya Sheria wa kutamka kiwango husika kupitia Kanuni, tunaona uendelee ili kuruhusu *flexibility* kutokana na mabadiliko ya kiuchumi ambayo yanatokea hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa Tanzania unabadilika kwa haraka sana, tunaweza tukaweka dola elfu kumi leo lakini baadaye ikaja ikaonekana kwamba dola elfu kumi hazitoshi au kubwa mno. Kwa hiyo, tungependa kuwe na *flexibility,* kiwango kibaki kwenye Kanuni na kwamba kama mambo yakibadilika tunaweza kubadilisha tukaweka kiwango kingine kuliko kuweka kiwango ndani ya Sheria ambayo inaweza kusababisha kurudi Bungeni kubadilisha Sheria ili uweze kuweka kiwango kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu utekelezaji wa Sheria kwa makini, tunasema tangu kutumika kwa Sheria hii, utekelezaji wake umekuwa ni wa makini na wa uadilifu mkubwa na hivyo Serikali itaendelea kutekeleza Sheria hii kwa umakini kwa kufuata utaratibu ili kuepuka usumbufu kwa wananchi katika shughuli zao za kibiashara. Ikiwa mabadiliko haya yatapitishwa, tutahakikisha kwamba kule kote kulikokuwa na upungufu kutapewa nguvu na kwa hiyo utekelezaji wake utakuwa mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu mgongano wa kimawazo kati ya mamlaka za usimamizi na watoa taarifa pale ambapo mamlaka ya usimamizi ni mtoa taarifa pia. Tunasema kwamba hakuna mgongano wa mawazo kati ya mamlaka za usimamizi na watoa taarifa kwa kuwa mamlaka za usimamizi hutoa taarifa kwa kitengo cha *Financial Inteligence Unit* pale mamlaka hizo zinapofanya ukaguzi na kubaini mambo yanayohusiana na fedha haramu na ufadhili wa ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu Kitengo cha *Financial Inteligence Unit* kisiwekwe chini ya Wizara ya Fedha, hili ni suala la kisera linahitaji kufanyiwa kazi. Kwa nchi zote 15 ambazo ni wanachama wa *ECAMLAG*, Kitengo hiki kiko chini ya Wizara ya Fedha. Tuseme tu kwamba tunalipokea wazo hili litafanyiwa kazi na kama ikibidi kwamba Kitengo hiki kiondolewe chini ya Wizara ya Fedha basi utaratibu muafaka utaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu Kamati ya kumshauri Rais kumuondoa Kamishna wa *Financial Inteligence Unit* madarakani usihusishwe wateuliwa na Rais. Kamati ya kumshauri Rais kumuondoa Kamishna wa *Financial Intelligence Unit* madarakani itaundwa na watu wenye dhamana na nyadhifa zao na watakaotumia busara katika kumshauri Rais kulingana na aina ya tuhuma itakayokuwa inamkabili Kamishna wa *Financial Intelligence Unit.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilihusu uhalali wa Benki Kuu kuwa msimamizi wa masuala ya fedha haramu kwa mabenki, Benki Kuu ni taasisi iliyoundwa kisheria kusimamia shughuli za mabenki, hivyo Benki Kuu iko katika nafasi nzuri ya kubaini matatizo yanayojitokeza wakati wa ukaguzi wa mabenki hayo.

Aidha, makosa yanayofanywa na Watumishi wa Benki Kuu katika utendaji wa shughuli zao ambayo ni makosa ya jinai yanapaswa kushughulikiwa kwa utaratibu wa Sheria dhidi ya watu hao kulingana na makosa yaliyofanywa pasipo kuhusisha Benki Kuu kama taasisi. Tunasema hata hivyo hili nalo ni suala la Kisera, Wizara italiangalia na kuona nini cha kufanyika lakini tunasema kwa sasa kwa sababu Sheria ya Benki Kuu inaruhusu kazi hiyo ifanywe na Benki Kuu, ni muhimu Benki Kuu ikaendelea kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizojitokeza ni nyingi zile ambazo Naibu Waziri na mimi hatukuweza kuzijibu moja kwa moja tutaziandalia maandishi na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge pamoja na haya yote ambayo tumeyajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako lipitishe Marekebisho ya Sheria hii ili kuiboresha, kuipa meno iweze kufanya kazi mahiri ya kudhibiti fedha haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu wa Mwaka 2012 *(The Anti – Money Laundering [Amendment] Bill, 2012)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati*

*ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Ibara ya 3, inahusu taasisi za usimamizi kwa maana ya *regulators* na mapendekezo yangu ni kwamba miongoni mwa *regulators* kuingizwe *Registrar of Political Parties* kwa maana ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Sababu ya mapendekezo yangu ni kwamba hivi karibuni palifanyika utafiti wa Taasisi ya *Africa Power and Politics* ya *The Political Economy of the Investment Climate in Tanzania.* Katika utafiti wao walibainisha kwamba Tanzania inakabiliwa na changamoto ya masuala ya fedha haramu ikiwemo nyakati za uchaguzi na fedha haramu wakati wa michakato ya kisiasa. Sasa Sheria hii haijaweka Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa miongoni mwa *regulators*. Tatizo kubwa sana ambalo utafiti huu wa Juni, 2011 uliainisha ni dhana waliyoiita *state capture* kwa maana ya dola kutekwa. Sasa hili ni tatizo kubwa zaidi, madhara ya fedha haramu yakiingia kwenye uchaguzi ni makubwa zaidi kwa sababu yanaathiri upatikanaji wa viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeshauri kwamba hilo pendekezo liweze kukubaliwa ili liendane vilevile na Sheria zetu zingine mbili ambazo Bunge hili limezitunga. Moja, ni Sheria ya Vyama vya Siasa ambayo kifungu cha 13 na 14 kinamtaja Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa chombo ambacho kitahusika na kupokea taarifa za Vyama na taarifa za fedha na matumizi ya fedha. Vilevile Sheria ya Fedha za Uchaguzi *(Election Expenses Act),* kifungu cha 3, 4 na 5 na vyenyewe vinamtaja Msajili wa Vyama vya Siasa. Sasa ili kuepusha huko mbele tunakokwenda kwenye chaguzi zinazofuata na kwenye Vyama vya Siasa kujitokeza kama masuala ya fedha za *EPA*, Meremeta, Kagoda, *Deepgreen, Tangold* na mengineyo kutumika kwenye kampeni za kisiasa hususani za Chama Tawala CCM basi hiki kifungu kiingizwe ili Vyama vyote viweze kutoa taarifa husika ili tupunguze fedha haramu kwenye uchaguzi. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Ibara ya 3 ya Sheria ya Asili pamoja na mabadiliko haya utaona kwamba wale *regulators* wanaotajwa pale *essentially* ni wale wanaoshughulika na mambo ya fedha. Mapendekezo ambayo Mheshimiwa Mnyika anapendekeza yatatusaidia pia, ni kweli kwamba yanaweza kusaidia kwenye matumizi ya fedha za uchaguzi kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi. Kwa hiyo, sina matatizo nayo. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja Marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Nasimama kwenye eneo ambalo naamini ni vizuri Waheshimiwa Wabunge wote tukalifahamu. Kuanzia ukurasa wa 4 na wa 5 wa Muswada, eneo hili kwenye (f) (i), (g) ambapo tunatoa tafsiri ya *Reporting Person* kwa maana ya kuipanua, inaanza kuainisha pale *Pension Funds Managers* utaiona kwenye *schedule of amendment* lakini inajumuisha sasa na *Savings and Credit Cooperative Societies* ambayo ni *SACCOS*. Sasa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi tuliishauri Serikali na ikatuelewa kwamba ukitaka kuingiza *SACCOS* kama *reporting person,* unachotakiwa kufanya hata kama unaifanya kwa nia njema kwa sababu wanashughulika na masuala ya fedha, kama alivyosema Mwanasheria Mkuu, utakuwa umeingiza na Vyama vya Kuweka Akiba na Kukopa ambavyo havisimamiwi na Benki Kuu kwa sababu yako makundi, kuna *Microfinance* na yenyewe inaanzia kuanzia shilingi 800 kwenda juu halafu Vyama vya Ushirika vinavyosimamiwa na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika. Sasa tukawashauri tui-*capture* hiyo na wamejitahidi wakachukua mapendekezo ya Kamati wameingiza *Microfinancing Institutions and Companies* sawa kabisa na ndio sheria inavyosema lakini bahati mbaya mimi nataka kupenda kuamini kwamba hii bahati mbaya wamerudia tena yale maneno ambayo yalikuwa yanatusumbua sisi ya *Savings and Credit Cooperative*. Sasa hii kwa maana hii sasa hata Vyama vidogo vya Ushirika kule Mwasinasye, Izagoyo, Lugulu, Urombola ambavyo hata kujaza fomu zao wenyewe wana shida, wanatakiwa wawe *reporting person*. Tukasema kwamba unapotaka kutekeleza Sheria yoyote lazima iangalie mazingira ya nchi. Kwa maana hiyo, napenda hayo maneno *Savings and Credit Cooperative* yafutwe kwa sababu hayana maana ambayo ilikusudiwa. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilikubali wakati wa Kamati nadhani katika kufanya mabadiliko ilisahau kuifuta, hatuna tatizo, tunaiondoa hiyo *SACCOS*.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 5

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Mkosamali kwenye ombi lako umenukuu Kanuni ya Kudumu ya mwaka 2012, kwa hiyo, ombi lako ni batili na nilikutaka utoe maelezo kwa Kanuni hii ambayo umeinukuu ambayo haipo.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *typing error* tu naomba iwe 2007.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali endelea.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nielezee, mapendekezo yangu ni kwamba, Kamishna huyu akishateuliwa na Rais, nimependekeza kwamba tuongeze kifungu pale awe anakuwa *approved* na Bunge hili Tukufu kwa sababu ya kazi zake. Ukisoma kwenye Sheria yenyewe inayobadilishwa, utaona yeye ndiye ambaye watu wanaripoti kwake, wanaangalia mashtaka yapelekwe wapi, ana kazi kubwa za kuhakikisha kwamba Sheria hii inatekelezwa. Kwa hiyo, nikashauri kwamba akishakuwa *appointed* basi aje kuwa *approved* na Bunge kwa sababu ana majukumu makubwa, ana *deal* na *transaction* kubwa na wizi ambao ni mkubwa sana. Kwa hiyo, mapendekezo yangu ni hayo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mtu pekee anayethibitishwa na Bunge ni Waziri Mkuu. Kwa mujibu wa Katiba hiyo, labda tutakapoingia kwenye mchakato, tutakuwa na Maafisa wengine kama *Attorney General*, Majaji, kuweza kuthibitishwa na Bunge lakini kwa sasa utaratibu tulionao ni huu wa kumthibitisha Waziri Mkuu peke yake. Napendekeza kwamba Mheshimiwa Mkosamali aelewe msingi huo wa Katiba na aondoe mapendekezo yake. Ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kifungu cha Sheria yenyewe siyo Muswada, Sheria inayobadilishwa, majukumu haya ni mazito sana na kama nia ya Serikali ni kupata Katiba Mpya, tuanze na Sheria hii, tunampa mtu mamlaka makubwa sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felix Mkosamali, kwa sababu suala hili ni la Kikatiba basi wakati Taifa linapojiandaa kuandika Katiba Mpya, naomba basi tuchukue suala hili kwenye Marekebisho ya Katiba Mpya ili tuone kama inafaa kufanya marekebisho. Kwa hiyo, naomba tuendelee.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo Juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10

*Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 12
Ibara ya 13
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 16

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 17

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 19

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nimependekeza kwamba adhabu iongezwe kwa sababu makosa mengine ni makubwa sana, huwezi kumfunga mtu miaka mitatu. Kwa hiyo, napendekeza iwe kuanzia miaka mitatu mpaka kumi, siyo chini ya miaka mitatu, ndio pendekezo langu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu hizi zinazopendekezwa na Mheshimiwa Mkosamali haziwiani na adhabu ambazo ziko kwenye Sheria yetu ya jumla ya *Penal Code* na zinaweza kuchukuliwa kama ni adhabu ambazo zinakweza na kwa hiyo kuwa kinyume cha Ibara ya 13 ya Katiba ya Nchi. Namwomba Mheshimiwa Mkosamali akipenda aondoe pendekezo lake.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, haya makosa ya *money laundering* ni makosa ambayo ni makubwa sana. Kuyawekea kifungo kidogo cha miaka mitatu ni kuwafanya watu waendelee kufanya uhalifu huu. Kwa hiyo, mimi napendekeza kabisa kwa nia nzuri, adhabu hizi ziongezwe, mnavyoziacha hivi, watu watazidi kufanya *money laundering*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa nia njema ya Mheshimiwa Mkosamali lakini hatuhitaji kutunga Sheria kwa hasira. Adhabu ya kifungo hata kama ni mwaka mmoja au siku moja inatosha. Ukiangalia Sheria ilivyo sasa hivi, muda huu wa miaka mitatu kwa kweli unatosha na ni *proportionate* na adhabu zilizopangwa kwenye Sheria yetu ya Mgao wa Adhabu yaani mgao wa fedha na mgao wa kifungo. Kwa hiyo, napendekeza Mheshimiwa Mkosamali kwa sasa twende na adhabu inayopendekezwa na kwamba aondoe adhabu ambayo yeye anapendekeza.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Niko kwenye suala hilohilo la adhabu lakini kwa hoja tofauti. Kwanza, ningeomba marekebisho ya makosa ya uchapaji maneno *three times* yawe *deleted* kwenye (a) na (b).

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo nalipendekeza ni kwamba, ninachopendekeza ni kwamba kwenye kifungu kile cha 28B(a), imesemwa kwamba atakayefanya makosa haya atatozwa faini ya kiwango kisichozidi milioni 500 na kisichopungua milioni 100 au kifungo cha muda usiozidi miaka mitatu, lakini makosa haya wakati mwingine yanahusiana vilevile na masuala ya fedha ama mali. Kwa hiyo, pendekezo langu, ningeomba kuongezwe maneno:-

*'or be ordered to pay the amount equivalent to the total amount of money involved or market value of property whichever amount is greater'.*

Kwa upande wa Taasisi vilevile iwe hivyohivyo:-

'*or be ordered to pay the amount equivalent to the total amount of money involved or market value of property whichever amount is greater'.*

Ili pamoja na kifungo, pamoja na faini ya kawaida misingi ya faini ikokotolewe, Mahakama iwe na *option* ya kukokotoa adhabu kwa kuangalia kiwango cha fedha kilichokuwa *involved* kwenye kosa lenyewe ama kiwango cha mali ambacho kimehusika katika hayo masuala ya uhamishaji wa fedha haramu. Ni vyema jambo hili likazingatiwa kwa sababu makosa haya ya matumizi ya fedha haramu yanakwamisha sana harakati za vita dhidi ya ufisadi, yanachangia kwenye mfumuko wa bei na yanachangia vilevile kwenye kuporomoka kwa shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna yoyote ile, tukiacha bila yule anayefungwa ama anafungwa au bila yeye vilevile kuhisi maumivu kwenye mali ama kiwango cha fedha kilichohusika na makosa hayo, itawafanya hawa wakosaji wayafanye haya makosa wakijua kwamba nitakwenda jela, nitafungwa miaka hiyo michache, nitatoka na nitaendelea na shughuli zangu kama kawaida. Kwa hiyo, naomba hilo pendekezo lizingatiwe. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno hayo yanavutia sana lakini ukisoma Sheria ilivyo yaani adhabu zinazotolewa kwenye Sheria, Sheria yenyewe ya *Money Laundering* ukiangalia kifungu cha 12 na cha 13, makosa hayo na adhabu ambazo sisi tunapendekeza, kifungu kile cha 28B (1)(a) kinasema kwamba, *"in case of an individual person, be liable to a fine not exceeding five hundred million shillings",* sio kiwango kidogo hicho, "*and not less than one hundred million shillings or imprisonment for a term not exceeding three years"*. Kama nilivyosema mwanzoni, hii miaka mitatu inaonekana midogo, lakini ukiangalia kwenye ulinganifu, ukianzia kwenye *Penal Code* na ukienda pia kwenye *Cap.1* utaona kwamba hii adhabu ya fedha na miaka inawiana. Napendekeza Mheshimiwa Mnyika akubaliane na mapendekezo hayo yaliyoko kwenye Muswada na kama tutakapokuwa tunatumia Sheria kukiwa na haja ya kuongeza adhabu hiyo basi tuongeze.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya ulinganisho haina msingi kwa sababu Bunge hilihili lilitunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na ikaweka adhabu kwenye masuala ya utoaji wa elimu ya Mabadiliko ya Katiba na ukusanyaji wa maoni ya kifungo cha kati ya miaka mitatu mpaka saba. Kwa hiyo, sasa kama mtu anajihusisha na biashara ya fedha haramu anafungwa miaka mitatu, halafu Sheria nyingine kifungo ni kikali zaidi, hiyo *Penal Code* sidhani kama inatumika katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa turudi kwenye hoja ya msingi na nashukuru *AG* amerejea Sheria yenyewe ya msingi na ningemwomba *Attorney General* aende kwenye Sheria yenyewe ile iliyotungwa mwaka 2006, kifungu cha 13B kinazungumza kuhusu makosa haya na *spirit* ya kifungu hiki, hili wazo la kuingiza *value* ya *property* ama kuingiza *property* kama sehemu ya adhabu yaani kuchukuliwa kwa mali ama kutozwa faini kulingana na thamani ya mali si geni. Kifungu hiki cha Sheria kinasema na nanukuu, tena ni pendekezo langu, nimepunguza kidogo kiwango cha adhabu kilichopo kwenye Sheria hapa, kinasema:-

*"be ordered to pay the amount equivalent three times the market value of property whichever amount is greater".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa Sheria ilivyo sasa imetoa *room* ya mtu kuweza kutozwa/kupewa hukumu sawasawa na kiwango cha mali mara tatu ya ile mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini bado nimeleta mapendekezo haya na ningemwomba Mheshimiwa *AG* kwa kweli ayakubali, kifungu cha 13 cha Sheria yetu ya sasa kinahusu makosa yanayohusiana na kukiuka kifungu cha 12, Mheshimiwa AG ningeshauri unisikilize. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI**: Endelea!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba AG anisikilize. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa Mnyika, naomba uendelee.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasema, kifungu nilichokinukuu cha 12 kinahusiana na makosa ya *property* ambayo yamekuwa *specified* kwenye Sheria, lakini kifungu tunachokijadili sasa na ni muhimu sana kikakubalika kinahusu *general penalty* kwamba mtu anaweza akafanya kosa la kuivunja Sheria hii lakini haijatajwa kwenye kifungu cha 12, sasa kifungu hiki kinatumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema *AG* akakubali tu kwa sababu kwenye hotuba ya Kambi ya Upinzani tumeeleza kiwango cha fedha haramu ambacho kinahusika mpaka inafika bilioni 150, kuna watu kwenye taarifa...

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa inatosha, umeeleweka.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafikiri *scheme* iliyoko kwenye kifungu cha 12 na kifungu cha 13 *they are different* na ndiyo maana sisi tunapendekeza adhabu ile kutegemea na zile *schemes* na ni vizuri kufahamu hivyo. Sasa sijui nitaeleza kwa lugha gani nzuri zaidi ambayo itamfanya Mheshimiwa Mnyika aelewe lakini *scheme* ya *twelve* ambayo ni *prohibition of money laundering* na *scheme* ya *thirteen* ambayo ni *penalties for acts of money laundering, these are different* na ndiyo maana sisi tumetoa hayo mapendekezo, hatusemi kwa sauti kubwa kama wewe lakini ni kwamba *scheme* zile ni tofauti. *(Makofi)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati
ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu ya Mwaka 2012 *(The Anti-Money Laundering (Amendment) Bill, 2012)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae, Katibu!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa Spika!

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imepitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya mwaka 2012 kifungu kwa kifungu na kuukubali. Kwa hiyo, naomba kutoa hoja kwamba taarifa hiyo sasa ikubaliwe rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono, sasa nitawahoji, wanaoafiki waseme ndiyo!

**WABUNGE FULANI:** Ndiyoo!

**MWENYEKITI:** Na wasioafiki waseme siyo!

**WABUNGE FULANI:** Siyo!

**MWENYEKITI:** Naamini walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Katibu, *AG, AG! (Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwona Mheshimiwa Ole-Sendeka amesimama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu, hoja baada ya kuwa Spika ameshawahoji Wajumbe na kuiafiki, hakuna tena Mwongozo baada ya hapo. Kwa hiyo, Katibu! *(Makofi)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa*
*Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI**: Waheshimiwa, kama Kanuni zetu zinavyoelekeza, Muswada huu umepitia hatua zote na sasa nina furaha kutangaza kwamba Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Kudhibiti Matumizi ya Fedha Haramu umepitishwa na Bunge hili Tukufu tarehe 3 Februari, 2012 na kwa vile kazi ambazo ziko Mezani katika *Order Paper* zimemalizika, kabla ya kuahirisha Bunge hili, nina matangazo yafuatayo:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Margaret Sitta anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hii mara baada ya kuahirisha kikao hiki wafike katika kikao kifupi kitakachofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa B.

Pia Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anaomba niwatangazie Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi wakutane mara baada ya kikao hiki, Ukumbi wa Msekwa.

Kwa hiyo, napenda kuwatakia *weekend* njema lakini vilevile...

**T A A R I F A**

**MBUNGE FULANI:** Taarifa!

**MWENYEKITI:** Haya taarifa. Mheshimiwa kwanza hebu kaa. *(Makofi)*

Mwenyekiti au Spika anaposimama kwenye Kiti hiki, tunaomba tuzingatie utaratibu wetu kwamba unaketi chini, sasa naomba utoe taarifa yako Mheshimiwa Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza bila kuathiri mamlaka uliyopewa na Kanuni ya 5 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, nimesimama kuomba Mwongozo wako kwa sababu umepewa Mamlaka yote hapo kwenye Kanuni ya 5 lakini na wewe ni binadamu. Tulipokuwa tunashughulikia sehemu ya mwisho ya mabadiliko yaliyowasilishwa hapa ya kifungu cha 19, ulipokuwa ukihoji, nataka uweke *record* vizuri kwa ajili ya *Hansard*. *(Makofi)*

Baada ya kwamba Mheshimiwa John Mnyika ametoa hoja yake, ilijibiwa na Mheshimiwa *Attorney General* na baada ya hapo kauli ya mwisho ilikuwa ya *Attorney General* na kimsingi alikuwa amekwishafanya mabadiliko kwamba hakukubaliana na mabadiliko ya Mheshimiwa Mnyika na kwa maana hiyo wakati ulipokuwa unahoji kulikuwa na utata kwa sababu ulisema kifungu kinakubalika pamoja na mabadiliko wakati mabadiliko yenyewe yalikuwa hayajapita. Tukasema ni vizuri utuwekee kumbukumbu ili haya mambo yakae vizuri kwa ajili ya *record* zilizopo. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu Bunge hili haliwezi kutunga Sheria inayokinzana na Sheria nyingine na *Attorney General* ametusaidia hapa katika sehemu ya adhabu na tukifanya hivyo, tutafanya kazi hii kwa ushabiki sio tu kwamba tutakuwa hatuwatendei haki Watanzania, tutakuwa tunamomonyoa hadhi ya Bunge lako. Tunaomba utuwekee kumbukumbu vizuri kwenye *Hansard* hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru sana, naomba tu niseme kwamba sote tunaamini kwa imani zetu, amekamilika Mwenyezi Mungu peke yake, nafuta yale maneno kwamba na marekebisho haya. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo...

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI**: Ninaahirisha shughuli hizi mpaka siku ya Jumatatu asubuhi.

**MBUNGE FULANI**: Hizo sio Kanuni!

*(Saa 1.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 6 Februari, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*